# KUCHUNGUZA MATUMIZI YA LUGHA NA DHAMIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA MWANDISHI EMMANUEL MBOGO

**SAFINIA KHAMIS ALI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo ***Matumizi ya Lugha na Dhamira katika Tamthilia Teule za Mwandishi Emmanuel Mbogo*** na anapendekeza kuwa ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

…………………………………….

**Dkt. Mohammed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

……………………………………..

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

**TAMKO**

Mimi, **Safinia Khamis Ali,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada kama hii au nyengine yoyote.

………………………….

Sahihi

………………………….

Tarehe

## TABARUKU

Napenda kuitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa, bibi Kudura Khamis Omar na bwana Khamis Ali Shauri, mume wangu bwana Shehe Abdalla Moh'd na watoto wangu Mundhir, Rahma na Munawwar .

## SHUKURANI

Kazi hii ya utafiti ni matokeo ya michango na mashirikiano makubwa baina yangu na watu wengi. Kutokana na ukweli huo, sio rahisi kuandika mchango wa kila aliyenisaidia kuikamilisha kazi hii. Kwa shauku kubwa nataka kuwashukuru wale wote ambao kwa namna moja ama nyengine wamenipa ushauri na mchango wa kitaaluma. Kwa namna ya pekee zaidi, napenda kuwapa shukrani wafuatao:

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai, uzima, afya, nguvu na fahamu katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii, DKT. Mohammed Omary Maguo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri, kunielekeza na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Msaada wake hauwezi kukisiwa wala kulipwa. Ninachoweza kusema ni kutoa shukran zangu za dhati kwa kusema Ahsante sana DKT Omary, Mwenyezi Mungu Akubariki na Akujaalie afya njema na maisha marefu yenye kheri na mafanikio mema kwako na familia yako kwa ujumla. Aaamin, Aaamin, Aaamin.

Tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengine wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa msaada mkubwa walionipatia katika kipindi chote cha masomo yangu. Walimu hao ni Sheikh, Profesa, Daktari, T.S.Y.M. Sengo, Profesa Emmanuel Mbogo, DKT. Anna Kishe, DKT. Hanna Simpasa, DKT. Zelda Elisifa, DKT. Hadija Jilala na DKT. Gress Kisasi.

Nne, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu ambayo haikuwa nyuma katika kunipatia msaada wa kihali na mali ili niweze kuifanya kazi hii kwa ufanisi zaidi hadi kufikia mwisho wa kazi hii ya utafiti, nikianzia na mume wangu mpenzi Shehe Abdalla Moh'd, watoto wangu wapenzi Mundhir Shehe Abdalla, Rahma Shehe Abdalla na Munawwar Shehe Abdalla, wazee wangu wapenzi bi Kudura Khamis Omar na bwana Khamis Ali Shauri ambae ameshatungulia mbele ya haki, nakuomba mwenyezi Mungu umpe maisha mema huko aliko. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu na mashirikiano muliyonipa katika kipindi chote kigumu cha masomo. Pia ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wapenzi wa kozi ya Uzamivu kwa kuwa nami bega kwa bega katika hatua zote muhimu za utafiti huu kuanzia mwanzo mpaka kukamilika kwake, bila ya kumsahau bi Zainab Ramadhan haji kwa michango yake iliyosaidia sana kukamilika kwa kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia matumizi ya lugha katika Tamthiliya Teule za mwandishi Emmanuel Mbogo pamoja na dhamira zilizojitokeza ndani ya utumizi huo wa lugha. Uchambuzi ulijikita katika malengo mahususi mawili ambayo ni kuchambua matumizi ya lugha katika tamthiiya teule za Emmanuel mbogo na kubainisha namna matumizi ya lugha yalivyojenga dhamira katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo. Katika kukusanya data mtafiti alitumia mbinu ya Upitiaji wa nyaraka, kompyuta, Usomaji wa makini, uchambuzi wa data zilizochambuliwa kwa kutumia maswali yaliyowasilishwa mwanzoni pamoja na mbinu ya kimaelezo katika kuchambua data. Uchambuzi umeonesha kwamba matumizi ya lugha na dhamira zilizomo ndani ya tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo zimejenga umahiri wa mtunzi pamoja na kwenda sambamba na muktadha husika kupitia utomeaji wa maneno teule, ubunifu wa hali ya juu, kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Dhamira zilizomo katika uchanganuzi wa data ni kuchanganua matumizi ya lugha yalivyotumika kisanii kwa kuisana lugha ya kiswahii na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Vile vile, utafiti umeonesha kwamba mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mtunzi kwenye matumizi ya lugha ni nyingi ikiwemo, matumizi ya lugha kwa ujumla, utumizi wa tamathali za usemi kama vile semi, misemo, methali, lugha ya picha, takriri, tanakali sauti, lugha ya ishara, tashbiha, tash-hisi, mdokezo na mubalagha. Mwishoni mwa utafiti kumetolewa mapendekezo kwa ajili ya tafiti zijazo (za baadae) kwa kupitia utanzu wa fasihi Andishi kwa matumizi ya lugha ili kulipata pengo ambalo kalikupatiwa ufumbuzi na kulitafutia ufumbuzi kwa upande mwengine wa kazi za tamthiliya ambazo ni miongoni mwa kazi za fasihi kupitia lugha kupitia vipengele vyengine vya lugha.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ **ii**

**HAKIMILIKI** ........ **iii**

**TAMKO** ........ **iv**

**TABARUKU** ........ **v**

**SHUKURANI** ........ **vi**

**IKISIRI** ........ **viii**

**YALIYOMO** ........ **ix**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

**1.0 UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 6

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 6

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti ........ 6

1.3.2 Malengo Mahususi ........ 6

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 7

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 7

1.6 Mipaka ya Utafiti ........ 8

1.7 Mpangilio wa Tasinifu ........ 8

**SURA YA PILI** ........ **9**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ........ **9**

2.1 Utangulizi ........ 9

2.2 Historia ya Tamthiliya ........ 9

2.2.1 Kabla ya Ukoloni .......... 10
2.2.2 Wakati wa Ukoloni .......... 11
2.2.3 Kipindi cha Baada ya Ukoloni .......... 14
2.3 Mapitio ya Kazi Kuhusu Mada ya Utafiti .......... 22
2.3.1 Kazi Tangulizi za Matumizi ya Lugha katika Nyanja Mbalimbali .......... 22
2.3.2 Kazi Tangulizi Juu ya Tamthiliya .......... 28
2.4 Tafiti kuhusu Lugha .......... 35
2.5 Mkabala wa Kinadharia .......... 39
2.6 Nadhariya ya Semiotiki/umatini .......... 39
2.7 Hitimisho .......... 44
**SURA YA TATU .......... 45**
**3.0 MBINU ZA UTAFITI .......... 45**
3.1 Utangulizi .......... 45
3.2 Eneo la Utafiti .......... 45
3.3 Usanifu wa Utafiti .......... 46
3.4 Kundi Lengwa .......... 46
3.5 Sampuli na Usampulishaji .......... 46
3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa .......... 47
3.6.1 Data za Upili .......... 47
3.6.2 Data za Msingi .......... 47
3.7 Mbinu za Kukusanya Data .......... 48
3.7.1 Usomaji Makini .......... 48
3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka .......... 49
3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data .......... 49

3.9 Maadili ya Utafiti ... 49

3.10 Hitimisho ... 50

**SURA YA NNE ... 51**

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ... 51**

4.1 Utangulizi ... 51

4.2 Emmanuel Mbogo ni Nani? ... 51

4.3 Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya Teule ... 54

4.3.1 Lugha ya Picha ... 55

4.3.2 Matumizi ya Semi/Misemo ... 58

4.3.3 Matumizi ya Tamathali za Semi ... 65

4.4 Matrumizi ya Lugha katika Tamthiliya ya John Okello ... 72

4.4.1 Matumizi ya Misemo ... 73

4.4.2 Methali ... 76

4.4.3 Matumizi ya Tamathali za Semi ... 78

4.5 Hitimisho ... 104

**SURA YA TANO ... 105**

**5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 105**

5.1 Utangulizi ... 105

5.2 Muhutasari wa Utafiti ... 105

5.3 Hitimisho ... 105

5.4 Mapendekezo ... 106

**MAREJELEO ... 108**

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kwa mujibu wa Mohammed (1981) lugha hubadilika na kufuata tabia, kanuni na kaida fulani kutegemea wapi inatumika au uwanja gani wa matumizi inayotumikia. Kwa hali hii lugha ya maelezo ya kisayansi itatofautiana na lugha ya kifasihi kwa sababu malengo na madhmuni ya mawasiliano na fikira na matumizi ya lugha katika kuwasilisha fikira hizo hutofautiana.

Kazi yoyote ya fasihi haina lengo la kueleza na kuwasilisha mawazo, fikra na falsafa za msanii tu, bali pia hutoa hisi za mwandishi ili kuibua hisi za hadhira yake. Pia fasihi huwa na kazi ya kufurahisha, kuipendeza hadhira na kuivutia hadhira. Mkolezo wa Riwaya, Tamthiliya na ushairi haumo katika mawazo, maoni, fikra na falsafa ya mwandishi tu, bali pia katika mpiko wa mkolezo wa lugha ya kisanaa yenye kunata ladha na utamu wa ajabu katika nafsi ya hadhira. Mwandishi hodari hujibainisha katika uzito wa mawazo yake na ufundi wa lugha yake.

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba “lugha ni chombo cha fasihi” na kwa maana hiyo ni muhimu kwa msomaji na mchambuzi wa fasihi aangalie namna lugha ilivyofinyangwa. Katika kujadili sanaa kama inavyojitokeza katika fasihi, mhakiki anapaswa kuzingatia tamathali kadhaa za usemi, na mbinu nyingine za kisanii, tamathali hizo za usemi zilivyotumika katika kazi ya fasihi na jinsi zinavyokwenda

sambamba na mbinu kama vile tashbiha, tash-hisi, jazanda, chuku, tafsida, taswira, taharuki, mbinu rejeshi, viangaza mbele na taashira.

Wamitila (2008) katika maelezo yake kuhusu matumizi ya lugha ni kwamba lugha huundwa na msamiati. 'Msamiati' hapa hautumiwi tu kumaanisha maneno magumu katika lugha bali ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Msamiati ni nyenzo ya kimsingi aliyonayo mwandishi, na nyenzo hii ina nafasi na umuhimu mkubwa katika utunzi na uandishi wake. Uwasilishaji wa ujumbe, dhamira na tasnifu yake, athari yake hutegemea msamiati wake na jinsi anavyouteua msamiati huo.

Kwa msingi huu basi, ni muhimu pia kuchunguza suala zima la uteuzi na mpangilio wa msamiati ambapo uteuzi wa msamiati unaweza pia kuhakikisha kuwa msomaji ameathiriwa na janga linalompata muhusika mkuu au laa. Vile vile, wamezungumzia tamathali za usemi, mbinu nyengine katika uchanganuzi wa matini au kazi, za fasihi, matumzi ya jazanda- jazanda za kimalezi/maelezo na jazanda na kisheria.

Kwa ujumla, matumzi ya lugha katika fasihi huwa yanachukua nafasi kubwa na iliyo muhimu ndani ya kazi ya sanaa kwani lugha na matumzi yake ni sawa na samaki na maji akiwa baharini, hii ndio nguvu ya kumfanya samaki huyo kuendelea kuishi na kuwa hai na kupata nguvu zaidi katika hali ya mazingira yake yaliyomzunguka. Hivyo basi, matumzi ya lugha ndani ya kazi ya fasihi ni suala ambalo haliwezi kuepukwa, hii si kwa kutumia lugha tu, lazima pawe na vigezo maalumu vya kutumika katika utumizi wa lugha kwa muandishi wa kazi ya fasihi na kumrahisishia msomaji au mhakiki kuweza kuvibaini vipengele hivyo muhimu ambavyo muandishi atakuwa amevitumia.

Vile vile, tunaweza kusema kwamba matumzi ya lugha yana umuhimu wake katika kuwasiliana baina ya mtu mmoja na mwengine. Kwa mfano, katika kupashana habari juu ya jambo fulani, kutaka kuunganisha watu na kuleta uelewano miongoni mwa wanajamii pamoja na kutofautisha jamii moja na nyingine, kujenga jamii katika shughuli za maendeleo ya jamii huleta amani na mshikamano katika jamii, kufundisha elimu, kutambulisha jamii ya watu fulani na kuhifadhi lugha (Habwe na Karanja, 2004).

Tamthiliya ni utanzu ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji ili kuwasilisha ujumbe wake. Huu ni utanzu ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika (Wamitila 2007). Mkwera (h.t) anaeleza kuwa tamthiliya ni mchezo wa kuigiza au utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo." Othman (2004) anaona kuwa matumzi ya lugha katika Tamthliya ni namna lugha inavyotumika katika kazi ya mwandishi ili kufikisha lengo linalokusudiwa katika jamii.

Kimsingi, mitazamo huweza kutoa taswira ya maana ya lugha inavyoweza kuwa. Mitazamo yenyewe inatokana na wataalamu mbali mbali wanavyoiangalia lugha na matumzi yake kwa jamii husika ili kuepuka masuala ya utata katika kufahamiana na kuweza kufikisha ujumbe kwa jamii inayohusika. Lugha ya kifasihi, ikiwemo tamthilia pia, husharabu kwa maana ya kwamba huchukua maneno kutoka lugha nyengine ili kujiongezea, hali halisi ya matumzi ya lugha hiyo tuiitayo utendaji wa kisarufi.

Kipengele cha lugha ni muhimu sana katika fasihi kwani ndicho hutenganisha fasihi na sanaa nyengine. Vipengele vya lugha katika fasihi vipo vya aina mbali mbali, kama vile tamathali za semi, misemo, nahau, methali, lahaja za wahusika, uchunguzi wa misamiati na miundo ya sentensi (Shule direct.co.tz/notes/view-notes cdDWgy).

Watafiti wengi wa fasihi wamejaribu kuangalia vipengele mbalimbali katika tamthilia kama inavyojithibitisha katika mifano ifuatayo: Dhihai (2005) ameangalia "Nafasi ya Natiki katika jamii ya leo ya Kiunguja." Katika kazi yake hii amebainisha kuwa michezo ya kuigiza katika jamii ya Kiunguja ina mchango mkubwa katika kuburudisha na kuelimisha jamii juu ya mambo mbalimbali. Mambo hayo ni kuheshimiana, kupambana na umasikini, kupunguza utabaka, upatikanaji wa haki na usawa na upambanaji dhidi ya rushwa. Dhamira hizi aliweza kuzibainisha baada ya kutazama matumizi ya lugha ingawa haikuwa sehemu ya malengo ya utafiti. Utafiti wake umetusaidia kufahamu kuwa matumizi ya lugha ya tamathali za semi zina mchango mkubwa katika kuwasilisha dhamira ndani ya tamthiliya. Tumeuchukuwa ujuzi huu na kuutumia katika utafiti wetu.

Naye Mtumwa (2007) alichunguza "Nafasi ya Mwanamke katika Tamthiliya za Penina Muhando," na kubainisha kuwa mwanamke anasawiriwa katika hali chanya na hasi katika tamthiliya za mtunzi huyo. Kwa upande wa hali chanya mwanamke anasawiriwa kama mama mlezi, mchapakazi hodari, mshauri mzuri, shujaa, kiumbe jasiri na kiumbe mpenda maendeleo. Kwa upande wa hali hasi anasawiriwa kama mtu mwenye kupenda starehe za anasa, malaya au kahaba, mfitinishaji, kiumbe muovu, mbeya na msengenyaji. Penina Mlama ni mmoja kati ya wana harakati wa

haki za wanawake ambaye pamoja na mambo mengine ametunga tamthiliya zake kama chombo cha kumsawiri mwanamke katika hali chanya. Hata hivyo, amejikuta akimsawiri mwanamke katika hali hasi pia kudhihirisha kuwa mfumo dume uliopo katika jamii ndio chanzo cha kumfanya mwanamke kuonekana kama kiumbe duni. Katika utafiti wake hakushughulikia matumizi ya lugha ya tamathali lakini ametusaidia kufahamu namna dhamira zinavyojengwa na kuwasilishwa katika tamthiliya.

Tafiti zote hizo hazikujikita kwa undani hassa katika kuchanganua matumizi ya lugha katika kazi hizo, bali lugha ikiwa ni kama kipengele kimojawapo katika kazi walizozishughulikia. Hivyo basi mtafiti baada ya kugundua tatizo hili ambalo ni pengo lililoachwa na watafiti wengi, mtafiti amekusudia kuchambua kwa kina zaidi matumzi ya lugha katika Tamthiliya ya Muandishi Emmanuael Mbogo. Utafiti huu utahusisha Tamthiliya mbili, *Sadaka ya John Okello* na *Fumo Liongo*, ili kuziba pengo hilo na kutatua tatizo la utafiti lililojitokeza.

Kutokana na tafiti za watafiti waliotangulia katika kazi za fasihi ndani ya kazi za tamthiliya inaonesha wazi kuwa kuna mapungufu wa mawanda ya uchanganuzi wa kazi za fasihi ndani ya kipengele cha lugha ambayo ndio mzizi wa kazi ya fasihi na ni kitu pekee kinachoimarisha kazi za kisanaa katika kipengele cha lugha. Hivyo, kuufanya utafiti huu kunaipa nafasi nzuri na ni muhimu kwa watafiti kujishughulisha kwazo ili kuipa haki yake lugha inayotumiwa kuiakisi na kuisawiri kazi ya fasihi kwa undani zaidi. Mtafiti alijikita katika kubaini jinsi gani lugha ilivyofinyangwa na dhamira za kutomea vionjo mbali mbali vya lugha.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Uandishi wa tamthiliya za Kiswahili ni moja kati ya utanzu wa fasihi andishi ambao umepiga hatua kubwa ya maendeleo katika kutafitiwa na kuhakikiwa (Njogu na Chimerah, 1999). Hata hivyo, bado haijafikia hatua kubwa zaidi ya kufanyiwa utafiti ikilinganishwa na ushairi na riwaya ya Kiswahili (Kezilahabi, 1983). Kazi za tamthiliya ambazo zimetafitiwa kwa kiasi Kikubwa ni zile za Ebrahim Hussein, Penina Mlama na Said Ahmed Mohamed (Shemwetta, 2015). Emmanuel Mbogo ni mmoja kati ya watunzi wa tamthiliya za Kiswahili na mpaka kufikia hivi sasa ameandika zaidi ya tamthiliya 10. Hivi karibuni ametoa tamthiliya mpya kadhaa ikiwemo *Sadaka ya John Okello* na nyinginezo. Mpaka sasa hakuna mtafiti aliyechunguza matumizi ya lugha katika tamthiliya hii pamoja na ile ya *Fumo Liongo* ambayo ni ya zamani kidogo. Hii imetusaidia kufahamu mabadiliko ya matumizi ya lugha katika tamthiliya mpya na za zamani za mwandishi Emmanuel Mbogo.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti wetu umejengwa kutokana na lengo kuu na malengo mahususi. Lengo kuu la utafiti ni moja na malengo mahususi ni mawili.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumzi ya lugha katika Tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

i) Kuchambua matumizi ya lugha katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

ii) Kubainisha matumizi ya lugha yanavyojenga dhamira katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unakusudia kujibu masuali yafuatayo:

i) Ni vipengele gani vya matumizi ya lugha vilivyojitokeza katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo?

ii) Ni kwa vipi matumizi ya lugha yametumika katika kujenga dhamira katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kwa kuwa utafiti huu unategemea kuchunguza matumzi ya lugha katika Tamthliya za E. Mbogo ili kukikuza na kukiendeleza Kiswahili kwa uteuzi wake wa maneno teule kwa faida ya jamii ya Watanzania, ni wazi kwamba matokeo yake yanatarajiwa kuasaidia watu wengi kwa hali tofauti kama ifuatavyo:

Kwanza, utasaidia uimarishaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kwa matumzi yake ndani ya kazi ya Fasihi kwa upande wa tamthiliya zetu na kwa faida ya jamii za watanzania wote.Pili, Utafiti huu utasaidia kuweza kutoa mchango wa kuweza kuisoma kazi ya Fasihi kwa kutumia vionjo mbali mbali vya lugha ambayo itatusaidia katika uteuzi wa sentensi na wahusika wake katika Tamthiiya. Tatu, kusaidia kuweka kumbukumbu nzuri ya uhifadhi wa hazina hii muhimu/ adhimu, maalumu ya utumizi wa lugha ili isipotee, iendelezwe kwa kutumiwa na Waandishi

wa kazi za Fasihi na wahakiki wa kazi hizo. Nne, utafiti utasaidia kukuza ari za wahakiki na watafiti katika kuifanyia kazi lugha kwa utumizi wake utakaozingatia jamii unayoiwakilisha na wahuska wake. Tano, utafiti huu utasaidia katika kuliziba pengo kuhusu matumizi ya lugha katika Tamthiliya pale utakapokamilika.

Mwisho utafiti huu utakuwa ni marejeleo muhimu kwa watafiti wa baadae ambao watakuja kushughulikia vipengele ambavyo havijaangaliwa kwa undani katika utafiti huu.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unashughulikia tamthilia teule za Emmanuel Mbogo za *Fumo Liongo* na *Sadaka ya John Okello* tu. Hivyo basi, utafiti huu na uchambuzi wake utajikita katika kuchambua matumizi ya lugha katika tamthilia teule hizo za *Fumo Liongo* na *Sadaka ya John Okello* tu.

## 1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii sura tano ambazo zimewasilisha mambo mbalimbali kulingana na malengo ya utafiti huu. Sura ya kwanza imewasilisha vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Sura ya pili imewasilisha mapitio ya kazi Tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu imeshughulika mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya, kuchambua, kuwasilisha na kujadili data za utafiti na hatimaye kuandika tasinifu hii. Sura ya tano ilihusu hitimisho, muhtasari na mapendekezo kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ina sehemu kuu tatu ambazo ni historiya ya tamthiliya, mapitio ya Maandiko na kiunzi cha Nadhariya. Katika sehemu ya kwanza tumejadili historiya ya tamthiliya, sehemu ya pili inahusu mapitio ya machapisho yanayohusiana na tamathali za usemi katika Tamthiliya, utalii wa kazi tangulizi zinazohusiana na utumizi wa lugha ya Kiswahili katika maeneo tofauti, kazi tangulizi zinazohusiana na tamthiliya katika matumizi ya lugha, pengo la utafiti, kiunzi cha nadharia; Nadhariya ya Simiotiki na mwisho kabisa ni hitimisho.

## 2.2 Historia ya Tamthiliya

Chimbuko la utanzu wa tamthiliya ya Kiswahili linahusishwa na Afrika mashariki hususan Kenya. Tamthiliya za Kiswahili zina asili ya fasihi ya Kiengereza kwani kazi za mwanzo zinazochukuliwa kua ni tamthiliya za kiswahili zina mjengeko na muelekeo wa tamthiliya za kimagharibi, kama anavyosema Burtoncini (1989), Kenya inachukuliwa kuwa ni chanzo cha tamthiliya ya Kiswahili.Tamthiliya ya Kiswahili nchini Kenya ilianzishwa na mzungu Grahan Hyslop, katika awamu ya pili ya miaka ya hamsini. Hyslop katika mwaka (1957), aliandika michezo miwili mifupi ya kuigiza: *Mgeni Karibu* na *Afadhali Mchawi*. Kazi ya Hyslop iliendelezwa na wanafunzi wake wawili Henry Kuria, *Nakupenda Lakini* (1957) na Gerison Ngugi aliyeandika *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (1961).Tamthiliya hizi za awali zilikuwa na mjengeko wa kimagharibi na maudhui yake yalikuwa ya kufurahisha tu. Masuala

yaliyozungumziwa hayakuwa na ukweli wowote kwa jamii ya Mwafrika bali yalilenga kumsifu mkoloni Mwengereza na kumbeza Muafrika.

Nchini Tanzania, uandishi wa tamthiliya umeanza mwishoni mwa miaka ya sitini baada ya Kenya. Hata hivyo, uandishi wa tamthiliya nchini Tanzania ulishika kasi na kuendelea zaidi kuliko Kenya hadi kufikia miaka ya 1980. Zanzibar ambako ndiko asili ya hadithi fupi na riwaya ya kisasa, uandishi wa tamthiliya haukuendelezwa sana nchini humo (Bertoncini 2009). Muasisi wa uandishi wa tamthiliya Zanzibar ni Farouk Topan aliyekua mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alieandika *Mfame Juha* mnamo mwaka 1963 lakini kilichapishwa mwaka wa 1971 kwa lengo kutumbuiza.

### 2.2.1 Kabla ya Ukoloni

Tamthiliya kama tanzu nyengine za fasihi andishi ina misingi katika fasihi simulizi. Fasihi simulizi ndiyo jumla ya maisha ya jamii kwani inahusu matukio, imani, mwelekeo, kazi, itikadi, mwono ulimwengu, mila na tamaduni katika mazingira maalum. Fasihi simulizi ni mfumo mzima wa jamii na hivyo barani Afrika imechukuliwa kuwa tukio la kijamii kwa kuwa inamhusisha kila mtu katika jamii. Matukio katika fasihi simulizi yalihusu maisha halisi ya wanajamii husika.

Tamthiliya zilizoandikwa ili ziigizwe jukwaani hazikuwepo kabla ya ukoloni. Badala yake zilikuwepo Tamthiliya zisizoandikwa, zilizogezwa au kufaraguzwa (improvised) kwa ajili ya kuonyeshwa kwenye shughuli maalum, kwa mfano kwenye sherehe za jando na unyago, mazishi, kutawazwa kwa mtemi, arusi na michezo ya

watoto. Tamthiliya hizozilikuwa na sifa kadha za tamthiliya yaani hadithi, vitendo, wahusika na waigizaji wao na dialogia. Halikadhalika zilikuwa na sifa 7 za sanaa za maonesho zilizotajwa katika muhadhara wa 11. Hata hivyo tamthiliya hizo hazikuwa nap loti ya kiaristotle wala matini yaliyoandikwa. Hivyo hizi zilikuwa ni tamthiliya simulizi. Mfumo mzuri wa tathiliya hizi za awali ni maigizo ya watoto wakati wanapocheza. Kwa mfano watoto A, B, C na D wanaamuwa kuigiza mchezo wa unyumba. Katika igizo hilo, mtoto A (mvulana) ankuwa baba mwenye nyumba, B (msichana) anakuwa mama, C na D (mvulana na msichana ) wankuwa watoto na kadhalika. Mchezo unaanza kwa A kumwambia B aandae chakula, B anafanya hivyo wakati C ankwenda mtoni kuchota maji na D anapeleka mbuzi malishoni. Chakula kinapoiva wote wananawa mikono wanakusanyika na kula.

Baada ya kula wanafunga milango na kulala, na kadhalika. Michezo ya aina hii ambayo hadi leo ipo, ni tamthiliya halisi ya kubuni yenye kumathilisha maisha.

### 2.2.2 Wakati wa Ukoloni

Ukoloni ulianza rasmi barani Afrika mwaka 1885 hata hivyo uandishi na uchapishaji wa tamthiliya kwa lugha ya Kiswahili haukutiliwa maanani hadi mwaka 1957. Kama anavyosema Mugambi (1982) kuwa tamthiliya zilizochapishwa katika lugha ya Kiswahili katika muundo wa fasihi ya Kiingereza ziliandikwa kuanzia mwaka wa 1957. Tamthiliya hizi zilikuwa vichekesho na tamthiliya fupifupi ambazo ziliigizwa katika mashule mwishoni mwa muhula au kama mashindano wakati wa sherehe maalum.

Mifano ya tamthiliya zilizochapishwa katika kipindi hiki ni pamoja na; *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu* za Graham Hyslop (1957), *Nakupenda Lakini* (1957) ya Henry Kuria pamoja na *Nimelogwa Nisiwe Na Mpenzi* (1961) ya Gerishon Ngugi. *Afadhali Mchawi* inaonyesha mandhari ya hospitalini ambapo wahusika wakuu ni Issa na Ali. Issa ambaye ni mhusika mkuu amejenga maudhui ya ufisadi ambao unatokana na ubinafsi. Issa anauza dawa ambazo zinastahili kutibia wagonjwa bila kujali maslahi ya wengine. Hyslop amedhihirisha ufisadi huu miongoni mwa jamii ya Mwafrika aliyoibuni kupitia Issa. Maudhui mengine yanayojitokeza katika tamthiliya hii ni ukoloni, udhalimu wa ukoloni kupitia kutozwa kodi, elimu inayochukuliwa kama msingi wa Mwafrika wa kubatiliza mila na desturi za Waafrika huku waliosoma wakiiga tabia za kigeni kama vile, mavazi, lugha na hata taratibu za maisha. Hyslop ameisawiri jamii ya Mwafrika kama kielelezo cha kutoaminika, ufisadi, wizi na mtu duni.

Kwa upande mwingine amemjenga Mwingereza kuwa wa tabaka tawala, bepari, nyonyaji na tabaka lisilomthamini Mwafrika. Kwa upande wa wahusika, Hyslop katika kuusawiri ufisadi wa Issa, amewaumba wahusika waadilifu kama Ali ambaye ni tabibu mwadilifu pamoja na wazazi wake. *Mgeni Karibu* inamzungumzia mhusika mkuu Said. Kupitia Said tunauona usultani na utawala ambao aliurithi kupitia ufisadi wa babake. Maudhui mengine yanayojitokeza katika tamthiliya hii ni pamoja na ubinafsi na tamaa inayoendelezwa na mjomba wake Said; Shabani. Lengo la Hyslop katika tamthiliya hii ni kuwapotosha Waafrika wasiupinge utawala dhalimu. Ameichora jamii iliyochoshwa na utawala dhalimu lakini jitihada za kumwondoa

mkoloni zinapingwa. Kwa jumla, tamthiliya hii inalenga kuudunisha utu wa Mwafrika na kutukuza vitendo vya udhalimu vya Waingereza.

*Nakupenda Lakini*, inahusu suala la mapenzi na ubinafsi. Mhusika mkuu Kangwana anaongozwa na ubinafsi, anashiriki wizi na mauaji mradi apate pesa na kutajirika ili apendwe na Roda. Mapenzi baina ya Kangwana na Roda yanaonekana si ya dhati. Roda hampendi Kangwana lakini anaipenda mali yake. Mapenzi haya ndiyo yanayompelekea Kangwana kushiriki kitendo cha mauaji na wizi. Tamthiliya za Hyslop *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu* na tamthiliya ya Kuria *Nakupenda Lakini*, zimejikita katika ulimbwende huku wananchi wakiteswa na kuuwawa chini ya ukoloni katili na dhalimu.

*Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi*, inaangazia mapenzi baina ya vijana wa Kiafrika. Inaangazia mgongano baina ya wazee na vijana unaotokana na mabadiliko ya mazingira katika jamii. Wazee wanashurutisha ulipaji wa mahari ilhali vijana wanauona kama 'ununuzi'usio na msingi katika mapenzi ya dhati. Mapenzi ya dhati yanadhihirika baina ya Beatrice na Ben ambao ni wahusika wakuu.

Tamthiliya zilizoandikwa katika kipindi cha ukoloni zimejikita katika ulimbwende ambao lengo lake ni kufurahisha tu. Ni tamthiliya ambazo hazikuonyesha uhalisia katika jamii bali zilichukua muundo wa vichekesho. Wahusika walisukwa kwa namna ambayo walijenga tamthiliya hizo. Misuko sahili ilitumika katika tamthiliya hizo huku lugha ikiambatanishwa na mazingira ya matumizi.

### 2.2.3 Kipindi cha Baada ya Ukoloni

Muda mfupi tu baada ya uhuru baadhi ya tamthiliya zilitungwa moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili huku nyingine zikitafsiriwa kutoka lugha kutoka lugha ya Kiingereza. Kwa mfano, tafsiri ya Morrison-*Mchuuzi Muungwana* (1966) ya Moliere. Mwaka wa 1967 Hussein aliandika *Wakati Ukuta* na *Alikiona*. Mwaka wa 1968, Nkwera aliandika *Johari Ndogo* huku Mushi akiandika tafsiri ya Macbeth ya Shakespeare. Tafsiri nyingi zilichapishwa mwaka wa 1969 ambazo ni pamoja na *Tufani* ya Mushi, *Juliasi Kaizari* na *Mabepari wa Venisi* ziliotafsiriwa na J.K Nyerere.

Ilipofika miaka ya thamanini taswira ya tamthiliya ilbadilika kama anavyosema Mlama (1983) katika Wafula (1999) anasema futuhi ziliendelea kuandikwa lakini katika kipindi hiki ziliwasuta Waafrika walioiga mienendo ya wazungu kikasuku. Kulingana na maoni yake Mlama, waandishi nchini Tanzania walianza kufungamanisha tamthiliya na mahitaji ya nchi ya Tanzania. Hivyo basi, maudhui yaliyodhihirika katika tamthiliya za kipindi hiki ni pamoja na; ukoloni, ukoloni mambo leo, umaskini, elimu, swala la mwanamke na utabaka. Kwa mfano: Mwanyengela Ngali mnamo mwaka 1971, alichapisha mkusanyiko wa michezo mitatu-*Mwana Taabu* na michezo mingine. *Mwana Taabu* ni mchezo unaozungumzia masuala muhimu katika jamii wakati huo. Mchezo huu unamhusu msichana ambaye ameelimishwa na wazazi wake kwa taabu wakidhani atawafaa katika maisha yao ya baadaye. Kinyume na matarajio ya wazazi wake, Taabu anaolewa pindi tu baada ya kukamilisha masomo yake na kukatiza mahusiano na wazazi wake.

*Kifo cha Penzi* ni mchezo unaochukua mkondo wa melodrama na unamhusu Maryamu na mchumba wake Juma ambaye anajiua kwa sababu ya mapenzi yake kwa Juma. *Mbio za Sakafuni* (1976) unaozungumzia mhusika mkuu wa kike Halima ambaye analazimishwa na wazazi wake kuolewa na Ahmad kwa sababu ya utajiri wake na kisha kushawishiwa atalikiwe na Ahmad na kuolewa na ambaye ni tajiri kuliko Ahmad. Jambo la kusikitisha ni kuwa Halima anabakia bila mume na hivyo kuwalaumu wazazi wake. Aidha hakuna kilele cha mchezo kama anavyoeleza Bertonchini (2009).

Mwaka wa 1980, Mzee na Muslim waliandika *Mkuki wa Moto,* mchezo ambao ulishughulikia masuala ya kihistoria ya Kenya tangu 1919 wakati walowezi wazungu walivamia ukikuyuni hadi wakati wa kujinyakulia uhuru. Bertoncini (2009) anadai hii ndiyo tamthiliya ya kwanza kuhusu vita vya Mau Mau. Waandishi katika kipindi hiki –Jay Kitsao, Zani Na Felix Osodo walitaka kuonyesha uhalisia wa kihistoria katika kazi zao lakini walishindwa kuzingatia uhalisia wa maisha katika kuunda maudhui yao. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Mwana Mpotevu* ya Zani, ukarimu unaojengwa ndani ya Hewala babake Mpotevu katu haujashuhudiwa katika mazingira ya Kiafrika ambayo yamejawa na ugandamizwaji wa kisiasa, kiuchumi na hata kiutamaduni pamoja na dhuluma za ukoloni mambo leo katika kizazi cha ubepari. Tamthiliya yenyewe ni kielelezo cha ubadhirifu kama anavyosema Mugambi (1982). Maudhui yamejengwa kupitia mhusika mkuu Mpotevu, ambaye ni mwana wa Mzee Hewala, mzee tajiri. Maudhui makuu katika tamthiliya *Mwana Mpotevu* ni tamaa ya mali na ukarimu.

Tamthiliya ya Jay Kitsao, *Jirani Kanyolewa* (1975) imeangazia mambo mawili; msimamo wa wanaume kuhusu wanawake kwa jumla na jitihada za kutekeleza wajibu kwa kujitolea kama anavyosawiriwa mwalimu wa Chadi. Babake Chadi na mwenzake Dadazha wanashikilia kuwa mahali pa mwanamke ni jikoni tu na kuwa hakuna maana ya elimu. Mbinu alizotumia kuendeleza tamthiliya yake ni pamoja na mfululizo bayana wa kisa chake na utani wa wazee unaodhihirisha msimamo wa dharau na kuwabeza wanawake.

Kwa jumla, tamthiliya hii hailandani kihalisia na mandhari ya mazingira yake. Sanaa ya Kitsao inaishia kuidhalilisha jamii kwani maudhui yake hayaonyeshi jamii ambayo ina uwezo wa kujikomboa.

Mchezo wake wa pili – *Mafarakano* (1975), unahusu uchawi. Mchawi katika mchezo huu analazimishwa kuacha uovu wake wa uchawi. Mchezo umeandikwa vizuri kuliko *Jirani Kanyolewa* lakini suluhu yake inafikiwa pasipo na taharuki yenye motisha. Kitsao ni mwandishi mtajika katika kipindi hicho hivyo aliandika tamthiliya nyingine nne: *Uasi* (1980), *Tazama Mbele* (1981), *Bibi Arusi* (1983) na *Malimwengu Ulimwenguni* (1983). *Uasi* inahusu wasichana wa kipindi hicho wanaolazimishwa katika ndoa zisizoelekezwa na mapenzi huku ikizungumzia masuala ya ndoa ambapo wasichana wanalaumiwa kwa kutaka kuolewa na mabwanyenye wazee huku wakiwakataa wanaume wa rika lao ambao ni fukara. Tamthiliya ya Osodo, *Hatari kwa Usalama* pia haijazingatia uhalisia wa jamii katika uundaji wake wa maudhui.

Kinyume na waandishi hawa, tumeangazia waandishi wa tamthiliya ambazo zinaafiki uhalisia wa kijamii. Tamthiliya hizi ni pamoja na; *Mashetani* (1971) ya Hussein, *Mzalendo Kimathi* (1978) ya Ngugi na Micere Mugo, *Mukhwava wa Uhehe* (1979) ya Mulokozi na *Kilio Cha Haki* (1981) ya Mazrui. Hussein, Ngugi, Micere Mugo, Mulokozi na Mazrui wanazingatia uhalisia wa kihistoria. Tamthiliya hizi zinadhihirisha mwamko wa kisiasa.

Wameonyesha fasihi ya mapambano dhidi ya unyonyaji na ugandamizaji wa mkoloni dhidi ya Mwafrika. Maudhui makuu katika *Mashetani* ni mtafaruku wa kitabaka chini ya ukoloni mambo leo. Mtafaruku huu unadhihirishwa na wahusika wakuu wawili Juma na Kitaru. Tamthiliya hii iliandikwa kutokana na yaliyotokea nchini Tanzania baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Tamthiliya hii imegawika katika sehemu mbili: Sehemu ya kwanza inaeleza juhudi za mkoloni kumtawala Mwafrika kiakili kama inavyojitokeza katika mchezo ndani ya mchezo baina ya Juma na Kitaru juu ya '*Mashetani'*.

Sehemu ya pili inajadili matatizo yanayowakabili Watanzania chini ya ukoloni mambo leo. Sehemu hii inaendelezwa katika akili ya Kitaru ambaye ni kielelezo cha Mwafrika aliyepumbazwa na elimu na athari za mkoloni. Sehemu hii inafafanua migongano ya kitabaka iliyoendelea na inayoendelea baada ya uhuru. Dhamira zinazoangaziwa ni pamoja na; utabaka, elimu ya kikoloni, ukoloni mambo leo, na ubepari kama mfumo wa kuwanyanyasa wanyonge kiuchumi. Hussein ameoanisha fani zifuatazo katika kuendeleza maudhui; nyimbo za sherehe zilizofuata uhuru, ndoto inayoonyesha ulimwengu ambao Kitaru anaona ni wa tabaka lake

na matumizi ya kina ya jazanda kwa mfano, shetani (mkoloni), binadamu (Mwafrika) na kisu (elimu). Kwa jumla, matatizo anayoeleza Hussein katika Mashetani si yanayowakumba Watanzania pekee bali mataifa ya Afrika Mashariki kwa jumla. Anaeleza jinsi matatizo yalianza wakati wa ukoloni na kuendelea hata baada ya uhuru wa bendera chini ya ukoloni mambo leo. Ujumbe wa Hussein kwa Mwafrika ni kwamba Mwafrika asake nafsi yake pasipo kuzingatia maisha ya Kizungu ambayo hayalingani na hali halisi ya jamii yake.

Ngugi na Micere Mugo katika *Mzalendo Kimathi* (1978) wanadhihirisha mwamko wa kisiasa. Tamthiliya hii inaangazia utetezi wa hadhi ya Mau Mau kama vita vya ukombozi vya kitaifa kwa jumla, vita ambavyo bado vinaendelezwa dhidi ya ukoloni mambo leo ambao unawadhulumu wafanyikazi na wakulima wadogo wadogo kiuchumi na kisiasa. Masuala yaliyoangaziwa ni pamoja na uzalendo, ukombozi, ujasiri na usaliti. Tamthiliya ya *Mzalendo Kimathi* imetumia mandhari yanayoambatana na uhalisia wa kihistoria wa jamii kwa kumtumia Kimathi kama mhusika pamoja na kuhukumiwa kwake Nyeri.

Tamthiliya ya Mazrui *Kilio Cha Haki* (1981) inatudokezea mapambano ya wafanyikazi dhidi ya udhalimu wa makaburu uliowakilishwa na Delamon. Tamthiliya inaanza kwa hamasa na ghadhabu ya hali ya juu ya wafanyakazi ambao wameamua kupigana dhidi ya kunyanyaswa na ukaburu. Kama anavyoeleza Mugambi (1982:160), *Kilio Cha Haki* ndiyo tamthiliya ya kipekee ya Kiswahili iliyofikia kilele kabisa katika kubainisha hisia za ukombozi wa jamii iliyobanwa katika utumwa. Baadhi ya masuala yanayozungumziwa katika *Kilio*

*cha Haki* ni pamoja na:- ubepari unaoendelezwa na Delamon ambaye ni kaburu mdhalimu, ukabaila, utabaka,ujasiri wa mhusika mkuu wa kike Lanina, Musa na Dewe katika harakati za kupigania haki za wafanyakazi, udhalimu, usaliti, ukombozi – wa wanawake, wa kisiasa na wa kiuchumi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke amesawiriwa kuwa kiumbe anayedhalilishwa.

Tamthiliya nyingine katika kipindi hiki ni pamoja na; *Mfalme Juha* (1971) ya Farouk Topan, na tafsiri ya *Mfalme Edipode* ya Mushi (1971), *Hatia* ya Mlama na *Kifo Barabarani* ya Ngahyoma zote za mwaka wa 1972, *Aliyeonja Pepo ya Topan* na *Tambueni Haki Zetu* ya Mlama zilizochapishwa mwaka wa 1973, *Heshima Yangu* ya Mlama na Yahya nae akatafsiri *Masaibu ya Ndugu Jero* mwaka wa 1974. Mwaka uliofuata, tamthiliya zifuatazo zilichapishwa; *Pambo* na *KortiniMtu Huyu* za Mlama, na *Mwanzo wa Tufani* ya Kulikoyela Kahigi na Ngerema. Mwakawa 1976, Hussein alichapisha *Jogoo Kijijini* na *Ngao Ya Jadi*. Mnamo mwaka wa 1977. *Machozi ya Mwanamke* iliandikwa na Ngozi, Mwaka wa 1978, Katalambulla alichapisha tamthiliya mbili, *Imani Yangu* na *Unono wa Mizani*. Mulokozi alichapisha mchezo wa kuigizwa *Mukwava wa Uhehe* mwaka wa 1979 pamoja na tafsiri ya Christon Mwakasaka.

Mwaka wa 1980 kulikuwa na tamthiliya nyingi zilizochapishwa kama vile *Maalim* na *Hukoo Darisalama* ya Muba, *Dhamana ya Mabatini* ya *Kaduma* na *Giza Limeingia* ya Mbogo. Mwaka wa 1981 Mbogo alichapisha *Tone la Mwisho* na *Watoto Wetu*. Mwaka wa 1982, Balisidya na Mlama waliandika *Harakati za Ukombozi* na Mlama akaandika *Nguzo Mama*, huku Chacha akiandika *Mke*

*Mwenza* naye Kibugi akatafsiri *Nitaolewa Nikipenda* (1983), Mulwa na Yahya wakaandika mchezo wa kuigiza wa *Buriani* na tamthiliya ya *Uchafu* ikaandikwa na Malima. Mulwa na Yahya waliandika Ukame (1984), Khaemba akaandika Visiki (1984) naye Omar akachapisha *Maisha Subira* (1985). *Zinduko* ya Ryanga na *Marejeo ya Chacha* zilichapishwa mwaka wa 1986. Tamthiliya zilizofuata ni, *Wingu Jeusi* (1987), tamthiliya ya Chacha na *Mama Ee* (1987) ya Ari Katini Mwachofi, Kwenye *Ukingo Wa Thim* (1988) ya Hussein, *Mkimbizi (*1988) ya Mulwa na Yahya na *Ngoma Ya Ng'wanamalundi* (1988) ya Mbogo. Tamthiliya katika miaka ya sabini hadi miaka ya thamanini zimeonyesha maendeleo makubwa. Zinatubainishia ujasiri wa waandishi ambao unatudhihirishia ujasiri wa jamii kwa jumla. Jamii imezinduka kimawazo na hivyo inaelewa bayana kuhusu dhuluma na ugandamizwaji waliopitia wakati wa ukoloni na hivyo wameamua kupigana na udhalimu huu.

Tamthiliya katika kipindi hiki hazionyeshi kudhalilishwa kwa Mwafrika wala utamaduni wake bali zinaonyesha kupigania haki za Mwafrika kupitia mapinduzi yanayoongozwa na Waafrika jasiri kama vile Kimathi na Lanina. Kipindi hiki kinadhihirisha kilele cha mwamko wa kisiasa, kilele cha kuzinduka na kilele chaujasiri ambao msingi na mhimili wake ni katika jamii.

Miongoni mwa tamthiliya zilizoandikwa katika kipindi hiki zinagusia masuala ya mapenzi pia. Mtindo unaotumiwa na waandishi katika kipindi hiki unaonyesha ukomavu mzuri unaowezesha dhamira na maudhui yajitokeze kwa nguvu na mnato wa kuridhisha.

Tamthiliya za kutoka miaka ya tisini hadi sasa zinachukua mkondo mpya tofauti na miegemeo ya tamthiliya za hapo awali ya uhalisia wa kihistoria. Tamthiliya katika kipindi hiki zinachukua mwelekeo wa nadharia ya usasa na usasa leo. Hivyo basi, tamthiliya za kipindi hiki zimekitwa katika uhalisiajabu uliochanganganywa na uhalisi uliopo katika jamii ya kisasa. Kwa mfano, tamthiliya ya Wamitila, *Wingu la Kupita* (1999) imejengwa katika misingi ya fasihi ya kimajaribio. Dhamira katika tamthiliya za kipindi hiki, zililenga changamoto zilizopo katika jamii kama vile; ukosefu wa kazi, umaskini, uongozi mbaya, ugonjwa wa ukimwi na matatizo katika asasi ya ndoa. Wahusika katika tamthiliya za kisasa wana mchocheo wa kutaka kujua ukweli na hivyo kuzuka kwa wahusika jasiri wa kimapinduzi.

Masuala ya teknolojia na lugha ya utandaridhi yanajitokeza katika tamthiliya hizi. Kwa jumla, tamthiliya katika kipindi hiki zinaangazia masuala yanayoizunguka jamii ya kisasa. Mifano ya tamthiliya katika kipindi hiki ni kama vile *Kivuli Kinaishi* (1990) na Amezidi (1995) za Mohammed, *Mawimbi na Kiumbe* (1991) za Eshamwata, Chacha-*Hukumu* (1992), *Mkutano wa Pili wa Ndege* (1992) ya Amandi na Lihamba, *Morani* (1993) na *Sundiata* (1994) za Mbogo, *Kaptula La Marx* (1996) ya Kezilahabi na *Unga* (1996) ya shaaban *Mnara Wawaka Moto* (1998) ya Chimerah, *Wingu La Kupita* (1999) ya Wamitila na Manamba (1999) ya Khaemba.

Tamthilia za kuanzia mwaka wa 2000 ni pamoja na:- *Upotovu* (2000) ya Kimunyi, *Siri* (2000) ya Farouk Topan, Kitumbua Kimeingia Mchanga (2000) ya

Mohamed , tamthiliya za Kithaka wa Mberia *Kifo Kisimani* (2004) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004), *Mazonge* (2004) ya Rashid, *Sudana* (2005) ya Mazrui, *Pango* (2004) na *Sumu ya Bafe* (2006) Wamitila, *Zilizala* (2006) Njogu, *Migogoro* (2006) ya Mbatiah, *Chamchela* (2007), *Mstahiki Meya* (2009) na *Kijiba cha Moyo* (2012) za Timothy Arege.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Kuhusu Mada ya Utafiti

Omary (2011) anasema kuwa, kazi tangulizi hutoa ujuzi na maarifa ya wanazuoni waliowahi kufanya kazi yenye muelekeo na lengo la mtafiti. Hii humsaidia mtafiti kutambua mambo yapi yamefanyiwa utafiti na yapi bado hayajashughulikiwa. Aidha katika kipengele hiki mtafiti amepitia kazi tangulizi mbalimbali ambazo zinazungumzia matumizi ya lugha na tafiti zilizowahi kufanywa kwa kukigusa kipengele hiki muhimu sana cha utumizi wa lugha katika kazi za fasihi.

### 2.3.1 Kazi Tangulizi za Matumizi ya Lugha katika Nyanja Mbalimbali

Butts na Cockburn (2011) watafiti hawa walifanya tathmini ya utumiaji wa ujumbe katika simu za kiganjani kama mbinu ya mawasiliano na waligundua kuwa utumiaji wa matini ni tabia iliyokuwa kwa haraka hasa miongoni mwa vijana. Pia waligundua kuwa kuanzia mwezi Januari hadi Disemba mwaka 2000, matini fupi fupi (ujumbe mfupi) zilizofumwa ziliongezeka kwa haraka kutoka matini bilioni 4 na kufikia bilioni 15 kwa mwezi.

Kwa ufupi uchunguzi wao ulilenga kuangalia kasi ya ukuaji tu, hawakuchunguza ujumbe wa sura gani na ulihusu mambo gani. Kipengele hiki kimetowa msukumo

kwa mtafiti kutaka kufanya uchunguzi kiundani zaidi kuhusu matumizi ya lugha yanavyojenga dhamira kupitia kazi za fasihi kwa upande wa tamthiliya jinsi lugha navyokuzwa na kuendelezwa na kwa kiasi gani inahusishwa. Kutokana na mapungufu haya mtafiti amejikiza katika kuipa kipaombele lugha na kuweza kuona jinsi fani hii muhimu sana inayoweza kuiwakilisha jamii juu ya lugha na kupitia utumizi wake.

Mphahlele na Mashamaite (2005), wameandika kuhusu athari za ujumbe mfupi mfupi katika kupata umahiri wa lugha. Lengo kuu la utafiti wao lilikuwa kufafanua kwa undani ni kwa namna gani mwanafunzi anashindwa kuwa mahiri katika lugha kutokana na matumizi ya lughatandawazi. Pia waliangalia nafasi ya Kamusi katika kuinua umahiri wa lugha kwa wanafunzi.

Rafi (h.t) alifanya uchambuzi wa matini za ujumbe mfupi katika lugha ya jinsi. Lengo kuu la utafiti wake lilikuwa kuchunguza uchanguzi wa msamiati na mofosintaksia wa wanawake na waume wanaotumia ujumbe mfupi. Katika utafiti wake ulipima Nadharia tete inayosema kuwa lughatandawazi ni kama pijini katika jamii kwa lugha yoyote. Pia utafiti wake ulipia nadharia tete nyengine kuwa kasi kubwa ya ujumbe mfupi iko kwa wanawake ambao msamiati na mofosintaksi wanaoutumia ni tofauti na wanaume.

Vile vile aliangalia lugha tandawazi katika lugha inayotumika katika vyombo vya habari. Katika utafiti huo zilichukuliwa matini za ujumbe mfupi 100 katika simu za kiganjani zilizoandikwa na wanawake na wanaume , matii hizo zilichambuliwa na

kuangaliwa ili kuangalia msamiati, mofolojia na sintaksia ya lugha kwa watumiaji wa ujumbe mfupi na kuangalia athari zake katika biashara.

Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa katika ujumbe mfupi kumekuwa na lugha mpya ambayo imekuwa inaathiri lugha ya vyombo vya habari vile vile matokeo yalionesha kuwa kuna tofauti za msamiati na mofosintaksia ya wanawake na wanaume katika ujumbe mfupi wa simu za kiganjani, hata hivyo athari hizo hazikuhusishwa na lugha ya Kiswahili. Utafiti huu uanampa nafasi mtafiti kuzitafutia ufumbuzi mongoni mwa changamoto zisizopewa nafasi zaidi kwa upande wa matumizi ya lugha katika tamthiliya na jinsi iavyotumiwa kisanaa na jinsi inavyotumika hazina hii muhimu.

Juma (2007) alifanya utafiti juu ya matumizi ya lugha katika nyimbo za Uganga Zanzibar, katika utafiti huu amezitafiti nyimbo amabazo huimbwa ugangani na jinsi zinavyotumia matamshi ya lugha teule ambayo ina maana ya ndani zaidi. Lugha katika nyimbo za uganga ikiwemo:

*Nyumbu wee nyumbu,*
*Mwana wa nyumbu,*
*Aliliya usinga si wake,*
*Nyamara Mwananguwe,*
*Usiliye nitakupa wako usinga.*

Katika wimbo huu tunaona utumiaji wa lugha teule ya kisanii, maneno kama vile; Nyumbu, Nyamara maneno haya yametumika kifasihi na kwa ustadi, kwani pamoja na kwamba ni maneno ya kawaida, lakini yanauathiri ujumbe kinyume na matumizi. Wimbo unaotumika katika Uganga wa majini, kuwa na maana kwamba ni kawaida ya jini ambae amempenda mtu. Jini analialia usinga si wake, maana yake ni kwamba

amempenda mtu bila ya ridhaa. Wimbo unaendelea kusema “Nyamara mwanangu usiliye” takupa wako usinga.” Jini anaendelea kuambiwa kwamba amuachiye huyo kiumbe aliyemtamani, atapewa anachokitaka.

Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba nyimbo za Uganga zinatumiya mafumbo zaidi na hivyo kuepuka kutaja wazi wazi kile kilichokusudiwa. Nyimbo pia hutumia lahaja ya Kipemba ambapo husababisha ugumu wa kupata ujumbe kwa wale wasioifahamu lahaja hiyo. Mtafiti amegundua kuwa lugha inayotumika katika nyimbo za Uganga inakiuka utaratiu wa Sarufi ya Kiswahili Sanifu, inawezekana hii ni kutokana na kutumia lahaja hiyo ya Kipemba. Pia ishara na Taswira zinazotumika kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za Uganga, ishara zilizotumika zinatowa mchango mkubwa katika kufikisha ujumbe kwa Hadhira.

Matumizi haya ya lugha yamemsaidia mtafiti kumpa msukumo kwa kuingia ndani zaidi katika kipengele ambacho hakijafayiwa utafiti wa kutosha juu ya matumizi ya lugha katika kazi za fasihi na uzichambuwa kwa lengo la kuakisi hali halisi iliyokusudiwa na mtunzi wa kazi za fasihi ambap watafit wengi hawakujadili vyema kipengele hicho.

Muhammed (2013) ameangalia matumizi ya lughatandawazi katika simu za kiganjani. Katika utafiti wake huo ameweza kubainisha kuwa matumizi ya lughatandawazi katika simu za viganjani ni ule ambao haufuati sarufi ya Kiswahili (Kuchanganya namba na herufi), unachanganya misimbo na hukata maneno au kudondosha irabu. Watumizi wakubwa wa mtindo huu ni vijana kuliko wazee.

Matokeo ya utafii huu yalionesha kwamba watumizi wa lughatandawazi hutumia njia hii ili kupunguza gharama za kutuma ujumbe, kuokoa muda wa kuandika ujumbe, kufupisha maneno ili ujumbe uwe mfupi na urahisi wa kuandika na kuwasilishana.

Kwa mujibu wa Kipacha (2003) amesema "Kila kitu ulimwenguni kipo katika hali ya mabadiliko lugha ikiwa ni miongoni mwao, hali hii inajidhihirisha pale wanapoweza kubagua baina ya lugha ya kisasa na lugha ya kizamani." Mutiso (1992) anasisistiza kuwa msamiati wa zamani ulifunguliwa na kupewa matumizi mapya kwa dhana ambazo tayari zina msamiati wa kiasili. Pia kazi ya Kuingo (1995) zilionesha mbinu mbali mbali za uundaji wa msamiati mpya yeye alisisitiza kuwa zoezi la kuunda misamiati sio la kipekee kwa Kiswahili bali ni uhai wa lugha zote.

Kutana na kipengele hicho kinachosisitiza uhai wa lugha mtafiti amejikita zaidi katika kipengele cha matumizi ya lugha na kuitafiti ili kuna jinsi gani ataweza kuyafanyia utafiti wa kutosha na kuyabainisha matumzi hayo ya lugha kwa matumizi ya semi, methali, tamathali za usemi na kadhalika.

Foucault (1981) imeeleza kuwa "Lugha hukua na kubadilika ingawa si lazima mabadiliko haya yawesambamba na mabadiliko katika jamii yote, akashadidia kwa kusema ujuzi wa lugha tulionao hutuwezesha kutoa na kuelekea msamiati wa sentensi mpya kila siku kama kanuni za misingi za lugha zitafuatwa. Hivyo, lugha zimefungamana sana na mfumo, mwenendo wa mabadiiiko ya maisha ya binaadamu. Naye Haji (2007) amefanya utafiti juu ya sababu zinazopelekea utatanishi katika matamshi kwenye lugha ya Kiswahili kisiwani Unguja, utafiti wake umeangalia zaidi utata unaojitokeza katika baadhi ya matamshi kama:

*Paa – la nyumba au Ezeko.*

*Kiboko – Fimbo au Bakora*

*Kikombe – cha chai au cha Ushindi.*

*Amepanda mti – Amekwea au Ameotesha.*

Matamshi mengi yanayofanana haya huwa yana utata fulani ambao unaweza kupoteza lengo iwapo hautafafanuliwa utata huo. Kutokana na kuwepo kwa sababu hizo zinazojitokeza kuwa kama ni utatanishi wa kimatamshi, mtafiti aliona bora alifanyie utafiti suala hili ili apate maoni na kutoa majibu na mapendekezo ya watafitiwa nay ale ya mtafiti katika utafiti wake.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba watafatitiwa wameona kwamba kuna umuhimu wa kusomeshwa mada hii mapema zaidi (yaani kuanzia darasa la 3) kimsingi wanafunzi waelezwe wawe makini wanaposikiliza taarifa, ili kuepukana na utatanishi katika matamshi, wanafunzi wafundishwe chanzo cha utatanishi, sababu na jinsi ya kutatua utatanishi, kuwepo mipumuo na misimamo wakati wa kuzungumza, kuongeza misamitai katika lugha, ni jambo muhimu katika lugha nahii itapelekea kupunguza au kuondoa utatanishi katika matamshi, inasaidia kutowa maana katika sentensi au muktadha mbali mbali kwani kila lugha zimo sentensi tatanishi hali hii haina maana ya kwamba lugha ya Kiswahili ina upungufu wa misamiati bali nisifa ya lugha. Pia inahitaji kufundishwa skuli za Sekondari ili kuwafanya wanafunzi wawe weledi katika lugha yao.

Utafiti huu umesukuma mbele zaid shauku ya msanii kutaka kufanaya utafiti wa kina ili kuweza kugunduwa ni kwa namna gani muandishi amejikita katika matumizi ya

lugha na jinsi yanavyojenga dhamira kwa kila tamthiliya ambayo mtafiti ameikusudia kuifanyia utafiti.

### 2.3.2 Kazi Tangulizi Juu ya Tamthiliya

Ingawa uandishi wa tamthiliya nchini Tanzania ulianza miaka ya sitini lakini ulishika kasi miaka ya thamanini ambapo kulijitokeza waandishi mbali mbali wa tamthiliya kama vile Ebrahim Hussein, Penina Muhando, Said A. Muhammed na wengi wengine ambapo wote walikua na lengo la kukosoa na kuendeleza jamii ya kiafrika. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu tamthiliya na hasa hasa katika vipengele vya fani na maudhui. Lakini hadi sasa hakuna utafiti uliofanywa kuhusu tamathali za usemi kwa kulinganisha tamthiliya za mwandishi mmoja hasa katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Miongoni mwa walioandika kuhusu tamthiliya ni hawa wafuatao:

Mugabi (1982) ametumia nadharia ya U_Max kuhakiki maudhui katika tamthiliya zilizochapishwa nchini Kenya za kipindi kati ya mwaka 1957 hadi mwaka 1981. Katika utafiti wake Mugabi ameonesha mbinu (fani) walizozitumia waandishi wa tamthiliya katika kuendeleza dhamira mbali mbali. Miongoni mwa dhamira hizo alizozichanganua ni udhalimu, ukombozi, usaliti, nafasi ya mwanamke katika jamii, utetezi wa haki za wanyonge, ubepari na ukoloni mamboleo. Pia Mugabi ameonyesha mandhari, wahusika, matumizi ya lugha hasa jazanda na matumizi ya tamathali za usemi kama mbinu muhimu katika ujenzi wa maudhui na dhamira mbali mbali.

Kazi ya Mugabi ilitufaa sana katika utafiti wetu kwa vile amechambua tamathali za

usemi kipengele ambacho ndio hasa kilichoshughulikiwa katika utafiti wetu. Utafiti wa Mugabi ulitusaidia sana kuchunguza matumizi ya lugha ingawa sisi tulijadili kwa kupitia tamthiliya za Emmanual Mbogo. Aidha utafiti huu ulijikita zaidi kuchunguza tamathali za usemi kama ni kipengele cha fani ili kubaini jinsi kinavyoibua dhamira huku tukitumia nadharia ya Simiotiki.

Chesaina (1987) alitumia tamthiliya ya Mlama (1972) ‘*Hatia*’ na tamthiliya ya Muhando (1982) ‘*Nguzo mama*’ huku akitumia nadharia ya ufimenisti kueleza utata unaomkabili mwanamke katika hali zake zote za maisha. Tofauti na yeye ni kwamba sisi tulitumia tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Kazi ya Chasino imejikita zaidi kufafanua nafasi ya mwanamke, kazi yetu ilichunguza matumizi ya lugha katika tamthiliya teule za Emmanual Mbogo.

Kiango (1992) ametumia nadharia ya ufimenisti kutafiti maudhui katika tamthiliya kwa kulenga taswira ya mwanamke katika tamthiliya, katika kazi yake mwanamke amesawiriwa kwa njia hasi kama kiumbe tofauti na mwanamme. Mwanamke amesawiriwa kuwa mzinifu, mbaya na muuwaji. Tofauti na Kiango, utafiti huu ulichunguza dhamira zilizomo katika tamathali za usemi. Kiango amemsawiri muhusika wa kike katika njia hasi, sisi kwa kutumia nadharia ya simiotiki tulichunguza lugha ya kitamathali ilivyotumiwa na wahusika wa kike na wakiume kwa njia hasi na chanya ili kuziba pengo lililoachwa.

Masota (1993) amehakiki dhamira katika tamthiliya za Emmanual Mbogo: *Giza Limeingia* (1981), *Tone la Mwisho* (1981), *Watoto Wetu* (1981) na *Ngoma ya*

*Ngwanamalundi* (1988). Masota amehakiki Dhamira katika mazingira ya uyakinifu wa kijamaa. Miongoni mwa dhamira aliyoyahakiki ni ukombozi, usaliti, ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Utafiti wa Masota ulitusaidia sana katika kuibua dhamira za tamthiliya za Emmanual Mbogo ambazo nasi ndizo tulizozijadili. Tofauti na Masota uchunguzi huu ulijikita katika tamthliya ya *Fumo Liongo* na *Morani* kwa kuchunguza vipengele vya tamathali za usemi huku tukilinganisha na kulinganua tamthilya hizo.

Hivyo mtafiti ametumia tamthiliya ili kuweza kuipata hali halisi ya utumzi wa lugha pamoja na kuyaachuguza jinsi yaavyojenga dhamira.

Musyoka (1996) amehakiki fani katika tamthilia nne za Tay Kitsao: *Uasi* (1980), *Malimwengu Ulimwenguni* (1983), *Bibi Arusi* (1983) *na Tazama Mbele (*1983), Msyoka amehakiki vipengele vya fani na madhui kwa kubainisha ufanifu au udhaifu ulioko katika uumbaji wa vipengele vya fani katika usambamba wa msingi na kaida za utanzu wa tamthiliya. Kazi hii inatubainishia kua fani ni uumbaji na ufundi wa kipekee ambao huhusishwa na mtindo wa mwandishi mahsusi kwa jumla. Masyoka ametumia nadharia ya umuundo kutathmini umbuji wa msanii na jinsi fani ilivyoathiri na kuchangia katika kiwango cha kisanaa cha kazi hizo.

Utafiti wa Musyoka ni muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu ulitusaidia kujadili kipengele cha fani hasa katika kipengele cha lugha ambacho ndicho tulichokishughulikia katika uchunguzi wetu. Aidha utafiti wake ulitusaidia kwa vile amechunguza kazi za mwandishi mmoja kama tulivyofanya katika uchunguzi wetu

huu, ambapo tulichunguza tamathali za usemi jinsi zinavyoibua dhamira katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo pekee.

Sarara (1997), amechanganua dhamira katika tamthiliya za Mohammed za *Pungwa* (1988), *Kivuli kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995), amechanganua maudhui katika misingi ya uyakinifu wa kisosholojia, miongoni mwa dhamira alizozichambua ni ufisadi, umasikini na ukombozi. Utafiti wa Sarara umejikita katika kutathmini dhamira kinyume na lengo letu ambapo sisi tulichunguza tamathali za usemi zilizomo katika tamthiliya zilizotungwa na mwandishi mmoja na kujadili kwa kiwango gani tamathali hizo zinasaidia kuibua dhamira za tamthiliya. Kazi ya Sarara ilitusaidia sana katika kuchunguza dhamira zilizojiibua katika tamathali za usemi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo, ingawa yeye ameegemea zaidi katika nadharia ya uyakinifu wa kisoshologia kinyume na sisi ambapo kazi yetu iliegemea zaidi katika nadharia ya simiotiki.

Magare (2002) amehakiki tamthiliya Mohammed *Amezidi* (1995) kwa kutumia nadharia ya udhanaishi kwa kuzingatia kipengele cha ubwege. Magare alichunguza kwa kiasi gani amezidi ni kazi ya kibwege kwa kuzingatia maudhui na fani. Katika utafiti huu mtafiti alitumia nadharia ya simiotiki kuhakiki fani katika kipengele cha tamathali za usemi na kuchunguza kwa namna gani inaibua dhamira. Utafiti wa Magare ulitusaidia sana kuweza kubaini dhamira zilizoibuliwa katika vipengele mbali mbali vya tamathali za usemi.

Katola (2006) ameshughulikia "Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthiliya nne za Kiswahili." Tamthilia hizo ni za waandishi wa jinsia tofauti

ambao ni Muhando, *Hatia* (1972), Mwachofi *Mama Ee (*1987). Hawa ni waandishi wa kike. Waandishi wa kiume ni Mulwa aliandika *Buriani* (1983) na Mohamed *Kitumbua Kimeingia Mchanga,* (2000). Katika kazi yake hakuegemea upande wowote wa waandishi ila ameonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa na mifumo ya kiume katika taasisi ambazo zimejikita kwenye misingi ya ubabe-dume. Baadhi ya dhuluma alizotambua ni wanawake kutishwa, kuteswa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii. Matokeo yake ni mtazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Kazi ya Katola ilikuwa na manufaa kwetu kwani iliibua dhamira mbalimbali kama kazi yetu ilivyonuiya kutumia tamathali za usemi kuibua dhamira ila kazi hii ilijikita katika tamthliya ya *Fumo Liongo* na *Morani* huku ikichunguza mfanano na mlingano wa matumizi hayo ya tamathali za usemi.

Kutokana na utafiti huu mtafiti amejikita katika kpegele ambacho hakikupewa kipao mbele zaidi ambapo watafiti waliotangulia hawakukifayia kazi kiengele hicho kwa ufafanuzi wa kutosha kupitia tamthiliya teule.

Mirikau (2011) alishughulikia taswira ya mwanamke katika tamthiliya za Wamitila. Katika kazi hiyo, Mirikau amejitahidi sana kufafanua istilahi “taswira kwamba, ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Anaendelea kueleza kuwa picha hii aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa kupitia mambo yanayopitikia akilini mwa binadamu. Mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Mwanamke anatendewa na hata mwenyewe huweza kujitendea mambo ya kushangaza katika jamii husika. Anatamatisha kwa kusema kuwa, taswira hii ni kuhusu ngazi katika jamii ambayo

mwanamke hujikuta amewekwa na kukubaliana na uamuzi huo unaomfanya aidha atukuzwe au adhalilishwe na hata kujidhalilisha mwenyewe.

Mawazo ya Mirikau yalitusaidia kuchunguza tamthiliya zetu teule ili kuyafikia malengo yetu ingawa yeye ametumia taswira kuchunguza nafasi ya mwanamke sisi tulitumia tamathali za usemi kama ni kipengele cha fani ili kujadili kwa namna gani tamathali zinasawiri dhamira za kazi ya fasihi huku tukitumia nadharia ya simiotiki ambayo itatupa picha halisi ya dhamira katika tamthiliya teule ambaz kwazo azikujadiliwa kwa kina kupitia muandishi wake mahiri kwa upande wa fani hii muhimu katika kazi za fasihi.

Nguta (2011) ameangazia fanina usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *PangoNa Mama Ee*. Kazi yake ni muhimu kwetu kwa kuwa yeye ameangazia 'fani' na vipengele vyake vyote. Sisi pia tulijikita katika tamthiliya za Profesa Emmanuel Mbogo, tofauti na Nguta utafiti huu ulikusudia kuchunguza kipengele cha fani cha tamathali za usemi pekee. Nguta ametumia nadharia mbili ambazo ni urasimu (ufani) na ile ya ufeministi. Sisi tulitumia nadharia ya Simiotiki. Kwa mukhutasari, kazi ya Nguta imeangazia baadhi ya vipengele tulivyodhamiria kuangazia hivyo basi vilitunufaisha kwa njia moja au nyingine hasa kwa vile Nguta amejadili jinsi wahusika wanavyotumia lugha katika mazungumzo baina yao na uzungumzi nafsia (balagha).

Abbas (2015) amefanya utafiti juu ya ''Uchunguzi wa Tamathali za usemi katika kuibua dhamira katika tamthiliya, ulinganishi wa Morani na Fumo Liongo'' utafiti

huu ulibaini kuwa, tamthiliya hizo zinafanana katika matumizi na dhamira za tamathali za usemi. Ilielezwa na wahojiwa kuwa msanii ametumia tamathali za usemi kwa lengo la kuibua dhamira za kazi zake za sanaa. Aidha, ilielezwa kuwa msanii anatumia sitiari zaidi kama mbinu kuu ya mtindo katika kuibua dhamira wakati tamathali zingine za usemi zinatumika kama kijenzi cha tamathali kuu. Kwa maana hiyo, utafiti huu ulibaini kuwa sitiairi ndiyo inayobeba dhamira kuu ya kazi zote zilizochunguzwa.

Aidha, kufanana kunajitokeza pia katika dhamira zinazoibuliwa na tamathali za usemi. Ilielezwa na wahojiwa kuwa katika tamthiliya zote msanii ametumia tamathali ya usemi ya sitiari kuibua dhamira za ushujaa na uzalendo, kutokuthaminiwa kwa wananchi, ukatili na ushenzi, mauwaji yasio na hatia, ujinga, uzalendo na mapenzi ya nchi, ujasiri na ukakamavu, udikteta, tamaa na usaliti, uaminifu, ulaghai, na vuguvugu la kurejesha nyuma harakati za ukombozi.

Licha ya kwamba matumzi ya lugha yameendelea kukua na kuenea zaidi katika jamii zetu za Tanzania na hadi kufikia kutumika kazi za kifasihi kwa ustadi wa hali ya juu zaidi. Tafiti za watafiti waliotangulia hazijajitosheleza zaidi kwani bado kuna maeneno mengi yanahitaji kufanyiwa utafiti kwa uelewa wa mtafiti hadi sasa kuna tafiti chache sana ambazo zimejaribu kutafiti baadhi ya vipengele vya matumizi ya lugha ambapo yaelekea kuwa ni maeneo machache ambayo watafiti hujikita nayo zaidi na sio kuingalia kwa undani zaidi nafasi hii ya kipengele cha matumizi ya lugha, "Matumzi ya lugha katika Tamthiliya za Muandishi Emmanuel Mbogo," utafiti huu utaangalia zaidi vitabu viwili vya tamthiliya ya ''Fumo liongo na

tamthiliya ya Sadaka ya John Okello,’’kupitia kazi mbili hizi mtafiti ataangalia zaidi matumizi ya lugha yanavyojitokeza katika Tamthiliya na kufafanua sababu za kutumia matumizi hayo ya lugha. Kupitia Tamthilia hizo zilizotajwa hapo juu.

## 2.4 Tafiti kuhusu Matumizi ya Lugha

Ligembe (1995) amechambua matumizi ya sitiari katika kazi ya ya *Lina Ubani* iliyoandikwa na Penina Muhando. Katika uchunguzi wake amejadili muundo na umbo la tamthiliya ya Kiswahili. Amebainisha kiungo, kifananishi na kizungumzwa na kuelezea mchango wake katika uelewa wa tamthiliya. Tofauti na watafiti wengine Ligembe (keshatajwa) amejikita zaidi katika umbo la tamthiliya ya Kiswahili na kubinisha aina za sitiari. Utafiti wake haukuonesha uhusianao uliopo baina ya aina ya sitiari na ujenzi wa dhamira katika tamthiliya. Kwa upande wetu tulichunguza dhamira zinazodokezwa katika tamathali za usemi mbali mbali na si sitiari peke yake.

Hata hivyo utafiti huu umeweza kumsaida mtafiti kuliona pengo ambalo limejitokeza katika kuichunguza lugha kwa kuvitathmini vipengele hivi vya lugha na kuweza kuyabainisha mifano mbali mbali iliyojitokeza na kuweza kuona jinsi gani matumizi hayo ya lugha yamejenga dhamira zilizolengwa na muadishi kupitia wahusika na uhusika wao kuligana na muktadha ulijegwa na msanii.

Ramadhani (2005) alifanya utafiti wa matumizi ya sitiari katika tamthiliya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na *Ngoma ya Ng’wanamalundi* ya Emmanuel Mbogo. Utafiti wake ni utafiti linganishi wa kielimumitindo ambapo analinganisha tamthiliya mbili. Aidha katika ulinganishi hakuwa mbali na hitimisho la Mosha kuwa sitiari sahili

ndiyo yenye mdafao mkubwa kuliko sitiari zingine katika tamthiliya zote. Aidha alihitimisha kuwa sitiari hutumika katika ujenzi wa dhamira mbalimbali katika tamthiliya zote mbili. Kwa utafiti huu amabao umelenga zaidi matumzi ya sitiari, matafti amelipata pengo litokanalo na ufinyu wa uchunguzi wa matumizi ya lugha na alishajihika zaidi katika kuchunguza dhamira zilizomo katika tamathali za usemi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo.

Omari (2006) aliandika makala juu ya mitindo na matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya Tanzania. Katika makala hii amebainisha jinsi wasanii wa muziki wa kizazi kipya wanavyoitumia lugha katika kazi zao. Amebainisha matumizi ya lugha ya majigambo, nyimbo za watoto, kuchanganya lugha, lafudhi mbalimbali, taswira, misimu au misemo, tashihisi, lugha isotafsida, tanakali sauti, methali, takriri, sitiari, tashibiha na utohoaji wa maneno. Hivyo, katika kazi yake hakuonesha ni jinsi gani lugha inatumika katika ujenzi wa maana, ujumbe na dhamira za kazi za fasihi. Katika utafiti huu tulichunguza dhamira zinazopatikana katika tamathali za usemi katika tamthiliya mbili za Emmanuel Mbogo kwa kuegemea katika nadharia ya simiotiki.

Hivyo mtafiti alitumia tafiti zilizotangulia na kuweza kuliona pengo la utafiti ambalo limejitokeza na kulitaftia utatuzi wake kwa kuingia katika kuchunguza matumizi ya lugha na dhamira zilivyojengwa kupitia matumizi ya lugha husika.

Jilala (2008) alifanya utafiti juu ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa kuchunguza jinsi wasanii wanavyotumia sitiari kisanii katika ujenzi wa maana

na ujumbe. Katika utafiti wake alihitimisha kuwa sitiari pana ndiyo yenye mdafao mkubwa zaidi ya sitiari sahili na changamano. Hii ni kwa sababu nyimbo za kizazi kipya hutumia vipengele vya lugha kisanii katika kujenga maana na ujumbe. Aidha anaongeza kuwa sitiari hutumika katika kujenga maana na ujumbe na vilevile dhamira mbali mbali katika kazi za fasihi huibuliwa kutokana na sitiari iliyotumika. Jilala anaendelea kusema kuwa muktadha wa utumizi, uzoefu, maarifa na ujuzi na utamaduni wa jamii iliyomlea msanii na hadhira yake ndiyo huongoza katika tafsirip ya maana ya sitiari na ubuniji wa kazi ya fasihi. Jilala amejikita katika sitiari pekee, ambapo mtafiti aliezisoma kazi zilizotangulia amekusudia kulitafuta pengo la utafiti amelipata na mtafiti amejikiza zaidi katika kuutafuta utatuzi wa tatizo la utafiti na ameendelea na utatuzi wa tatizo katika kuchunguza tamathali mbali mbali za usemi kwa kuzilinganisha tamthiliya mbili za mwandishi mmoja. Utafiti huu umetoa changamoto kubwa kwa mafiti kuufanya utafiti huu.

Wanyonyi (2009) alihakiki riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ya Said Ahmed Mohammed. Katika kazi yake alishughulikia matumizi ya lugha ya kitamathali kama vile tafsida, ishara za uwashiriaji na maswala ya balagha. Vilevile, aliangazia kazi yake kwa mtazamo wa Saikolojia Changanuzi. Ingawa kazi ya Wanyoni ni katika utanzu wa riweaya lakini ilitusadia sana katika kubaini vipengele vya tamathali za usemi ikiwa ni sehemu ya vipengele kama hivyo ndivyo kazi hii ilivichunguza, ingawa kazi hii iliegemea katika utanzu wa tamthiliya kinyume na kazi ya Wanyoni ambayo iliegemea katika utanzu wa riwaya. Aidha kazi yetu ilijikita katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo ambapo tulitumia nadharia ya simiotiki kinyume na

Wanyonyi ambae ametumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Hivyo utafiti huu unatowa msukumo kwa mtafiti kufanya uchunguzi zaidi wa matumizi wa lugha kwa mchanganuo wa kipenele cha lugha na dhamira zilizojengwa kwa kila kipengele kama zilivyojitokeza.

Jilala (2011) katika makala yake ya lugha na ujinsia katika ushairi ambapo alifanya uchunguzi wa sitiari za UKIMWI na mapenzi katika mashairi ya Bongo fleva, Jilala anajadili kuwa katika mashairi ya Bongo fleva sitiari zinazomrejelea mwanamke zimebeba dhana nne ambazo zimeundwa kitaswira kumuashiria mwanamke na nafasi yake katika jamii. Dhana hizo ni thamani, unyenyekevu, utamu na mvuto. Dhamira hizi alizoziibua zilitusaidia sana katika kujadili dhamira zilizojiibua katika tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani* na *Fumo Liongo. Kutokana na utafiti uliotangulia pamoja na uchanagnuzi wake inadhihrsha kwamba mtafiti ametumia kufanyia kazi tamthiliya za muandishi katika kuipa kipaombele lugha na kuifanyia kazi tunu hii ya matumizi ya lugha ili kupatia nafasi muhimu pamoja na kuzichambua dhamira zilivyojengwa.*

Too (2011) alitafiti tamthiliya ya *Nguzo Mama* (1982) ya Penina Muhando. Alitumia nadharia mbili ambazo ni Umuundo na Semiotiki kuchanganulia mbinu anuwai za lugha. Mbinu hizi ni pamoja na tamathali za usemi kama vile tashbiha, sitiari, chuku, majazi, tanakali sauti na mbinu nyingine za lugha. Ingawaje utafiti huu kwa ujumla uligusia vipengele ambavyo tulivishughulikia, kazi yetu ililenga tamthiliya za Emmanuel Mbogo ambapo tulijadili vipengele maalum vya lugha ikiwa ni vipengele vya tamathali za usemi miongoni mwa vipengele hivyo ni tashbiha, sitiari, takriri na

tashihisi. Kubwa zaidi Too alitumia nadharia ya simiotiki na umuundo wakati uchunguzi ulitumia nadharia ya simiotiki pekee kuibui na kuchambua dhamira. Hata hivyo mtafiti alitafuta vionjo mbali mbali vya lugha vinavyojitokeza katika kazi za fasihi ili kuipa nafasi stahiki pamoja na kuzichambu na dhamira zake ambazo kwazo watafiti waliotangulia wamezitaja tu au kuzigusia moja moja au mbili mpaka tatu na hawakujifaraguwa zaidi katika kuiangalia lugha kwa upana zaidi.

## 2.5 Mkabala wa Kinadharia

Kwa mujibu wa Masamba (2009) Nadhariya ni taratibu, kanuni na misingi iliyojengwa kwa pamoja kiukamilishano kwa madhumuni ya kuwa kigezo cha kuelezea jambo au mambo kadhaa.Wanjala (2011) anaeleza kuwa nadhariya hii ni muongozo wa mawazo au marrifa yanayotumiwa na binaadamu kwa kukabiliana na mazingira yake. Au ni mfumo wa mawazo au maarifa yanayofasili taaluma mahsusi kwa kutoa maoni, mtazamo au falsafa juu ya matumzi na taratibu za utafiti.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) nadhariya ni sayansi au sanaa inavyohusika na kanuni za kiujumla na mikabala fulani au hata kanuni fulani zinazotumiwa katika uchunguzi wa suala fulani. Nae Sengo (2009) anaeleza kuwa nadhariya ni wazo kuu fikra kuu au muongozo mkuu wa mtu / watu ambao hufuatwa na watafiti wakati wa kuchambua kazi za kifasihi ili kuwaongoza katika kazi zao za utafiti.

## 2.6 Nadhariya ya Simiotiki

Ferdinand de Saussure na Charles Pierce ni waasisi wa nadharia hii ya Semiotiki. Saussure katika nadharia hii ameeleza dhima ya ishara katika jamii na Pierce amezungumzia maana halisi ya lugha ya ishara inavyohusiana kimantiki na


utamaduni wa jamii fulani kwa madhumuni ya kutoa maana maalum. Blamires (1991) amewanukuu Geoffrey, Hill, Paul na Hold wanazuoni wa Chuo Kikuu cha Yale, wakisema matini moja yaweza kuwa na fasili nyingi zinazolingana au kukinzana na zote zikakubalika.

Kwa mujibu wa wavuti (http://oak.cats.ohiou.edu/~mv537899/sc.htm) nadharia ya simiotiki husisitiza kuwepo kwa ujumbe kila mahali. Kwa hiyo, inatarajiwa kuwa kila usemi itaangaliwa kwa jicho la ndani ili kupata maana au ujumbe fulani. Katika kuchunguza athari za nadharia ya simiotiki kwa jamii, Krawsczyn (2006) anadai kuwa nadharia ya simiotiki inaweza kuleta mabadiliko katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii kwa kuwa itawatia motisha wanajamii kuchunguza mazingira yao kwa jicho pekuzi huku wakizingatia kuwa kila usemi haukosi maana. Isitoshe, simiotiki itawafanya wanajamii kuwa makini zaidi wanapoelewa kuwa ishara ndogo au sahili ina uwezo wa kubeba ujumbe muhimu. Kama tamthiliya ni mchakato wa kueneza ujumbe kutoka kwa mwandishi wake au mtunzi hadi kwa hadhira, basi nadharia hii ya simiotiki inahusu kueneza ujumbe uliosimbwa katika semi mbali mbali ili kumfikia hadhira. Mwananadharia wa Marekani, Pierce (1839 – 1914) amewasilisha nadharia ya simiotiki kwa kutumia umbo lifuatalo: Jambo/ kitu/umbo Ishara (maneno, rangi na mtindo) Mfasiri. Katika umbo hili kuna uhusiano baina ya ishara, kitu/jambo linalowasilishwa na mfasiri anayeipa ishara maana. Mfasiri huweza kuwa aliyesimba ujumbe au atakayesimbua ujumbe huu.

Kuzuka kwa nadhariya hii kunahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970.

Wakati huo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi nakuuacha umuundo ambao ulikuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Licha ya kuzuka kwake wakati huo, semiotiki ameieleza zaidi kutokana na mawazo ya mwana isimu wa Ki- Swizi, Ferdinand desaussure, pamoja na mwanafalsafa wa Ki-Marekani kwa ishara kinachohusishwa na pembe tatu.

*Ishara (sign)*



*Yambwa (object)* *Kifasiri (interpretant).*

Wamitila (2002) anasema nadharia hii imetumika sana katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, ambapo inashughulikia ishara na uashiriaji. Ishara zinazojitokeza katika kazi za kifashi huundwa na mtunzi (msanii) kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. (Wamitila ameshatajwa) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili, ambavyo ni kitaja (a signifier) yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejelee (a signified) yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo.

Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja na kirejelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao.

Nadharia ya Semiotiki imejengwa kwa mihimili mitano ikiwa ndio misingi yake katika kuzifumbua ishara zilizotumika katika kazi ya fasihi. Misingi hiyo ni muktadha, ujumbe, msemaji, mpokeaji na lugha.

Barthes (1994) anaeleza kwamba, kuna aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi ya kifasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Semiotiki. Mhakiki huyu alizuka na dhana hii kupendekeza jinsi bora ya kuisoma kazi ya kifasihi au matini ya kifasihi. Lengo la Barthes (ameshatajwa) ni kuivunja matini ya kifasihi kwenye sehemu ndogo ndogo alizoziita leksia. Hivi ni kama vitengo vidogo vya kisomaji ambavyo vina urefu sawa. Kwa mujibu wa mawazo yake, kila leksia hudhihirisha misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri. Aina tano kuu za misimbo imeishia kuitwa 'misimbo ya usomaji' na ni nguzo muhimu katika nadharia hii. Aina hizo za misimbo ni msimbo wa kimatukio, kihementiki, kiseme, kiishara na kirejelezi.

Msimbo wa matukio: unahusu jinsi matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na kusababishana au kuathiriana katika mashairi husika (Omari, 2015). Imezoeleka kuona wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wakihusisha dhana ya matukio na vitushi na tanzu za riwaya na tamthilia kuliko ushairi (Njogu na Chimera, 1999). Hata hivyo tunafahamisha kwamba, hata katika ushairi wa Kiswahili ambamo ndani yake kuna kipera cha nyimbo kuna matukio mbali mbali yanayotokea hususani katika tamthiliya kupitia kipengele cha matumizi ya lugha, ambapo kunapatikana hadithi au simulizi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari.

Msimbo wa kihementiki: unahusu taharuki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia au kutamba hadithi. Kimsingi, msimbo wa kihementiki

humfikirisha msomaji juu ya kile anachokusudia kukisoma au kukitafiti. Katika utafiti wetu tuliongozwa na msimbo huu katika kujua kilichokuwa kinataka kusimuliwa na wasanii. Kwa mfano, msemo uliojitokeza katika mtamthiliya ya fumo liongo ‘ukimng’ata kwa meno, yeye atajing’atua kwa maneno tu, kupitia msomaji wa tamthilya hii atakuwa na shauku ya kutaka kujuwa kwa nini yametumika maneno hayo? Yanahusianaje na muktadha yaliyotumiwa na ni muhusika gani huyo? Katika kutaka kufahamu majibu ya maswali haya msomaji hulazimika kuisoma sehemu nzima ya tukio ili apate majibu yake.

Msimbo wa kiseme: kwa asili unatokana na neno sema. Wamitila (2002) anaeleza kwamba neno sema hutumiwa kuielezea elementi nasibishi ya kisemantiki, hizi ni elementi ambazo zinatuwezesha kupata picha fulani, kutokana na viashiria fulani hupelekea kuelewa sifa kamili ya jambo, tukio, hali au muhusika fulani wa kazi ya fasihi. Kupitia msimbo huu tulinasibisha baina ya vitu, watu, tukio na hali zinazojitokeza katika tamthiliya na kuihusisha na hali iliopo katika jamii.

Msimbo wa kiishara: ni msimbo muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi kwani unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavumbua maana za kiishara katika kazi ya kifasihi (Omari, 2015).

Msimbo kirejelezi: huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika ya kifasihi. Wamitila (2002) anaeleza kwamba, urejelezi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi fulani nguzo za kiutamaduni.

Nadharia ya Simiotiki imeteuliwa kutumika katika kuchambua data za utafiti huu kwa sababu inahusiana moja kwa moja na mada ya utafiti huu. Utafiti huu unahusu matumizi ya lugha na nadharia ya Simiotiki inahusu inazungumzia juu ya lugha ya picha, ishara, taswira na mafumbo. Hivyo, kupitia nadharia hii tumeweza kuchambua matumizi ya lugha na vile yalivyochangia katika kuwasilisha dhamira ndani ya tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii ya pili ya tasinifu yetu imeasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Tumetoa historia fupi ya utanzu wa tamthiliya, kazi tangulizi zilizotafiti matumizi ya lugha katika nyanja mbalimbali na kisha kazi tangulizi zilizohusiana na tamthiliya ya Kiswahili. Kwa jumla, tumebaini kuwa hakuna utafiti hata mmoja ambao umefanywa kwa lengo la kushughulikia matumizi ya lugha katika tamthiliya za Sadaka ya John Okello na Fumo Liongo. Pia katika sura hii tumeilezea nadharia ya Simiotiki kuwa ndiyo iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha mbinu za utafiti kama vile; eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, mbinu ya usomaji makini, usaili, maadili ya utafiti pamoja na makadirio na muda wa utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti ni lazima ufanyike katika eneo maalum. Eneo la utafiti ni sehemu ambayo mtafiti amefanyia utafiti wake, ikihusisha zaidi sehemu ambazo mtafiti amezitumia kukusanya data kwa ajili ya utafiti wake. Sehemu kubwa ya utafiti ilikuwa ni mapitio ya maandishi na hivyo maktaba mbali mbali zilitumiwa na mtafiti katika kupata data muhimu. Utafiti huu ulifanyika Unguja, katika maktaba za tawi la Chuo Kikuu Huria lililopo Beit-el-Raas pamoja na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Mtafiti pia alikusanya data kwa kusoma na kuchambua maandiko mbalimbali kutoka katika maktaba mbali mbali kama vile Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Maktaba Kuu ya Zanzibar na mapitio mengine yatokanayo na tafiti mbali mbali zilizofanywa na wataalamu na wanafunzi mbalimbali zinazohusiana na mada husika. Kwa vile utafiti huu kwa sehemu kubwa ni utafiti wa Maktabani, maeneo hayo yalichaguliwa kutokana na ukweli kuwa ni sehemu muhimu ambazo mtafiti aliweza kufanya mapitio ya kazi mbalimbali kwa mujibu wa utafiti wake.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti unaelezwa na Babbie (1999) kuwa ni ramani inayoeleza namna utafiti husika utakavyofanyika kuanzia katika kukusanya data za utafiti mpaka kuzichambua na kuandika tasinifu. Kuna aina mbalimbali za usanifu wa utafiti lakini katika tasinifu yetu tumetumia usanifu aina ya uchunguzi kifani. Uchunguzi Kifani ni mbinu ya kukusanya data za utafiti kwa mtafiti kuteua mahali au kitu maalumu cha kukifanyia utafiti kulingana na malengo ya utafiti wake (Kothari, 2008). Katika utafiti huu tuliteua tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Fumo Liongo* kwa lengo la kuchunguza matumizi ya lugha na namna matumizi hayo ya lugha yalivyosaidia katika kujenga dhamira katika tamthiliya hizo. Usanifu wa uchunguzi kifani umetusaidia kupata data za utafiti kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

## 3.4 Kundi Lengwa

Kundi lengwa huhususha watu au vitu ambavyo vimeteuliwa kuwa ndio watafitiwa katika utafiti husika (Robson, 2007). Kundi lengwa katika utafiti wetu ni tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Fumo Liongo* zilizotungwa na Emmanuel Mbogo. Tamthiliya hizi zimeteuliwa mara baada ya kujiridhisha kuwa bado hazijafanyiwa utafiti kama huu na hivyo ni muhimu kwetu kufanya utafiti ili hatimaye tutambuwe matumizi ya lugha yaliyopo katika tamthiliya hizi kwa lengo la kukuza zaidi maarifa na ujuzi kuhusu tamthiliya ya Kiswahili.

## 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti wowote ule wa kitaaluma ni lazima uwe na sampuli ya watafitiwa ambao watatumika katika kutoa data za utafiti. Sampuli ni sehemu ya watafitiwa kutoka

katika kundin kubwa la wanajamii ili kuwa ndicho kiwakishi cha jamii nzima katika utafiti kama watafitiwa (Babbie, 1999). Sampuli ya utafiti huu ni tamthiliya mbili zilizotungwa na mwandishi Emmanuel Mbogo. Tamthilia hizo ni *Sadaka ya John Okello* na *Fumo Liongo* ambazo zimeteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Usampulishaji lengwa ni mbinu ya kuteua sampuli kwa makusudi mtafiti akiwa na uhakika kuwa sampuli hiyo ndiyo pekee itakayompatia data za utafiti. Usampulishaji lengwa ni mbinu nzuri ambayo humfanya mtafiti kupata data za uhakika kwa muda mfupi na gharama kidogo.

## 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti huu ulikusanya data za msingi na upili ambazo kimsingi ndizo aina za data zinazojenga utafiti wa kitaaluma.

### 3.6.1 Data za Upili

Data za upili ni aina ya data ambazo tayari zipi maktabani katika machapisho, majarida, vitabu, makala, tasinifu, magazeti na vipeperushi. Hizi ni data ambazo tayari kwa matumizi ya watafiti wengine wa baadaye. Data hizi husaidia katika uoanisha na data za msingi za utafiti kwa lengo la kuzipa nguvu zaidi na kuzifanya ziaminike kitaaluma. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

### 3.6.2 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine akiwa na malengo ya utafiti kama huu wa kwetu

(Kothari, 1990). Data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa katika tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Fumo Liongo* za Emmanuel Mbogo.

### 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (1990), anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data, kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika lengo lake la utafiti. Aidha, Kothari anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua ya ukusanyaji wa data. Hivyo, katika kukusanya data za utafiti huu tulitumia mbinu tatu ambazo ni; mbinu ya usomaji makini, upitiaji wa nyaraka. Sehemu ifuatayo imewasilisha mbinu hizo na namna zilizotumika katika utafiti huu.

#### 3.7.1 Usomaji Makini

Jilala (2014) anaifafanua mbinu hii kuwa, huhusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika vile vitabu vya mashairi, riwaya, tamthiliya au hadithi fupi. Mbinu hii ilitumika kukusanya data kutoka katika tamthiliya za *Sadaka ya John okello* na *Fumo Liongo* pamoja na kupitia machapisho, kama vile vitabu teule, majarida, pamoja na tasnifu zinazohusina na mada yetu ili kupata data zinazohusiana na matumizi ya lugha katika tamthiliya hizo.

Kwa ujumla mbinu hii ilitusaidia kupata data za kutosha kuhusu tamathali za usemi katika utunzi wa Emmanuel Mbogo. Kwa kufanya hivi, tuliweza kukusanya data za kutosha ingawa bado tuliona kuwa hatuwezi kutumia mbinu hii pekee katika kukusanya data zote za utafiti huu. Hivyo, tulitumia pia mbinu ya upitiaji wa nyaraka katika kukusanya data za upili za utafiti huu.

### 3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka

Hii ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa kusoma nyaraka mbalimbali maktabani ambazo zinahusiana na mada ya utafiti husika (Babbie, 1999). Nyaraka zinazopitiwa huwa ni vitabu, makala, tasinifu, magazeti, majarida, vipeperushi na maandiko yanayopatika katika tovuti na wavuti. Katika utafiti wetu tulitumia mbinu hii kukusanya data za upili ambazo tulizitumia kukazia maarifa na hoja zilizoibuliwa kutokana na data za msingi za utafiti wetu. Kwa kuwa data hizi hukusanywa maktabani, nasi tuliteua maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maktaba ya Chuo Kiuu cha Taifa cha Zanzibar na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data hufanywa mara baada ya data kukusanywa na kupangiliwa katika mpango mzuri na rahisi kwa uchambuzi. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kutolea ufafanuzi data zilizokusanywa ili ziweze kutimiza lengo kuu la utafiti (Kothari, 1990). Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Hii ni mbinu ya kuchambua data za utafiti kwa kuzielezea kwa maneno kwa kuzingatia malengo ya utafiti husika. Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti ambapo data za kila lengo zilichambuliwa kwa mbinu ya kimaelezo.

## 3.9 Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Talcot (2010) maadili ya utafiti huhakikisha usalama wa watafitiwa pamoja na udhibiti wa data zinazokusanywa, na kujumuisha mambo kama kuomba

ruhusa ya kukusanya data, idhini ya wata fitiwa, udhibiti wa data pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Katika kufanya Utafiti huu mtafiti alijitahidi sana kufuata maadili yote ya utafiti kadiri ilivyowezekana. Maadili hayo ni pamoja na kupata ruhusa ya maandishi kutoka Chuoni ya kumuwezesha kufanya Utafiti huu pamoja na kuomba ruhusa katika taasisi zote zilizopangwa kutembelea katika kutafuta data za utafiti huu.

## 3.10 Hitimisho

Sura hii kwa ujumla imewasilisha vipengele mbalimbali vya mbinu za utafiti ambazo zilitumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wetu. Vipengele hivyo ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji na aina ya data zilizokusanywa. Pia, vipengele vya mbinu za kukusanya data, kuchambua data na maadili ya utafiti vimewasilishwa katika sura hii.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Lego la sura hii ni kuwasilisha wasifu wa mtunzi wa tamthiliya hizi mbili na kuchambua data zilizokusanywa juu ya matumizi ya lugha katika Tamthiliya za maandishi Emmanuel Mbogo katika vitabu vyake viwili vya tamthiliya ikiwemo *Fumo Liongo* na *Sadaka ya John Okello*. Kutokana na ukaribu wa kimantiki wa malengo mahususi ya utafiti huu tumeona kuwa ni vema tuyaunganishe katika uchambuzi wa data. Hii ni kutokana na ukweli kuwa lengo mahususi la kwanza lililenga kubainisha matumizi ya lugha katika tamthiliya teule na wakati hilo likifanyika bila shaka dhamira zibebwazo na matumizi hayo ya lugha nazo zinaelezwa hapohapo. Data zote zilizokusanywa zitawalishwa na kuchambuliwa kwa kina katika sura hii.

## 4.2 Emmanuel Mbogo ni Nani?

Profesa Emmanuel Yakobo Mbogo ni mtunzi na mwandishi wa tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Ni msomi na Profesa wa sanaa za maonyesho na Fasihi ya Kiswahili. Wakati wa usaili na msanii huyu, tuliweza kupata usuli wa maisha yake na utunzi kwa ujumla. Kutokana na maelezo yake, Emmanuel Mbogo alizaliwa tarehe 01/03/1947 katika wilaya ya Kongwa, mkoa wa Dodoma. Alisoma katika shule ya msingi Mpwapwa na kuhitimu darasa la nane mwaka 1963. Baadaye alijiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Indian ( kwa sasa

inajulikana kama Shule ya Sekondari Dodoma) na kuhitimu mwaka 1967.

Wakati akisubiri matokeo yake, ya mtihani wa Sekondari alifanya kazi ya ukarani katika Wizara ya Kilimo, mkoani Dodoma. Baada ya kufaulu mwaka 1968, alijiunga na Chuo cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA na kuhitimu mwaka 1969. Akiwa chuoni hapo, ndipo alipogundua kipaji chake cha uandishi. Hii ni baada ya kuandika hadithi aliyoiita *James I Die of Love* (1968) katika jarida la chuo lililokuwa linaitwa *Morani*, hadithi hiyo iliwavutia wasomaji na kusifiwa sana na mwalimu wake wa Fasihi ya Kiingereza na wanachuo wenzake.Hadithi hii ndiyo iliyomtanabaishia uwezo wake wa kutunga hadithi na kumpa hamasa na ari ya kuingia katika ulimwengu wa sanaa na utunzi.

Mwaka 1970, alipangiwa kufundisha katika shule ya msingi Mwitikira iliyopo mkoani Dodoma. Akiwa anaendelea kufanya kazi, alijiunga na Chuo cha Rapid Results College kilichopo nchini London kwa mfumo wa elimu masafa, na kusomea masomo ya Kiswahili na Jiografia kwa lengo la kuongeza alama zitakazomwezesha kujiunga na masomo ya stashahada. Wakati huohuo akiwa katika shule hiyo, alitunga tamthiliya yake ya kwanza aliyoiita *Mama Tamasha* (1970).Mwaka1971alihamia katika shule ya msingi Nara.

Akiwa katika shule ya msingi Nara, aliufanyia mazoezi mchezo huo na wanafunzi wake darasani, lengo likiwa ni kusikiliza namna unavyosikika katika mazungumzo na vitendo. Mchezo huo uliigizwa mwaka 1972 alipokuwa akifundisha shule ya Msingi Bwigiri. Wakati huo yeye na kundi lake la waigizaji ambao ni wanafunzi

wake, walitembea na kuigiza mchezo huo katika vijiji na shule mbalimbali kwa kutumia usafiri wa magari yaliyokuwa yanahamishia watu kwenye kijiji vya ujamaa. Mchezo huu aliubadili jina na kuuita *Watoto Wetu* (1972).

Mwaka 1973 alijiunga na masomo ya stashahada ya ualimu na sanaa za maonyesho katika Chuo cha Ualimu Chang'ombe, kilichopo jijini Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 1974. Baada ya kumaliza mafunzo ya stashahada, alipangwa kufundisha katika Chuo cha Ualimu Katoke, ambapo alifundisha hadi Juni 1976, alipojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kusomea shahada ya kwanza na ya pili katika Sanaa za Maonyesho (B.A in Theatre Arts na M.A in Theatre Arts). Akiwa chuoni hapo, alitunga tamthiliya yake ya pili iliyoitwa *Tone la Mwisho* (1981). Akiwa bado mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam alitunga tamthiliya nyingine iliyoitwa *Giza Limeingia* (1977), ambayo ilivutia na kuonyesha uwezo na kipaji chake.Yeye ndiye alikuwa mwongozaji wa tamthiliya hiyo iliyoigizwa katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam.Mbogo, alihitimu masomo yake ya shahada ya Sanaa za maonyesho mwaka 1981.Mwaka 1982 alijiunga na Chuo Kikuu cha Humboldt kilichopo mjini Berlin nchini Ujerumani, kwa masomo ya shahada ya tatu katika sanaa za Maonyesho (PhD in Theatre Arts) na kuhitimu mwaka 1984.

Baada ya kumaliza masomo yake alirudi nchini Tanzania na kufanya kazi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), ambayo kwa sasa inatambulika kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi mwaka 1989. Mwaka 1990, alikwenda nchini Kenya na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Moi hadi mwaka 1991. Mwaka 1992 alihama na kwenda kufundisha

katika Chuo Kikuu cha Maseno kilichopo Kisumu hadi mwaka 2002, kisha mwaka 2003 alihamia Chuo Kikuu cha Kenyata ambapo alifundisha hadi mwaka 2006. Baada ya hapo mwaka 2007 alikwenda nchini Rwanda na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Kigali kwa muda wa mwaka mmoja. Mwaka 2008 alirudi nchini Tanzania na kujiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ambapo yupo hadi sasa akiwa ni mhadhiri chuoni hapo.

Mtunzi ameshatunga vitabu kadhaa vya riwaya na tamthiliya. Tamthiliya alizokwishatunga na kuzichapisha ni *Watoto Wetu (1972), Giza Limeingia (1980), Tone la Mwisho (1981), Ngoma ya Ng'wanamalundi (1988)*, *Morani (1993), Fumo Liongo (2009), Sundiata (2011), Sadaka ya John Okelo (2014) na Nyerere na safari ya Kanaani (2015).* Vilevile ametunga tamthiliya iitwayo *Tunuafrika-Wangari Maasai (haijatoka)*Pamoja na tamthiliya hizo, ametunga pia riwaya kama vile *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Vipuli vya Figo*(2008) na *Siri ya Maisha*(2010). Katika utafiti huu tulichagua tamthiliya zake mbili *Fumo Liongo na Sadaka ya John okello* kama ilivyojadiliwa katika sura zilizotangulia. Kwa hiyo mjadala wetu utajikita katika tamthiliya hizo mbili.

### 4.3 Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya Teule

Kipengele hiki kitahusisha matumizi ya lugha yalivyojitokeza katiika vipengele mbali mbali ikiwemo matumizi ya lugha ya lugha picha, lugha ya ishara, misemo, kejeli, ishara, Takriri, Mdokezo, tanakali sauti, na taharuki pamoja na dhima zake ambazo zimejengwa kupitia matumizi hayo ya lugha katika tamthiliya hii ya Fumo Liongo.

Hivyo basi katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambayo muandishi Emmanuel Mbogo ameifanyia kazi Tamthiliya hiyo kuna matumizi ya lugha mbali mbali ambayo ameyatumia kulingana na wahusika, muktadha au Mazingira ambayo yameizunguka jamii ya Pate, iliyozungukwa na uongozi wa Mtawala Daudi Mringwari aliitawala Pate kwa imla na khofu iliyotokana na umaarufu wa Nduguye Fumo Liongo aliyekuwa shujaa vitani, aliyependwa na watu, malenga stadi na mkosoaji wa siasa za Sultani. Hivyo basi, uchambuzi huu umeyachambua matumizi hayo kwa kukipitia kipengele kimoja kimoja ili kuyaweka wazi matumizi hayo ya lugha. Matumizi ya lugha ndani ya Tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambayo mtafiti ameyafanyia kazi na kuyabainisha pamoja na dhamira zake ni kama vile; matumizi ya lugha ya picha, misemo, kejeli, ishara, takriri, mdokezo, tanakali sauti, taharuki na tash-hisi.

### 4.3.1 Lugha ya Picha

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (2008) lugha ya picha/taswira hutumika kuleta picha au hali fulani akilini mwa msomaji au msikilizaji, anaweza kuona, kusika, kuonja, kunusa, kupenda au kuchukizwa au kudharau kilchosawiriwa kutegemea nguvu za taswira zilizotumika. Neno hili 'taswira' linatokana na "sura" yaani "picha".

Hivyo basi kadiri muandishi anavyoweza kueleza habari ambapo msomaji au msikilizaji akaweza kujenga mawazo ya waziwazi kuhusu habari hiyo. Muandishi anaweza kueleza kuhusu hisia zake, mji au mahali fulani, wasifu wa mtu, mnyama au hata hali ya matokeo mbali mbali. Yote haya huelezwa kwa maneno yanayoweza kuibua hisia na kuchora picha hiyo katika akili ya msomaji au msikilizaji. Ili

kuthibitisha haya na tuangalie jinsi yalivyoweza kujitokeza baadhi ya mifano iliyomo ndani ya Tamthiliya hii ya *Fumo Liongo*:

> *MKE: "Usifikiiri ni rahisi kiumbe kutembea kwa miguu miwili iendayo uchiuchi! We shukuru unayo mitatu ". (UK:1)*

Kutokana na mfano huu tunapata picha ya watu wawili wanaotembea pamoja na mmoja anatembea akiwa hana viatu na njia ilikuwa ina vichaka vinavyoumiza miguu na muhusika mwengine anatembea kwa miguu miwili na gongo la kumsaidia kuzivuta hatua za mwendo wakati wa safari hadi kuanza kuvutana baina yao ili kuweza kufika wanakotaka kwenda. Dhamira ya Umasikini uliopo kwa wanakijiji cha Pate na kutomudu hata kiatu cha kuvaa wakiwa katika harakati za kushajihishana. kwa kuipa nafasi hadhira na kuzivuta hisia za msomaji kivitendo katika kuitafakari hali ya mwendo na uhusika wa wahusika wake inavyojitokeza sambamba na tukio husika kwa ustadi wa maneno teule yanayoiakisi hali hiyo, Mfano huu unakwenda sambamba na msimbo wa kimatukio (matukio) kutokana na jinsi matukio yanvyoungana kutokana na kusababishana au kuathiriana katika tamthiliya hii kutokana na nadhariya ya simiotiki.

> *MACHAKA: Tusipompata kwa mtego wa nyongo ya mamba katika kinywa chake, basi tutambaka kwa nguvu za minyororo ya Ufalme (UK:11).*

Kupitia kauli hizi za muhusika wa uongozi wa Mfalme Mringwari kwa Machaka tunapata Taswira (Picha) ambayo inaonesha jinisi mtego wa nyongo ya mamba kuwa ni kifaa au kitu kinachotoa sumu na kuingizwa katika kinywaji (kileo) kilichokususdiwa kumuuwa Liongo, na vile vile tunapata picha nyengine kwamba Mfalme wa Pate anaashiria kutumia nguvu zake kumkamata Liongo hata kwa kutumia minyororo na kumfunga kwa kumfanya anavyotaka. Dhamira ya kuonesha

Unyanyaswaji wa raia ndani ya nchi ya nchi yao kama ilivyopangwa kumtendea Liongo imedhihirisha kitendo cha wahusika kwa kuikamilisha nia waliyonayo juu ya muhusika msemaji na msemwaji kwa lengo la kumfanya muhakiki kuijenga hisia kwa kuiona hali halisi na tukio akilini mwake. Mfano huu unaenda sambamba na nadhariya ya simiotiki kupitia msimbo wa kiseme ambao unatokana na elementi zinazopelekea kupata picha fulani kutokana na viashiria fulani, kuelewa sifa kamili ya jambo, tukio na hali zinazojitokeza katika tamthiliya.

> MBWASHO: *Mazabania walionekana wakimburuta Msheki huku kafungwa Kaniki usoni. Walipofika Pwani walimtwanga mtalimbo wa utosini na kutoasa baharini (UK:15).*

Hapa tunapata taswira ya kuburutwa kwa msheki, kufungwa kaniki usoni, maeneo ya pwani na kutwangwa mtalimbo wa utosini na kitendo cha kumtosa baharini, hali zote hizi zinatoa taswira ambayo kwa wale wanaosimuliwa kujenga picha kimawazo na kukiona kile kitendo kilichokuwa kinatokea wakati wa tukio husika. Dhamira inayohusiana na tukio hili ni ile ya Uongozi mbaya, kwa kuujenga uhalisia wa wahusika, tukio, na matendo pindi tu mwanafasihi atakapojikita katika kuifanyia kazi tamthiliya hii ya Fumo Liongo, sambamba na msimbo wa kimatukio unaoendana na matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na kusababishana katika tamthiliya.

Pia tunapata lugha ya picha ambayo imejitokeza katika kurasa ya kaditama hii ni kurasa iliyokusanya majonzi/ masikitiko, maswali mbali mbali ambayo muuhusika MACHAKA huwa anajiuliza kwa lengo la kuiangalia khatima ya maisha yao na jinsi watakavyoweza kuendelea kuishi hapa tunapata Taswira kama zifuatazo:-

> *MACHAKA: "Liongo kule mbali, kuleee!*
> *Naona msururu wa watu weusi watumwa*
> *Wako uchi wa nyama: wake, waume na vigoli*
> *haijambo wameleta korwani na ibada Lakini hili je?*
> *La kutunadi kama mbuzi?*

*La kuchambua ngozi kwa bakora na herizani?*
*La kutuchunguza kwa shanga, kaniki na korofindo?" (UK : 50 )*

Kutokana na matamshi hayo yanayotokana na Machaka yanaonesha wazi jinsi yalivyosheheni Taswira mbali mbali ambazo zinaonesha jinsi wahusika walivyokuwa na maoni yanayojenga picha ambazo zinauzingatia zaidi muonekano unaofuatia baada ya harakati za kujitafutia uhuru na jinsi hali halisi ilivyokuwa inajtokeza baadae, picha iliyojitokeza inatokana na ule utumizi wa lugha ya picha ikiwemo ile ya "Msururu wa watu weusi- watumwa, wako uchi wa mnyama, wake, waume na vigoli, kutunadi kama mbuzi, kutuchambua ngozi kwa bakara na henzirani, kutuchuuza kwa shanga, kaniki na korofindo."

Dhamira iliyojengeka hapa nai ile ya kuonesha Utabaka unaoonekanwa baada ya mapambano kati ya watawala na watwaliwa katika makucha ya utawala wa kiongozi wa Pate ambae alikuwa anatumia mabavu zaidi, lakini katika maelezo yanayofuatia tunaona kuwa kuna mabadiliko ya kiutawala. Pia kulikuwa na lengo la kuivutia hadhira kwa kuijenga picha ya historia ya utawala wa nyuma nchini Afrika hasa maeneo ya Afrika Mashariki kwa kujionea wenyewe kififikra na kuijenga jamii inyosomwa ndani ya tamthilyia hii makilini na machoni mwa msomaji wa kazi hii ya fasihi.Sanjari na nadhariya ya simiotiki tunaupata msimbo wa kihementiki unaohusu taharuki na unajulikana kama msimbo wa kusimulia au kutamba hadithi anayoisimulia Machaka baada ya mapambano na kubaki na upweke kwa kupoteza ndugu na jamaa walioshiriki vita na kile kinchofuatia baada ya mapambano.

### 4.3.2 Matumizi ya Semi/Misemo

Kwa mujibu wa K.W. Wamitila (2008), anaeleza kwamba tamathali za usemi

huchukua nafasi muhimu katika uchanganuzi wa mtindo katika matini au kazi za fasihi.Lugha ya msemo/ semi ni tungo au kauli fuza kisanaa zenye kubeba maana au mambo muhimu ya kijamii, kumbo hili linatanzu za methali, vitendawili, mafumbo, misimu, lakabu na kauli tauriya.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), semi/ misemo ni tungo fupifupi za kisanaa ambazo huwa zimebeba maana fulani kulingana na muktadha uliotumika kisanaa ndani ya kazi ya fasihi, misemo hiyo hutoa ujumbe mfupi ambao unatoa maana pana zaidi endapo utaangaliwa kiundani zaidi hadi kufikia kuipata maana na lengo lake. Katika Tamthiliya ya Muandishi Emmanuel Mbogo ya “Fumo Liongo” kuna misemo mbali mbali iliyojitokeza kama ifuatavyo:-

> *MKE: Basi nenda, we nenda tu, “Watakuja watu wengine waniokote miye nisiyeshina (UK: 2)*

msemo huu unatoa maana ya kwamba Mke kakosa msaada kwa mwenziwe (mume) huenda akaupata msaada anaohitaji kupitia kwa wengine kwani yeye amekosa msaada ambao utampa nguvu ili aende sambamba na Mumewe safarini na vile vile inatoa maana ya kutokata tamaa endapo hutopata msaada wa mtu mmoja huenda ukapata msaada kwa watu wengine. Dhamira inayojengeka hapa ni ya kuwa na Ushirikiano kwa wanandoa na wanajamii ya wapate ili kuyajenga mazingira yaliyokusudiwa yawe timilifu wa wapate wenyewe na matukio yao yalivyoiakisi jamii hiyo huzivuta hisia za msomaji na hata msimuliwaji ya tamthilia hii kwa kuvikamilisha vipengele vya kazi hii kwa ubunifu wa hali ya juu sambamba na hili linadhihisha kuwa linaendana na nadhariya ya simiotiki kutokana na msimbo wa

kiseme ambao uanampa na nafasi msomaji kuweza kuelewa kunachokusudiwa kutokana na hali iliyojitokeza.

*WEMA: …Ukimnasa kwa Ulimbo atajinasua kwa fimbo tu. (UK: 4).*

Msemo huu unaashiria kitu kinachotakwa kuingizwa katika mtego na kupatikanwa kwa lengo la kupatiwa adhabu au hukumu kikiwa na mbinu au ujanja wowote ule yaani kwa lengo la kujinasuwa au kujiokoa kutokana na mtegoi aliotekwa au aliotegewa.

Vile vile tunapata dhima nyengine ambayo ina ubainifu wa usanii wa msanii wa kazi hii ya fasihi kwa kwenda sambamba na utumizi wa maneno teule ya msanii na kuwabebesha wahusika wake katika uhusika wao na kuzifanyia kazi kulingana na tukio, tukio hili linakwenda sambamba na matumizi ya lugha na ishara inayotokana na nadhaiya ya simiotiki katika msimbo wa kiseme ambao unampa nafasi msomaji kuipata maana ya kitu au hali kutokana na hali ilivyojitokeza.

*MRIGWARI: Dunia na maisha ya binaadamu yako katika mwendo wa kupituka ( UK:5).*

Msemo huu uliotokana na kauli ya Muhuska MRIGWARI una maana ya kwamba dunia na maisha ya binaadamu yanakwenda kwa kuja na kuondoka na sio maiasha ya kudumu kwani mwanaadamu huyu ameletwa katika dunia hii kwa muda na ataondoka kwa muda aliopangiwa, Hapa tunapata dhamira ya uelimishaji wa jamii kiufundi kulingana na kupatikanwa kwa uongozi usojali hisia za wengine na kutaka kutwala kwa mabavu, kupitia busara za msanii tunaweza kusema kuwa hapa tumepata ya ushajihishaji unaozingatia ukweli na khatima ya mwanaadamu popote alipo. Usemi wa aina hii unkwenda sambamba na msimbo wa kiishara ambao

unatokana na nadhariya ya simiotiki ambao unahusisha msomaji na jinsi anavyovumbua maana kiishara kama ilivyoashiriwa kutokana na matamshi ya muhusika .

*Msheki: Ili liweze kumea, hata shina hutegemea majani yake (UK:6).*

Maana ya msemo huu ni kwamba kitu chochote unapotaka kuotesha/ kupandwa au kuenziwa kitu hicho au jambo hilo linategemea na ile asili yake katika ukuaji wake au kuimarika kwake, umuhimu wa kuimarisha jambo unategemnea na uimara na ubora wa sehemu inayokusudiwa kuwekwa au kupandwa kwa mmea huo. Dhamira inayojengwa hapa ni ile ya kutanabahisha jamii kuwa makini zaidi katika kulikabili jambo lolote lile ni kulijulia chanzo chake na makuzi yake, msemo huu nao pia unaingia katika msimbo wa kiishara unaotokana na nadhariya ya simiotiki katika kipengele cha ishara ambayo hutoa maana Fulani kwa msomaji kutokana na msomaji anavyovumbua maana kiishara .

*LIONGO: Lakini tukumbuke kuwa Mbuzi akinguruma jua ameota meno, na samba akilia mee! Kumbe anang'oka meno (UK:10).*

Msemo huu unatoa maana pana kwamba mbuzi akinguruma/ akitoa mlio wa mngurumo kuwa tayari amekamilisha makuzi yake na anakuwa anauwezo wa kujikamilishia mahitaji yake katika kujipatia riziki zake, vile vile pale ambapo Simba anatoa sauti ya mlio wa mee! Hii inaashiria kuwa anapungukiwa na viungo muhumu chenywe viungo kama hivi ambavyo huashiria dhana au hali inayoweza kutanabahisha utendaji/ uwezo wa mtu/ watu, tunaweza kusema msemo huu unaigusa jamii ya Wapate kwa Liongo ambapo wakitaka kuwa na nguvu moja kwa lengo la kujikomboa na kuung'oa utawala uliokuwepo kwa kunguruma, kutoa sauti pale ambapo watakuwa wanaumizwa na watawala.

Dhimira ya usemi huu imejengwa na mapambano ya wahusika wakati wa kutafuta haki yao ameyatumia kwa mfumo wa maneno teule yatakayopunguza makali ya uchungu waliokua nao wahusika na kujadili matatizo yao kiungwana zaidi. Hali hii inasaidia katika kupunguza ukali wa maneno kwa wahusika na kuendeleza ushujaa wao.usemi huu unaendana na nadhariya ya simiotiki katika msimbo wa kiseme kwa kuashiria hali zinazojitokeza na kumpa nafasi msomaji kutokana vielezea vinvyoelezea sifa kamili ya hali zinavyojitokeza katika jamii.

> *MBWASHO: Ninyi vijana shujaa. Masimba lakini mawazo yenu bado machanga (UK:14).*

Msemo huu unaamaanisha kwamba vijana shujaa waliokususdiwa haapa wenye nguvu na uwezo wa kuenda mambo lakin mawazo ya ni mafupi na hayafikii malengo yanapelekea kuishia kushindwa na kuingia mashakani. Dhamira ya usemi huu ni kuelimisha vijana kwa kuiashiria jamii ya watu wa pate kutojisahau na kuingia katika mchakato kwa uwazi kabisa pasi na kificho. Hali iliyopelekea kutumika kwa lugha nyepesi inayofahamika.

> *LIONGO: "Itakuwaje? Shamba nilime mimi, mbegu nipande mimi, mavuno avune Mrigwari, e? (UK: 18)*

Msemo huu nao pia unaamaanisha kuwa kitendo anachokifanya Liongo katika kupanda mbegu katika shamba alilolima yeye na kuingiwa na watu wengine kwa kuvuna kile alichokipanda shambani, hali hii inadhihisrisha kuwa kuna waliokuwa wanataka kutumia mabavu katika kuchukua na kutumia mabavu katika kuchukua na kutumia vya watu pasi na kutumia nguvu zao kwa kuwadhulumu wenzao ndani ya maeneo yao. Dhamira iliyotumika hapa ni ya unyanyaswaji kwa raia wa Pate chini ya utawala wa Mfalme Mrigwari hali hii itawasaidia wanafasihi kuweza kuutafakari

utawala huo. Sambamba na hili ni kwamba inaendana na nadhariya ya simiotiki kupitia msimbo wa kiseme unaelezea tukio na jinsi inavyoashiria hali inavyojitokeza katika jamii.

> *LIONGO:Kobe hushindwa na gamba lisilo lake, na hili nililonalo si gamba langu, lina mwenyewe. (UK:21).*

Msemo huu una maana ya kwamba Kobe huendana na maumbile yake alivyo na sio yale ya kuanzimwa au kupewa, kwa hivyo Kobe huyu akipewa gamba lisilo la kwake huwa haliwezi, kwa hivyo hilo alilokuwa nalo si gamba lake halitafika pahala pegine ila lende kwa mwenyewe ili kuondowa mzigo usiokuwa wake na hali kama hii haitalifikisha jambo au kitu mahali isipokuwa kwa jambo linaloendana nalo. Dhamira inayo aliyetamka matamshi hayo ni kutokana na usemi huu ni ya kuitanabahisha jamii juu ya uhalisia wa kinachowasilishwa na muhusika kukuza utendaji na uhusika wa mtendaji kwa yanayoweza kuepukika kwa jamii husika, ni mfano mzuri unaoendana na nadhariya ya Simiotiki katika msimbo wa kiishara ambao unavumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

> *WAZIRI KIONGOZI… sisi tuliokula chumvi nyingi tumeona mengi (UK: 35).*

Hii inasadifu kauli za watu wazima waliotangulia maishani kuwa wameishi kwa muda mrefu na kuyaona mambo mengi yaliyotokea tangu enzi za utoto, ujana na utu uzima wao nao huwa wana mambo mengi ya kujifunzia kwa kuonya, kuelekeza au hata kutahadharisha jamii, mtu au watu pale panapostahili kufanywa hivyo. Damira inayojitokeza hapa ni ya kuikuza lugha kwa kuingiza misamiati yanayoikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili kisanaa. Pia tunapata msimbo wa kiseme unaotokana

na vielezea vinavyoelezea sifa kamili ya hali zinazojitokeza katika jamii kama yalivyotumiwa na muhusika aliyetajwa hapo juu.

> *Waziri Kiongozi: Naambiwa na Wazee mtukufu kuwa kitovu kibichi cha mtoto mchanga sharti kiangaliwe kisikatike na kudondokea pahala pasipostahiki kudondokea. (UK:40).*

Usemi huu unaendana na matamshi ya wazee kwa kuwapatia wazazi ili wajuwe jinsi ya kuwa waangalifu zaidi katika masuala ya ulezi wa watoto tokea kuzaliwa kwao kuenziwa na kuhifadhiwa kitovu cha mtoto mchanga kuanzia pale pahala kitakapodondokea na pale kitakapohifadhiwa baada ya kwisha kuanguka, kitovu hichi huangaliwa kwa uangalifu zaidi kitovuni na pale kinapoangukia/ kufikia. Dhamira ya utumizi wa msemo huu ni kudumisha mila na desturi za jamii husika kwani zina faida, hekima na busara zinazolinda na khifadhi utu wa mtu, pia tunaupata msimbo wa kiurejelezi ambao unatokana na viashiria vya kiutamaduni katika kazi inayowasilishwa na imejengwa na hekima na busara za kukuza utanabahisho na uangalifu kwa wahusika na wanafasihi ili kuzivuta fikra na kuwa na utayari wa kujenga jambo na kulitekeleza jambo. Hivyo umakini ndo silaha ya mafanikio.

> *LIONGO: … lakini giza halipaswi kuwa suke na upupu? Bali shuka ya manyoya laini ya kuwakumbatia binaadamu machovu ya kazi za siku nzima. (UK: 41).*

Msemo tunaoupata hapa ni ule wa kuonesha hali halisi mzunguko wa maisha ya wanaadamu na nyakati zinavyokwenda, hii inaamaanisha kwamba giza linapoingia liwe lenye kutoa nafasi kwa atakaepumzika na lisiwe linampatia dhiki na kumtia mashaka kwa usiku wa kucha, hivyo giza hilo linapaswa kuwa ni shuka ya manyoya laini ya kuwakumbatia wanaadamu katika machovu ya kazi za usiku nzima. Dhamira inayojitokeza hapa ni ile ya kutanabahisha jamii juu ya maisha yanavyokwenda

yanahitaji uelewa wa mtendaji na faraja ya mwanadamu nayo pia ina imuhimu wake. Kwa mujibu wa nadhariya inayohusishwa na kazi hii tunapata msimbo wakiseme ambao tunapata viashiria vya kuelewesha sifa kamili za jambo au tukio lilopo.

### 4.3.3 Matumizi ya Tamathali za Semi

Rashid (1992) ameeleza kwambaTamathali za semi ni sentesi fupi fupi ambazo hutumiwa na muandishi au wazungumzaji katika kuipamba kazi ya fasihi n kuiongezea utamu ili iwe na ladha. Tamathali za semi hufanikisha au kuwakilisha dhana Fulani kwa dhana nyengine zilizo tofauti au zilizofanana, kazi ya tamathali za semi ni kuifanya kazi ya fasihi iwe na uzuri wa aina yake , ivutie na ipendeze pia itowe ujumbe unaotakiwa (mwafaka) baadhi ya tamathalia za semi ni : tashbiha, sitiari. Tash-hisi, tauria (tafsida), ishara (taashira) na kutia chumvi (mubalagha).

#### 4.3.3.1 Tashhisi

Kwa mujibu wa Hamad na wenzake (1983) wameeleza kuwa. TASH-HISI ni aina ya Tamathali inavyotumia mbinu ya kuvipa uhai na uwezo wa kibinaadamu vitu ambavyo havina uhai wala si binaadamu kama vile “Mvua iliyonyesha Jana imeitafuna na kuimeza Ardhi ile yote “mfano huu unaonesha jnisi kitu kisichokuwa na uhai (mvua) kuweza kupa sifa ya Kiumbe chenye uhai katika kutumia neno “kutafuna” na “kuimeza Ardhi yote”

Katika Tamthiliya ya FumoLiongo, muandishi Emmanuel Mbogo amezitumia baadhi ya tash-hisi ambazo zimejotokeza katika (UK: 49) sehemu inayozungumzia kaditama

ya Tamthiliya hii iliyosheheni mazungumzo ya muhusika Machaka baada ya kwisha kufanya mapinduzi, Tash-hisi hizo zilijitokeza kama ifuatavyo:-

*Machaka: "Dongo limelala, limekumbatia vumbi, makaburi tayari yamepanua vinywa vyao" (UK:49):*

Tash- hisi iliyotumika hapa imejikita katika sifa ile ile ambayo kitu kisicho uhai kimechukua sifa ya kutenda kama kiumbe hai, kwani "Dongo" (kitu) amabacho kimepewa nafasi ya kitendo cha kulala na kupewa sifa nyengine zaidi ya kulikumbatia vumbi kama kiumbe hai, ilhali si kiumbe hai. Dhamira iliyojengwa hapa ni ile ya kuonesha khatima ya mwanaadamu, Tamthiliya hii imeweza kuonesha jinsi gani lugha katika matumizi yake huwa na utajiri mkubwa wa kuingiza viungo vyenye mvuto na mnato wa sifa za viumbe hai, ukuwaji na uimarishaji wake unaongezeka zaidi pale yanapotumika misamiati tofauti yenye ujumbe kwa hadhira, ujumbe huo unadhihirisha ukuwaji wa misamiati katika utumizi wa lugha ya Kiswahili. mfano huu unaenda sambamba na nadhariya ya simiotiki katika msimbo wa kiishara na jinsi yanavyotafsiriwa na msomaji wa kazi ya fasihi.

*Machaka: Hekima iliyotuunganisha sasa imeyayuka (UK: 49).*

Mfano uliopo hapo ambao unaonesha matumizi mbali mbali ya lugha ikiwemo hii ya Tash-hisi iliyojitokeza kupitia muhusika wake "Machaka" ndani ya *Fumo Liongo* msemo huu unamaanisha kwamba kuna haja ya kuimarisha uhusiano kwa hekima na sio kuubadilisha na kbadilisha muwlekeo, ikiwemo ile ya kuonesha jinsi hekima ilivyopewa nafasi ya kitu kinachokuwa na uwezo wa kuwepo na kuondoka kama viumbe vyengine vinavyoweza kutenda au kuwa na sifa ya uwepo wake na kuondoka kwake. Dhamira inayopatikanwa hapa ni ile ya kuielimisha jamii na kukuza lugha kwa kutumia misemo itumikayo ndani ya lugha ya Kiswahili kwani hali hii ndiyo

inayoboresha na kukuza kazi ya fasihi na kuipamba kwa ubunifu wa hali ya juu. Mfano huu unaingia katika msimbo wa kiishara ambao unaasshiria tendo ilililotokea na kuondowa hekima inayolengwa.

#### 4.3.3.2 Kejeli

Kwa mujibu wa Muhammed (1981) kejeli ni aina ya tamathali inayotumia maneno kinyume na yalivyo. Kejeli ni aina ya usemi unaotumiwa na wanafasihi katika kuipamba lugha kifasihi kwa kukipa sifa kitu kinyume na kilivyo kitu hicho au kumpa sifa mtu kinyume na alivyo kwa lengo la kumkejeli. Mifano kama hii imejitokeza katika tamthiliya ya Fumo Liongo ifuatavyo:

Katika UK: 22 – 23 kupitia muhusika MRIGWARI alipokuwa anazungumza na muhusika LIONGO kuwa:

> *MRIGWARI:"( Akihema kwa woga ) Nimekupata? Sikukupata? Kima we! (Anatema mate) Phuuu! Unajifanya una siri, siri gani uliyo nayo mshenzi mkubwa we! Hata jabali humegeka likaliwa na mvua, upepo na tufani, likafa. Hata nyota huseleleka na kuzama upande wa pili wa giza la anga. Ila mshenzi, anzali mmoja aitwa Liongo! Nilijuwa siku moja nitalikaba kabare na kuling'oa mashurubu na mapenzi yake ya ukaidi, nilirudishe majini nione kama litaibuka na kupiga mbizi tena kama zamani. Sema!''*

Kejeli iliyotumika hapa inaonesha jinsi muhusika anaezungumza MRIGWARI ni kiongozi wa mabavu asijali hali za wanaojitetea katika kutafuta haki yao hivyo anatumia maneno ya kejeli na kumkashifu muhusika LIONGO ili aweze kukamilisha matakwa yake bila ya kujali uzito wa maneno anayoyatumia kumwambia muhusika huyo. Dhamira iliyojengwa hapa ni ile ya kuonesha ukatili na dharau ambazo zinatokana na uongozi wa juu dhidi ya watawaliwa kutokana na mfumo wa

kimabavu unaoendeshwa kupitia utawala uliokuwepo. Kutokana na mfulululizo huu unaoelezea matukio na kupatikanwa kwa sifa kamili ya ya tukio hali hii inaingia katika msimbo wa kiseme ambao ndio zao la nadhariya ya Simiotiki katika msimbo wa kihementiki.

#### 4.3.3.3 Taharuki

Senkoro (1996) ameeleza kwamba taharuki katika fasihi hutumika mbinu ya taharuki ili kuvuta usikivu wa hadhira, hii huifanya hadhira kujiuliza mara kwa mara kuhusu matukio yatakayofuatia kuwa yatkuwa yan namna gani. Hii ni miongoni mwa hali ambayo muhusika Fulani au wahusika Fulani katika kazi ya fasihi huwa wameingiwa na hamasa ya kitu/ hali ambayo inawashajihisha kukifuatilia na kukifanyia kazi kitu hicho kwa hamasa, kwa upande mwengine Taharuki inaweza kuwa hali ya kuwa na khofu/wasiwasi/ jazba/kuchanagnyikiwa/ kutozwa nguvu/kutohimili jambo au hali iliyotokea, kutamka matamshi yanayokwenda sambamba na hali halisi wakati wa uwasilishaji.

Katika Tamthiliya ya muandishi Emmanuel Mbogo ndani ya kitabu chake cha Fumo Liongo ameelezea kwa ufanisi wa hali ya juu katika matukio tofauti yaliyojitokeza, kwa mfano:

> *WATU: ‘’* Motoooo!!! Uwa Mrigwari, Uwa!’’
> *MACHAKA;* ‘’Motoooo!!! Uwa Mrigwari, Uwa! *(Radi na ngurumo...Mvua inaanza kunyesha.... Watu wanaondokambio huku wakilia. Moto! Moto! Moto! Motooo!Sekunde zinapita. Wanawake na Wanaume kadhaa wanabeba maiti Ya Fumo Liongo, wanatoka Mbwasho akifuata nyuma. Sambamba Wimbo wa maombolezo unasikika ukiimbwa taratibu. Polepole Mwanga unafifia (uk.48).*

Taharuki iliyojitokeza hapa ni ile inayolenga kuhamasisha wana wa Pate katika

kupambana na adui wa kiongozi wao na wafuasi wa Liongo katika kutaka kujikomboa hali ambayo ilijenga taharuki baada ya kumuona Liongo amepoteza maisha kwa mbinu za wale wasiowatakia mema wana wa Pate na jamii zao kwa Ujumla. Dhamira iliyojengwa hapa nai ya umoja na mshikamano kwa wana wa Pate kuungana pamoja kumuuwa adui wa maisha ya watu wa Pate kutokana na tukio lililowasilishwa. Sambamba na hili tunapata msimbo wa kihementiki ambao unakwenda na taharuki ambao unajulikana kama mimbo wa kutamaba hadithi.

#### 4.3.3.4 Tanakali Sauti

Senkoro (1996) ameeleza kuwa maneno ya ki-tanakali sauti ni yale ambayo yanaigiza sauti ya kitu Fulani au tendo Fulani. Haya yameenea sana katika tanzu mbali mbali za fasihi simulizi, nayo yanasaidia sana kuyafanya yale anayoyaeleza mtambaji yaeleweke kwa hadhira yake, vile vile yanasaidia sana kukamilisha hisi za hadhira kwani mara nyingi hushughulikia milango yote mitano ya fahamu za mtu: ya kunusa, kusikia, kuona, kuhisi, na kuonja. Tanakali sauti zilizojitokeza ni kama hizi zifuatazo:

(uk:45) M’MKE 3 *:* “ Uuuuuuuuuwi*!’’*
RAIA: “Uuuuuuuuuwi!*’’*
M’ MKE *1&*
M’MKE 3 :” Uuuuuuuuuwi!’’
(UK : 15 ) *LIONGO*: Aaaa...!
( UK : 19 ) *MACHAKA* : ‘’Meeee!’’
(UK ; 20) *BITE : ‘*’Heee!’’
MACHAKA *:’’* Heee!’’
( UK : 24 *) MLINZI 2* “ Phuu!’’
(UK : 32 ) *MACHAKA : ‘*’ Aaaa!’’

(UK ; 42 ) ZAHIDI : ‘’Oo!’

Mifano yote iliyotajwa hapo juu ni miongoni mwa Tanakali sauti zilizojitokeza katika Tamthiliya ya Fumo Liongo ambayo imetuumika katika kukuza na kuendeleza matumizi ya vionjo vya lugha vyenye kukuza mnato na mvuto wa kazi za fasihi pamoja na kuzivuta hisia za msomaji. Dhamira iliyojengwa hapa ni ile ya ukuzaji wa lugha kwa vionjo vya lugha kisanaa.Pia tunapata msimbo wa kiishara ambapo msomaji huvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

#### 4.3.3.5 Takriri

Senkoro (1996) ameeleza kwamba kuna nia tofauti katika matumizi ya mbinu ya kurudirudia kauli au neon Fulani yanyofanywa an watmbaji. Ni miongoni mwa matumizi ya maneno au neno lenye kujirejea rejea katika kazi za fasihi, ndani ya tamthiliya ya fumo Liongo kuna takriri nyingi zilizojitokeza kama ifuatavyo:

(UK : 11 ) MACHAKA : ‘’ *Mhm! Mhm! Mhm!’’*
(UK : 16 ) LIONGO : *‘’ Aa! Aa!’’*
(UK : 26 ) LIONGO :’’ *Mama! Mama!’’*

Mifano hii ni miongoni mwa tanakali sauti ambazo zimejitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* katika hatuwa za ubunifu na umahiri wa muandnishi zenye dhima ya kutomea vionjo vya lugha kama ilivyojitokeza hapo juu, kupitia nadhariya ya simiotiki hali hii nayo inaingia katika msimbo wa kiishara ambao unamfanya msomaji aweze kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

#### 4.3.3.6 Mdokezo

Ni miongoni mwa matumizi ya lugha yanayojitokeza katika mawasiliano yenye kuacha baadhi ya maneno huwa hayajalizwi na kuachwa alama ya desh desh (...) wakati wa mazungumzo baina ya wahusika. Katika tamthiliya ya Fumo Liongo kuna mifano tofauti ambayo imejitokeza katika hali ya mdokezo ikiwemo kama hii ifuatayo;

*(UK : 25 ) SADA: '' Bwana....!''*
*Hujambo....? ( Akilia kwa kwikwi... anayakaguwa majeraha.) Pole Bwana wangu!'' '' Oh! Dunia hii....''*
*(UK: 27} LIONGO: ''Mama...! Mama! ...*
*(UK: 30) MACHAKA: ''Mimi Bwana...*
*W. KIONGOZI: Je....Tuseme kuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika?''*
*''Ee... kama kuondoa baadhi ya makombe ya tembo pale mezani?''*
*'' :'' Basi lazima Yule Liongo si mtu bali ni jinni......''*
*(UK: 40) W. KIONGZI: '' Sindano... ya .... shabaa....sha-a-baa!''*
*(UK : 41 ) LIONGO: '' Bali shuka ya manyoya laini ya kuwakumbatia binadamu wenye*
*Machovu ya kazi za siku nzima.... Nitarudi,''*
*(UK: 42 ) ZAHIDI: ''Baba... (kimya anatoka sindano...jogoo anawika tena... kisha tena ...kisha tena sauti za mbweha na fisi. Zahidi anamnyemelea na kumchoma Liongo sindano ya kitovu na kukimbia... sauti za radi...kunapita muda mfupi...kisha Liongo* anainuka,''

Mifano yote hiyo inaonesha jinsi mdokezo ulivyojitokeza katika tamthiliya hii ya *Fumo Liongo* kama ilivyojitokeza hapo juu kupitia wahusika wake. Dhamira iliyotumika hapa ni ile ya kukipa nafasi Kiswahili kuwa na maneno yenye kuhitaji mjazo Fulani ambao unahitaji kuuvuta umakini wa msomaji kwa kuwa muangalifu zaidi kwa kuukuza uelewa juu ya kile anachokisoma. Vile vile mifano hii inaingia katka msimbo wa kimatukio ambao unatokana na nadhariya ya simiotiki ambapo inaonesha jinsi matukio yanavyoungana na kushonana au kuathiriana katika tamthiliya hii.

Kwa ujumla Tamthiliya hii ya *Fumo Liongo* ndani ya igizo zima tunaona kwamba muandishi Emmanuel Mbogo" amefanikiwa kuweza kutumia matumizi mbali mbali ya lugha ambayo yamechukua nafasi ya kuimarisha na kuendeleza lugha ya

Kiswahili kwa kuingiza viunjo mbali mbali vya lugha ikiwemo lugha ya mshangao, lugha ya picha, misemo na semi mbali mbali ikiwemo lugha ya kejeli, lugha ya Mdokezo, Tanakali sauti, Taharuki, ushauri, Tash-hisi na lugha ya msisitizo. Utumzi wa vionjo vyote hivyo umeshtadi utamu/ ladha/ haiba/ ubora/ ubunifu/ umahiri na thamani iliyo na hazina muhimu katika kazi za fasihi. Mifano yote hiyo imejitokeza katika kitabu cha “Fumo Liongo” kama yalivyojieleza huko nyuma kwa kila kurasa ambayo ilikuwa na matumzi ya lugha pamoja na dhima zake kupitia muandishi Emmanuel mbogo."

Mwanafasihi huyu kindakindaki ambae ameshtadi uzalendo na upendo kwa wanafasihi wa kitanzania na watanzania wote kwa ujumla tutamuangalia zaida katika tamthiliya yake nyengine jinsi alivyojikita katika matumizi ya lugha kupitia tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello.*

## 4.4 Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya ya John Okello

Katika tamthiliya ya “Sadaka ya John okelo” ambayo pia mwandishi wake ni Emmanuel mbogo, ni miongoni mwa kitabu ambacho ndani yake kuna matumizi mbali mbali ya lugha yaliyotumika kupitia wahusika wake tofauti kupitia mazingira ya jamii yetu ya Zanzibar katika kipindi cha kutafuta uhuru wa nchi yao kwa kufanya mapinduzi yenye lengo la kumg’oa Sultan Jamshid usikuu wa kuamkia tarehe 12 Januari 1964.

Tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello* imesheheni matumizi ya lugha ambayo yamezungukwa na lugha ya na lugha ya uhamasishaji kuanzia ukurasa wa 1 hadi

ukurasa wa 45 miongoni mwa matumizi ya lugha yaliojitokeza katika tamthilia hii ni misemo, methali, lugha ya picha, lugha ya ishara, lugha ya kejeli, lugha ya kishairi, mafumbo, mdokezo, tanakali sauti, tash-hisi, matumizi ya lugha mchanganyiko, Tashbiha na Takriri.

### 4.4.1 Matumizi ya Misemo

Wamitila (2008) ameeleza kwamba “lugha ya kitamathali huwa na majukumu matatu makuu (a) urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kumbuji, (b) ufafanuzi au uelezeaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum na uthabitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti Fulani.Matumizi ya lugha hiyo hapo juu yanayojitokeza kupitia tamthiliya hii ya “Sadaka ya John Okelbo” tamthilia hii tumeweza kuipata katika kurasa tofauti, kwa mfano:

*GAVANA: Zanzibar imenawiri na kuimarika kwa shibe ya maziwa ya matiti ya mtukufu Malkia Elizabeth (UK.01).*

Katika msemo huu muandishi alikusudia kubainisha kisiwa cha Zanzibar na kuendelea kwake kumetokana na nguvu za Malkia Elizabeth, dhamira iliyolengwa hapa ni ya ubinishaji wa hali kwa kuonesha kwamba mtu anapoona kitu kimeimarika au kimekua kizuri ajue kuwa kuna nguvu au kazi iliyofanyika ili kukifanya kiwe kama hivyo kilivyo. katika mfano huu unakwenda sambamba na nadhariya ya simiotiki inayotokana na msimbo wa kiseme ambapo tunapata picha fulani kutokana na vaishiria vilivyozungumzwa na muhusika katika tamthiliya hii.

*JAMSHID: Zanzibar ni Pweza mwenye miguu na mikono lukuki* (UK:4).

Msemo huu nao umechukua nafasi ya kisiwa kilichokamilika katika kujimarisha kwa

kupiga hatua kwa kujituma na kuyaendea yao kwa miguu yao kwa kuyafanyia kazi kwa mikono yao, huu ni msukumo unaoangalia zaidi mabadiliko huenda yakarudi na kubadilisha kisiwa. Dhamira yake hasa ni ukombozi wa kiisiwa na kuwa ni sehemu ya kiunganishi cha mawasiliano kinavyoweza kutumika kuwaunganisha watu, na pia kimetumika katika lugha kwa ustadi usiobadilisha maana ili kuendeleza upekee wa muandishi katika ustadi wake.

> *JAMSHID: ... Fungate kati ya tawi la mlimao chunga na shina la mchungwa asili imegeuza Chungu ya limau kuwa tamu ya chungwa? (UK:4).*

Msemo huu umechukua lengo la ufafanuzi juu ya eneo la Zanzibar na vilivyomo vilitowa nafasi nzuri kwa mtawala na kumnogea, na pale ukweli ulipodhihiri sultan Jamshid mambo yalivyomgeukia na akaanza kupoteza matumaini kwa kuanza kumtumbukia nyongo na kupoteza haiba yake. Dhamira ya msemo huu ni kuonesha utawala wa kigeni ulivyokuwa visiwani Zanzibar na hali ya maisha kupitia mazingira yaliyompa nafasi mtawala (Sultan) kuweza kuwatawala na pale walipozinduka watawaliwa.usemi huu unaendana na msimbo wa kiishara ambapo tunaweza kuvumbua maana ya kiishara inayotokana na hali halisi ilivyotokea.

> *BABU: Mimi mnauliza Mioyo ya walala hoi itaendelea kuvunja damu hadi lini?, jasho la Walala puu, litaendela kuwa samadi ya bustani za ma mwimyi jana, leo na miaka alfulelaule? (UK: 5).*

Katika mfano huu muandishi amesheheneza misemo inayolenga hali za watu wa chini / duni jinsi wanavyoumia na kudhalilika, kutoka katika utawala wa sultani, pia faida zinazopatikanwa zinaishia upande wa utawala katika kipindi chote cha utawala kwa raia wa visiwani. Dhamira inayopatikanwa hapa ni ya ukombozi wa raia wa visiwani chini ya utawala wa kigeni kwa kufikisha ujumbe ndani ya jamii, katika

kipengele cha matumizi ya lugha kwa kutumia maneno teulemuandishi ametumia maneno hayo/ matmshi kwa lugha ya kisanaa ili kuiendeleza lugha ya kiswahili kupitia misemo/maneno teule. Usemi huu unaendana na msimbo wa kiseme amabapo elementi zinazopelekea kupata picha Fulani kutokana na viashiria Fulani tunapata kuelewa sifa kamili ya jambo, tukio, hali zinazojitokeza katika tamthiliya na kuihusisha na hali iliyopo katika jamii.

*KARUME: Huu ulimwengu hamna shujaa Chenye mwanzo kina mwisho (UK: 14).*

Msemo huu unamaanisha kuwa katika maisha ya hapa duniani hakuna hodari au anaeweza zaidi (Ukiwa ni kama binaadamu aliyeumbwa) kwa vile ameubwa na yuko aliena mwanzo- (Mwenyezi Mungu) kuna na mwisho wake binaadamu hivyo kwa kuweza kufikia kikomo (mwisho wa uhai wake). Dhamira inayojengeka hapa ni ile ya kuelimisha jamii na kuonesha ushujaa wa muhusika katika kujiamini katika maamuzi yake wakati wa mapambano kwa kumtegemea aliyemuumba kama ilivyjitokeza kupitia muhusika KARUME. Vile vile, tunapata msimbo wa kiishara ambapo msomaji anvyovumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

*RASHIDI: Karume hayo maneno yako debe shida, ni dua tu la kuku lisilomtisha mwewe sembuse tai wa Ikulu? (UK: 14).*
*IDDI: …….. Mtoto akilia wembe mpe umkate (UK: 24).*

Msemo huu unamainisha kwamba pale ambapo mtu atahitaji kitu kwa lazima basi na apewe ingawa linaonekanwa kuwa na madhara na likeshamdhuru basi atajuwa ubaya wa lile jambo/ kitu alichoking’ang’ania akipate/ apewe. Dhamira iliyojengwa hapa ni ile ya uelimishaji kwa jamiii, katika utumizi wa msemo huu tunapata hali ya tukio liliopo baina wahusika wa wafuasi wa watawala na wahusika wa watawaliwa. Hivyo,

muandishi hakuwa nyuma katika kutumia vionjo lugha kwa kuzingatia nafasi ya vionjo muhimu katika uandishi wa kazi zake kisanaa. Msemo huu uaendana na msimbo wa kiseme unaopelekea kupata picha Fulani kutokana na viashiria vinavyopelekea kuelewa sifa kamili ya jambo husika.

> *OKELLO: Minyororo ya mwafrika inamfunga na kumnyonga mwafrika mwenyewe, Nakwambia shukurani za Punda, mateke, Tenda wema nenda zako, mnyonge mnyongeni na haki yake umpe" (UK:65)*

Msemo huu unabainisha matumzi ya vionjo hivi vya misemo inayolenga lugha mkato na utajiri/ Uwezo wa lugha kuweza kumpatia muhusika kutumia nafasi yake vilivyo, kwani kilichokusudiwa hapa ni ile hali ya mwafrika kuwa katika hali ngumu ya kifungo na kumpelekea kumnyonga na kumfunga kutokana na kutotendewa haki, vile vile kutokuwa na shukurani kwa mwanaadamu ambae ametendewa wema au aliewatendea watu wema hupata majibu machafu yasiyokuwa na chembe ya shukurani kwa wale aliowatendea wema na khatimae hukosa thamani. Dhamira ya kupigania / kugombea haki kwa kutafuta na huku akiijutia jana yake na kuililia kesho yake. Mfano huu unaingia katika msimbo wa kimatukio ambao unahusu jinsi matukio yanavyoungana kushonana na kusababishana au kuathiriana.

### 4.4.2 Methali

Kwa mujibu wa Hamad (1981) katika kitabu chao cha "Misingi ya Nadharia ya Fasihi" Wameeleza kuwa "Methali" ni usemi mfupi wenye maana nzito au hekima ndani yake, methali hutumia lugha ya mkato ya kuonya au kusisitiza jambo fulani lugha huwa na mapigo maalum ya kuleta ladha ya ushairi. Aghlabu methali hutumika katika kuwaadhibu wadogo na kuwatanabahisha au kuwakumbusha wakubwa kwa

kawaida methali huwa inaeleza jambo au tendo fulani kwa sehemu moja na sehemu nyengine inatoa taathira, hila au rai ya tokeo hilo.

Hivyo basi, katika tamthilia ya "Sadaka ya John Okello" kuna baadhi ya methali ambazo zimejitokeza kama ifuatavyo:

*RAMADHANI: Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu (UK: 8).*

Methali hii imetoa maana ya kusisitiza zaidi watu kushirikiana na kuwa pamoja ili kuweza kuwa na nguvu moja na pia waweze kuepukana na udhaifu ambao utatokana na utengano kwa njia moja au nyengine.Dhamira ya methali hii ni kuimarisha ushirikiano kwa wanajamii ili wakamilishe malengo yao kwa urahisi na kuviepuka vikwazo vinavyoweza kuepukika. Pia methali hii inafungamana na msimbo wa kiseme ambao unatowa picha ambayo inafungamana na kuhusisha hali iliyopo na kuashiria hali ya furaha au msiba katika jamii iliyokusudiwa. Vile vile, tunapata msimbo wa kiishara ambao unahusisha jinsi msomaji anavyovumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

Vile vile kuna methali nyengine ambazo zimetumika na kuweza kustadi pale zilipofunika kwa mfano katika (UK: 650):

*OKELLO: Ama kweli mvumilivu hula mbovu.*

Methali hii imetumika katika kuipa sifa tofauti na ule uhalisia wa methali yenyewe isemayo, "Mstahamilivu hula mbivu" kutokana na matukio muhusika OKELLO amaeambulia dharau na kejeli kwa washirika wenziwe wa mapinduzi ya visiwani baada ya kwisha kuwapatia uhuru wao wazanzibari hali ilikuwa kinyume na

matarajio hali hii imesadifu mazingira ya ya mtendwa na kutumia kauli hiyo ya "mstahamilivu hula mbovu." Dhamira ya methali hii ni kuitanabahisha jamii juu ya kuzingatia haki na kuachana na batili kama ilivyojitokeza katika hali halisi ya mazingira ya muhusika hadi kufikia yale aliyoyapata ambyo hayakustahili na kuwa kama shukrani alizozipata baada ya kujitolea kihali na kwa bidii kubwa. Methali hii inakwenda sambamba na msimbo wa kiseme ambao unapelekea kupata picha kutokana na viashiria fulani na kuielewa sifa kamili ya jambo au hali zinazojitokeza katika tamthiliya.

### 4.4.3 Matumizi ya Tamathali za Semi

Katika sehemu hii tumewasilisha tamathali mbalimbali za semi kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.1 Tashbiha

Kwa mujibu wa, Hamad (1992) tash-biha ni mbinu inayotumika katika kulinganisha vitu vyenye sifa zilizofanana. Katika Tamthilia hii ya "Sadaka ya John Okelo" Tash-biha zimejitokeza kama ifuatavyo:

> *Jamshid: Utukufu wa Zanzibar ni kama bustani ya Mwenyezi Mungu (UK:4)*
> *Okello: Nikapiga magoti kama simba mwenye kiu (UK: 28).*
> *Okello: Nikainua kichwa kama Kiboko (UK: 28).*
> *Iddi: Nitajamchinja Rashid kama kuku wa kitoeo (UK: 35)*
> *Zanzibar: Mweusi kama chungu cha magimbi (UK: 39)*
> *Okkello: Tambaa kama chatu (UK: 41).*
> *Khalifa: Kayeyuka kama barafu (UK:49).*

Mifano ya Tashbiha zilizotajwa hapo tofauti kama vile umuhimu wa kuwa mpole wakati mtu anapokuwa na shida (*nikapiga magoti kama simba mwenye kiu),* umuhimu wa kujipanga katika jambo ambalo mtu anataka kulifanya *(tambaa kama*

*chatu),* pia inaonesha uzuri wa nchi ya Zanzibar *(utukufu wa Zanzibar ni kama bustani ya Mwenyezi Mungu). Dhamira ya kutumia tashbiha kama hizo ndani ya tamthiliya ni kuongeza ladha, haiba, mvuto na mnato wa lugha katika kuipamba lugha kwa umahiri wa hali ya juu. Vile vile tunapata msimbo wa kiishara ambao unahusisha jinsi msomaji wa kazi ya fasihi anavyoweza kuvumbua maana ya kiishara inayotokana na nadhariya ya simiotiki.*

#### 4.4.3.2 Lugha ya Ishara (Taashira)

Hamad (1992) ameeleza kuwa (ishara) ni mbinu ambayo hutumika katiaka kulipa neno maana pana zaidi, neno linakuwa kiwakilishi tu cha maana inayotakiwa, inaweza kuwa neno linahusishwa na chanzo kinachotaka kusema bali mpaka uhusishe na hicho kinachoelezwa. Katika Tamthiliya hi ya "Sadaka ya John Okello", muandishi ametumia baadhi ya lugha za ishara ambazo zimeweza kujitokeza kama ifuatavyo:-

> *BABU: Tuukatae uhuru wa Pweza hiki ni kibuyu hakina maji ndani (UK:6).*

Lugha hii ya ishara ambayo imetumika hapo ni sehemu iliyosheheni maana pana zaidi ili kulipatia ufumbuzi suala ambalo walikuwa wakilizungumzia kwa pamoja, neno uhuru wa pamoja ambalo utawatoa katika sehemu moja ya utawala / kutawaliwa na kuwaacha bila ya manufaa yao binafsi bali utakuwa ni udanganyifu tu, ili kuyaepuka yote hayo, muhusika Babu anawanasihi wenziwe kuachana na uhuru wa bandia. Dhamira ya lugha hii ya Ishara ni kujikombowa kwa kutoa angalizo maalum lililotumika kiufundi zaidi ili kukuza umahiri wake muandishi katika kipengele cha lugha na kumtaka msomaji wa Tamthilia hii kuhakiki lugha

iliyotunika kwa lengo la kuupata ujumbe uliokusudiwa kwa ustadi uliosahihi. Mfano huu unaingia katika msimbo wa kiishara ambao unamuhusisha msomaji na jinsi anvyovumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

> *OKELLO: Tutawafunza jinsi ya kukomanga vichwa vya Adui na kuukomboa ubongo wao (UK:9).*

Vile vile tunaweza kuona ya kwamba katika kipengele hiki kina lugha ya ishara ambayo imetumika mfano unaotoa maana pana zaidi ambayo ni “kuwakomanga” (kuukomanga) vichwa vya Adui na kumkomboa ubongo” maneno haya yanaashiria jinsi muhusika atakavyoweza kutekeleza majukumu yake kwa kutowa mafunzo ambayo yatajenga tabia zaidi kivitendo, ushujaa na kuachana na ujinga wa kutojielewa na badala yake kuweza kujikomboa wao (watawaliwa) na pia kuwajenga kiakili, na kuachana na wasiowapendelea raia kupata haki zao ndani ya nchi yao. Dhamira ya kutumia lugha hii ya Ishara inajemga ushujaa kwa raia kuwa tayari kujikomboa. Mfano huu unaingia katika msimbo wa kiishara ambao unampa nafasi msomaji kuweza kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

> *IDDIi: Njoni nyinyi mnayechimba dawa mmechuchumaa! (UK:23).*

Lugha ya ishara iliyotumika hapa ni ile ya mjengeko wa kitendo kinachoashiria watu wanaofanya kitendo cha kujisaidia katika hali ya kuchuchuma wakiwa wamo kwenye mapambano ya kutaka kujikomboa na muhusika huyu alitumia kauli hiyo hapo juu katika mazoezi ya kujiandaa na mapambano na alikuwa akionesha ukakamavu wake na jinsi atakavyoweza kupambana na maadui zake.Dhamira iliyojengwa hapa ni ya ukombozi kwa raia wa visiwani na kujipanga jinsi ya kukabiliana na utawala

uliokuwepo.Hapa tunapata msimbo wa kiishara ambao unaendana na nadhariya ya simiotiki inayomuhusisha msomaji kuvumbua maana kiishara katika kazi ya fasihi.

*IDDI: Nimerukia kule!Mkuki wangu koboakoboa unatema mate, Unatema mate ya sumu na kutetemeka kwa hasira dhidi ya vinyama- howa! Koboakoboa akapiga nelita (UK. 23).*

Vile vile, ndani ya mazungumzo ya muhusika “Iddi” majigambo yake yanaashiria hali tofauti kulingana na uwezo wake kimazoezi kwa lengo la kuung’oa utawala wa “Sultan Jamshid” Ishara zenyewe ni kitendo cha mkuki wake kuwa unatema mate, na mate hayo ni ya sumu na kutetemeka kwa hasira” hali hii haimaanishi kuwa mkuki unamaji ya sumu, bali kitendo cha ujasiri dhidi ya kumkabili “Adui” na uwezo wa mtendaji bila ya woga wa aina yoyote hadi kuwang’oa watawala na vibaraka vyao kwa pamoja na kuwarembea mkuki na kuufyatua bila ya woga. Dhamira iliyojengwa hapa ni ya kuitanabahisha jamii ya ya kuwa wakakamavu kwa kuweza kumpatia sifa kamilifu muhusika kulingana na uhusika wake wa kulifikia lengo lililokusudiwa. Hivyo msimbo wa kiishara unachukuwa nafasi yake katika mfano huu ambapo tunapata maana ya kiishara katika kazi hii ya fasihi ambapo mwanafasihi huvumbua maana kutokana na hali inavyojitkeza.

*MFARANYAKI : “ tumbueni macho yenu.*
*muimaki sheni yangu*
*sheni ya kondo dhidi ya wachuzi wa Binaadamu” (UK:24)*

Lugha ya ishara inayojitokeza hapa ni ile inayoashiria hali ya watu wanaoangalia kitu, jambo fulani kwa hali inavyojiri kwa watawala wanavyowauza na kununuliwa kama bidhaa kwa wageni, anaashiria utayari dhidi ya kutaka kujikomboa kutokana na unyonywaji na unyanyaswaji na kutafuta mbinu mbadala ya kuondoa hali hiyo.

Dhamira ya kuonesha majigambo kwa muhusika “mfaranyaki ambae alikuwa anatumia neno “muimaki shani yangu, shani ya kondo dhidi ya wachuuzi” yanayotokana na uboreshaji wa kimafumbo unaoashiria uangalifu wa kiutendaji. Vile vile tunapata msimbo wa kiseme ambao unapelekea kupata sifa kamili za jambo, tukio, au hali zinazojitokeza katika tamthiliya.

*OKELLO:“Mimba ilikaa kizazi kimoja*
*Na cha pili, kisha muda ulipotimu kinyonga alikwea mtini ,*
*Alikwea mtini, akadondoka na tumbo lake: Pwa! (uk:26).*

Ishara inayojitokeza hapa inatokana na neno “Mimba ambayo imechukua sifa ya kuchukua muda mrefu ambao umetumia kinyonga ili kuikammilisha sifa/tendo la myama huyo alieparamia(kukwea) mti akiwa na mimba yake na kudondoka, hii ina maanisha ni kuwa na matumaini ambayo yanabadilika kwa mujibu wa mazingira yalivyo, na pia kuna hali ya kuwa na matarajio ya kupata maisha mapya na tumaini jipya (mtoto atakaezaliwa)ili kupata mageuzi kimaendeleo ili kutikana na udhalilishaji unaotokana na Uongozi wa kigeni na kutarajia kuja kupata kiongozi wao ambae ataleta matumaini mazuri zaidi kwa muda wa pili ambao hautakuwa wa uhuru bandia, yaani watakapojitawala wenyewe kinyume na ule wa kwanza.

Dhamira ya lugha hii ya ishara ni kuzijenga Umakini wa wasomaji pamoja na kuzifanya fikra za msomaji ziende mbali zaidi kimawazo na kufumbua fumbo linaloashiria ujasiri wa wanaopambana na utawala wa kigeni ndani ya nchi yao. Msimbo wa kiishara unchukuwa nafasi ya kuendana na mfano uliotajwa hapo juu kwa msomaji kuweza kuvumbua maana ya kiishara.

*Okello: Povu moto linatoka mdomoni (UK: 28).*

Hapa tunaipata lugha ya ishara ambayo inatokana na moto kupewa sifa yenye maana pana zaidi kiutendaji kwa kuweza kutowa povu linalotoka mdomoni, na kuwa na maana ya kwamba muhusika huyu alitumia jitihada za hali ya juu hadi akaingia mori (jazba) ambayo ilipandisha hasira na kumfanya apambane kiume kwa kuukabili utawala wa kisultani kwa mbinu za hali ya juu bila ya kuwa na muhali wa aina yoyote. Dhamira ya kutumia lugha hii ni kuonesha ujasiri wa muhusika katika utendaji wake kwa mazingira ya uhusika wake katika kukabiliana na adui. Hivyo kupitia mfano huu tunapata msimbo wa kiishara amabo unafanya msomaji kuweza kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

Msemo mwengine unaopatikana hapa ni huu ufuatao;

*OKELLO: Tendawema uende zako (UK : 65).*

Msemo huu unamaanisha kwamba fanya jambo zuri kwa watu ukiwa na matumaini mema na usisubiri kusifiwa au kushukuriwa, ukishatenda wema uondoke na uwaachie mema yako.Dhamira ya kutumia usemi huu ni ya kujitolea kwa moyo wa dhati kama alivyofanya OKELLO kwa kuwapatia uhuru kwa msaada wake mkubwa visiwani Zanzibar yeye akiwa kama mdau mkuu wa mapambano hayo aliambulia lawama dharau na kejeli ambazo zilimfikisha pahala pabaya sana na kutopata shukrani ya kiungwana kwa wale aliowasaidia. kutokana na utumizi wa lugha hii ya ya ishara tunapata msimbo kiseme ambapo kutokana na elementi zinazopelekea picha Fulani kutokana na viashiria Fulani pamoja na kuelewa sifa kamili ya jambo, hali zinazojitokeza kwenye tamthiliya na kuihusisha na hali iliyopo kwenye jamii.

**4.4.3.3 Tash-hisi**

Njogu na Chimera (2008) wameeleza kwamba “Tash-hisi ni kuweka hisia au uhai

katika vitu visivyokuwa na uhai, ni kuvipa hisi za kibinaadamu." ni aina ya tamathali inayotumia mbinu ya kuvipa uhai na uwezo wa kibinaadamu vitu ambavyo havina uhai wala si biaadamu.

Katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* kuna Tash-hisi ambazo zimetumika kama ifuatavyo:

> *OKELLO: Mnasikia? Hata mbingu nazo zimekasirika. Radi na ngurumo zinaenda mbele yetu ili kuangamiza udhalimu (UK:42).*

Usemi huu wa Tash-hisi umechukua nafasi ya kuvipa uhai visivyokuwa na uhai, "Mbigu nazo pia zimepewa sifa za viumbe hai, kwa kutumia neno "zimekasirika" na "Radi" nayo imepewa sifa ya kutenda kitendo cha kuenda mbele "Zinaenda mbele" yetu kuvifanya kazi ya kuangamiza udhalimu sifa hizi ukizipembua unapata kitu kisicho uhai kubeba sifa ya kibinaadamu/ mtu alie hai na kutenda kitendo hicho. Dhamira ya usemi huu ni kujenga upembuzi wa mambo kulingana na mazingira ya muhusika "Okello" alipokuwa anahamasisha wenzake katika kujikomboa kutokana na utawala kwa waafrika wa visiwani katika kujikomboa kutokana na utawala wa "Jamshid"(sultan) ili kupata uhuru wao. Mfano huu umejikita zaidi katika msimbo wa kimatukio ambapo unahusu juu ya matukio yanavyoungana na kushonana katika tamthiliya hii pamoja na jamii inayohusishwa.

> *BAVUAI: Naona Mzee kombe la kiapo*
> *limekoleza ujasiri*
> *na ukatili ndani yako (UK: 46).*

Tash-hisi inayojitokeza hapa ni ile ya neno kombe" la kiapo ambalo limepewa sifa ya kutenda kama kumbe hai/binaadamu ambalo ndio lililokuwa na ujasiri na ukatili ambao limepoteza imani ya "IDDI" na hata kumchukia mwenziwe "Rashidi" kuwani

maana hasa iliyokusudiwa hapa ni ile ya kumkomaza moyo wa mwenye kutaka kujikomboa kutokana na sultani. Dhamira iliyojengwa hapa ni ile ya uzalendo kwa wazawa kuwa tayari kujitolea kwa manufaa ya nchi yao. Mfano huu unendana nadhariya ya simiotiki kupitia msimbo wa kiishsra ambao unahusisha jinsi msomaji wa kazi ya fasihi anavyoweza kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

#### 4.4.3.4 Tanakali Sauti

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) ameeleza kwamba tanakali sauti ni mbinu ambapo neno fulani linaigiza sauti ya kitu fulani, Tanakali sauti zimejengwa kwenye misingi ya ushabiki kweli wa kisauti, yaani kujaribu kuonyeshab mfanano wa ukweli wa sauti fulani. *Tanakali sauti hii ni ile hali ya kutumia mlio wa sauti ya kitu au mtu ambayo huwa yanatumia sauti zinayofanana kwa wakati mmoja.*

Katika tamathali ya sadaka ya John Okello" kuna matumizi ya tanakali sauti ambazo zimejitokeza kama ifuatavyo:-

*MFARANYAKI: Nikacheza ha! ha! ha!haaa" (Uk: 25)*
*BABU: "Aaa!" "Eeee!! (UK:15)*
*OKELLO: "Brruuu"*
*OKELLO: "Uwiii". (UK:26).*
*IDDI: "Papapa"! (UK: 23)*
*IDDI: "Wo". (UK:22).*
*MFARANYAKI: "Bruuurrruuu".*
*"Eeee". (UK : 25)*
*MFARANYAKI: "Tiii".*
*"Wee". (UK: 26).*
*OKELLO: "Tatatatatabatatatataaaa! (UK:27):*
*OKELLO: ''Bruuu!, paaa!''*
*"Waaaaa" (Uk:27)*
*OKELLO: "Yaaaaaaaaaaaaaaaaaaaaaa! (UK: 28).*
*IDDI: ''Aaa!'' (Uk: 35)*
*ZABANIA 2: ''Haa!" (UK:39)*
*ASKARI: Tu – tu – tututuuu! (UK:41).*

Mifano iliopo hapo juu ni miongoni mwa tanakali sauti ambazo zimejitokeza katika Tamthilia ya *Sadakya John Okello*, kupitia muandishi wake mahiri Emmanuel Mbogo ili kuyaendeleza matumizi ya Tamathali za semi kwa muendelezo wa kazi yake kifasihi na kwa ustadi wa hali ya juu. Dhamira ya utumizi wa Tanakali sauti hizi zilizomo ndani ya kazi yake hii ya fasihi na kuipa uhai zaidi lugha ya Kiswahili kwa kuongeza vionjo mbali mbali vya lugha ambavyo vitamvutia na kumpa nafasi zaidi msomaji ili aendelee kusoma na kuvutika na kazi hiyo ya fasihi. Pia kupitia tanakali sauti hizi tunapata msimbo wa kiseme ambao unatowa picha kutokana na viashiria Fulani na kuelewa sifa kamili ya jambo, tukio, na hali zinazojitokeza katika tamthiliya na kuzihusisha na hali iliyopo katika jamii.

#### 4.4.3.5 Takriri

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) ameeleza kwamba urudiaji ni sifa muhimu inayopatikana siyo tu katika mtindo wa kazi ya fasihi bali pia katika maisha ya binaadamu yenyewe. Uchunguzi katika kamusi yoyote ya lugha unadhihirishaukweli wa kwamba sifa ya urudiaji inajitokeza katika sehemu nyingi ingawa majina wanayoyatumia kuelezea yanatofautiana kutegemea ni nini au nani anayehusishwa na urudiaji huo. Khatib (Mulika 18) ameeleza kwamba Takriri ni usemi unaojidhihirisha katika neno au kifungu cha neno kwenye mfululizo na mfuatano wa sentensi. kwa upande wa Tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello* kuna baadhi ya Takriri ambazo zimejitokeza kama ifuatavyo:

*ASHURA: Leo! Leo!” (UK: 12).*
*IDDI “ Wai! Woi, Woi”! (UK: 22)*
*IDDI: Njoni! Njoni!”*
*Hola! Hola! Hola!”.*
*“Patupu!Patupu!”*

*"Hola!   Hola!" (UK: 23)*
*OKELLO: "Chukua Silaha! Chukua Silaha!" (UK:29)*
*BIBI: "Machozi! Machozi!" (UK: 36)*
*ASKARI: "Hiya!  Hiya! Hiyaaa!" (UK: 41)*
*ASKARI "Hiyaa! Hiyaa!"*
*ASKARI: "Chetuu! Chatuu! Chatuu!'*
*"Hiyaa!  Hiyaa!"*
*BAVUI "Uwa! Uwa!"*
*"Uwa! Uwa". (UK: 45)*
*OMARY: "Tuharakishe! Tuharakishe!" (UK:51)*
*ZIMWI 2: "Okello! Okello!" (UK: 55)*
*RASHIDI: "Baa – baa- Baba!?" (UK: 60 )*
*ABDULLA: "Miaka ikapita, Miaka Ikapita" (UK:61)*

Mifano yote hiyo ni miongoni mwa takriri ambazo muandishi wa kitabu hiki cha Sadaka ya John Okello" amezitumia na kuweza kujitokeza katika kurasa tofauti, takriri hizi zimechukuwa nafasi nzuri inayoongoza mvuto na ushaijihisho kupitia wahusika. Dhamira ya utumizi wa takriri ni ushereheshaji na upambaji wa lugha kwa kuingiza vionjo kama hivi na kuwa ni miongoni mwa mbinu zinazoengeza umahiri wa muandishi wa Tamthiliya na kuonesha msisitizoto juu ya kile kinachowakilishwa. Hivyo mifano yote hiyo inaendana na nadhariya ya simiotiki katika msimbo wa kiseme unaotowa maana kutokana na vielezea vinavyotowa sifa kamili ya hali zinazojitokeza katika jamii.

### 4.4.3.6 Lugha ya Picha/ Taswira

Kwa mujibu Haji (1992) anaeleza kwamba lugha ya picha inatokana na namna mwandishi au msimulizi anavyoweza kueleza habari hata msomaji au msikilizaji akaweza kujenga mawazo ya wazi wazi kuhusu habari hiyo. Muandishi anaweza kuelezea hisia zake kuhusu mji au mahali Fulani, wasfu wa mtu, mnyama au hata hali ya matokeo mbali mbali.

Katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* lugha ya picha imejitokeza kama ifuatavyo:

> *BABU: Hiki ni kibuyu hakuna maji ndani Hili ni boga, halina mbegu ndani,Hakika huu ni utasa, hauna mimba ndani wazanzibari amkeeeeeenii!!! (UK: 6).*

Hapa tunapata lugha ya picha ambayo inatokana na kibuyu ambacho kina maji ndani yake, inatokana na kibuyu na maji yaliyomo, pia tunapata picha ya boga ambalo limekosa kuendelea au kuku wa vizuri kwa vile halikuwa na matunda mengi yaliyo mazuri zaidi hapo pia tunapata picha, pia tunaweza kuuona utasa ambao hauna mimba, yaani ni kitu kisichokuwa na kizazi au matunda ambayo yalihusishwa na wazanzibar. Dhamira ni ya ukombozi ambayo imetumika hapa kuiendelea na kuikuza lugha kisanaa zaidi kwa kuipa akili nafasi ya kuliona au kulitafuta jambo lilivyo kwa mujibu wa Muktadha uliokuwa unazungumzwa na "Babu" kuhusiana na maisha ambayo walikuwa wanaijadili Zanzibar kutokana na hali ngumu ya maisha ambayo ilikuwa inaendeshwa na Uongozi wa Sultani Jamshidi. Vile vle tunaata msimbo wa kiishara ambao unampa nafasi msomaji ya kuivumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi, msmbo huu unakwenda sambamba na nadhariya ya simiotiki katiak utumiz wa lugha ya alama na ishara.

> *OKELLO: "Wazanzibari hawatabakia vifaaranga wa kunyakuliwa na vipanga na mwewe kwa mapanga na hata mawe. Mdhalimu mkoloni tutamtia kiwewe, tutawachoma moto ndani ya makasiri yao wenyewe. (Uk:7)*

Lugha ya picha ambayo tunaipata hapa ni kupitia mazungumzo ya "Okello" kuhusiana na Wazanzibari jinsi watakavyojikomboa na kuachana na hali ya kuwa kama matowezi ya watakaochukuliwa na vipanga na mwewe, picha hii ya vifaranga na mwewe tunaipata Kwa mapanga na hata mawe "pia tunaipata picha nyengine ya

mapanga na mawe na pia tunapata kitendo cha moto ambao unatiwa ndani ya Makasiri yao. Dhamira ambayo imejengwa hapa ni ya kuonesha unyanyaswaji wa rai. Msimbo wa kiishara unaendana na mfano uliotajwa hapo juu na kuonesha jinsi msomaji anavyovumbua maana ya kiishara katika kazi hii ya fsihi.

> *OKELLO: Katika hili tunahitaji kasi ya mawindo ya chuma msituni, stadi za mawindo ya mamba wa mtoni, mbinu za tai Mfalme wa anga na ujasiri wa samba mfalme wa Serengeti (UK: 8)*

Lugha ya picha ambayo inapatikana hapa ni ile kubainisha juhudi za wana mapinduzi watarajiwa katika kutafuta uhuru wao, picha ya mwendo wa kasi wa mawindo ya duma msituni unapata picha ya chuma" "mawindo" na msituni vile vile tunapata picha ya "mamba" wa mtoni", na "Simba wa Serengeti".Dhamira ambayo inapatikana hapa ni mapambano dhidi ya utawala wa kisultani.mfano huu unendana na msimbo wa kimatukio ambao unahusu jinsi matukio yanavyoungana kutokaana na kuathiriana katika tamthiliya.

> *OKELLO: Siri yetu midomoni mwao haitotoka. Tutavifunga viwanja na mioyo yao kwa kufuli za kiapo cha kifo atakaetoboa siri damu yake na damu ya ndugu zake itakuwa halali ya Jinni Makata, jinni subiani na Jini Maimuna (UK:9).*

Hapa tunapata lugha ya picha inayotokana na "Midomo" "Vinywa" na "mioyo ya" "kufuli za kiapo", kifo" "damu", pia tunapata picha ya hali ya viumbe visivyoonekana kwa macho| ''Jinni" vitu vyote vilivyotajwa hapo juu ndani ya sentensi zinazozungumzwa hapa vimetoa picha fulani kwa mujibu wa muktadha wa mazungumzo yanayoashiria kitakachotokea kupitia muhusika wake juu ya kuitunza siri yao.

Dhamira iliyojengwa hapa ni ya ujasiri inayopatikana na umuhimu wa kutunza siri ili kuweza kufanikisha mambo muhimu yaliyo na maslahi na jamii nzima. Kwamba

kuna wakati ni lazima wahusika walazimishwe kutunza siri hata kama ni kwa vitisho, ikiwa tu kuna lengo la kutaka kuikomboa jamii nzima kutokana na udhalimu uliopo. Hivyo uchanganuzi huuu unaendana na nadhariya ya simiotiki kupita msimbo wa kiseme ambao unahusisha viashiria vinavyojenga sifa kamili ya jambo kutokana na vishiria vya jambo au tukio.

> *RAMADHANI: Huwadunda na kuwatwanga waafrika kama anauwa nyoka, huwatia ngeni, majaraha na vilema vya kudumu na wengine hupoteza maisha. Tazama! (UK: 10).*

Lugha ya picha ambayo inapatikana katika kipengele hicho hapo juu ni ile ya “Waafrika”, katika kitendo cha “kuwadunda” na “kuwatwanga”, “nyoka”,” majeraha” “vilema vya kudumu” na pia kitendo cha kupoteza maisha kinatowa Taswira fulani ambayo ni kupoteza maisha (kwa kufariki). Dhamira iliyojengwa hapa inaonesha unyanyaswaji wa raia wa visiwani.ya kutumia lugha hii ya picha ni kuijenga hali ya uwazi kwa kivitendo baina ya muhusika anaetamka na wale wanaotamkiwa kuwa ni waafrika wenziwe. Vile vile tunapata msimbo wa kimatukio unaohusu matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na kusababishana na kuathirian kwa matukio kama yalivyojitokeza katika mfano ulitajwa hapo juu.

> *ASHURA! Machozi yangu yanaisuta jozi ya chura mwenye woga wa kuingia majini ili kupiga mbizi (UK:12).*

Lugha ya picha ambayo imejitokeza hapa ni ile ya kitendo cha mtu (ASHURA) ambae amejihusisha yeye na aliyonayo neno “Machozi,” jozi ya chura,” “majini,” (sehemu yenye maji maji yanayoingia chura, na pia tunapata kitendo cha “kupiga mbizi (kurukia majina kuyaingia ndani).” Dhamira iliyotumika hapa inajenga ujasiri wa muhusika katika kuithibitisha hali au tukio kupitia muhusika wake. Pia, ni ile ya kuibua fikra bainifu za muhusika kupitia msomaji wa kazi ya fasihi kwa hali

ilivyojitokeza kisanaa zaidi na kuzibaini picha zinazojengeka katika mazungumzo ya muhusika na mazingira. Mfano huu unaendana na msimbo wa kiseme unaopelekea kupata picha Fulani kutokana na viashiria vinavyoelezea sifa kamili ya jambo linalojitokeza.

> *RASHIDI: litakuja jeshi la mwewe na vipanga liwateke nyara ka vifaranga na jikoni tutawakaanga tuwapike kitoweo, kwa mchuzi wa karanga (UK:14).*

Lugha ya picha imejitokeza katika maneno ya “jeshi! La mwewe na vipanga” ambalo linatokana na hisia za machoni fadhaa na, picha ya kuwateka nyara ka vifaranga,’ napo pia tunapata picha ya viumbe hai wadogo sana wanochukuliwa kana vifaranga (vitoto vya kuku au mnyama fulani). Dhamira ya kujenga umakini wa msomaji wa kazi ya fasihi kwa kutumia lugha hii ya picha ni kuonesha uimara wa jeshi la kudai uhuru wa wanyonge. Nao pia ni mfano unaoendana na nadhariya ya simiotiki kupitia msimbo wa kiishara na jinsi msomaji anavyovumbua maana kiishara.

> *IDDI: Machozi ya karovya kifua chake… Mama nisubiri kidogo bado nasana silaha, bado natengeneza upinde wangu, bado nafua, mishale yangu (UK:22).*

Lugha ya picha imetumika katika hali ya kuonesha “machozi yakarovya kifua” unaiona picha halisi ya machozi yanavyorovya kifua na neno “kusana silaha” unaipata picha ya kuichukua silaha kuitengeneza au kuipanga vyema “upande” unaotengenezwa pamoja na “mishale” ambayo itatengenezwa. Dhamira ya ujasiri wa muhusika katika kupigania haki utumizi wa lugha hii ni kuonesha kuwa iwapo madhila yamezidi wanajamii hawana budi kujitayarisha ili kuweza kuondoa matatizo hayo kwa namna yoyote ile. Sambamba na hilo msimbo wa kiseme umechukua nafasi yake kutoka katika nadhariya hii ya simiotiki ambayo inatokana na vielezea vinavyoelezea sfa kamili ya hali zinazojitokeza katika jamii.

*IDDI: Nilikuwakabili na mkuki wangu huu*
*Mkuki wangu huu unaitwa koboa koboakoba, koboakobo niliyemsana tumboni mwa mamaangu mwajuma! (UK:23).*

Lugha ya picha ambayo imejitokeza hapa ni ile ya "Mkuki" na tumboni mwa mamaangu" unaipata taswira ambayo unaipata picha hasa na inajenga hali ya Ukoloni wa karuibu zaidi. Dhamira iliopo hapa ni ya kuijenga na kuipamba lugha ili kupata vionjo vinavyovutia na kuivutia hadhira. Mfano huu nao unaendana na nadhariya simiotiki kupitia msimbo wa kiishara unaoendana na kumpatia nafasi msomaji kuweza kuvumbua maana ya kiishara.

*MPARANYAKI: Wadhalimu waliokuwa wakichoma mishikaki mapaja ya dada zetu waliokuwa wakibanika na kula maini na figo za watoto wa visiwani (UK:24).*

Lugha ya picha ambayo imejitokeza hapa ni ile ya Wadhalimu waliokuwa "wakichoma Mishikaki mapaja" ya dada zetu, hii inatowa taswira ya kitendo cha kuchomwa mishikaki na hayo mapaja ya dada zao, unaona hali inavyozungumzwa na unavyojenga ufahamu wa kile kinachowasilishwa, "maini na figo ya watoto wa visiwani nayo pia unaipata picha fulani inayojitokeza kwa muktadha husika. Dhamira kujenga umakini wa msomaji katika utumizi wa lugha kisanaa ya lugha hii ya picha nayo pia imetokana na ustadi wa kuvihusisha viungo vya mwili wa binaadamu na visiwa vya Zanzibar kwa kuunganisha msamiati ilivyo na mafumbo na kumjengea picha fulani msomaji wa kazi ya fashi, ikiwemo, mishikaki ya mapaja, na maini na figo za watu". Hivyo basi msimbo wa kiishara unachukua nafasi zaidi kwa kumpa nafasi msomaji wa kazi ya fasihi kuweza kuvumbua maana ya kile kilichokusudiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ambapo msmbo huu unaenda sambamba na nadhariya ya simiotiki.

*MFARANYAKI: Wale wale nyama za watu wale! Wale mbweha kasoro mkia wale! Niliwakabili, nikifumbata upanga wangu, Huu uitwao: Chetocheto (UK: 25).*

Hapa tunaipata lugha ya picha kama vile “nyama za watu” “Mbweha” na “upanga” picha hizi zimetokana na tamathali za usemi uliotumika hapa na kupata hali fulani ambayo unajenga taswira inayoonekanwa na kufanyiwa kitendo cha kuliwa. Dhamira ya utumizi wa lugha ya picha hapa nikuonesha majigambo yanayoonesha ukakamavu wa muhusika. Kupitia mfano huu tunapata msimbo wa kiishara ambao unaashiria ukatili, ugumu na udhalimu wa utawala wa wageni (Sultani Jemshid) ndio uliopelekea kuibuka kwa wanaharakati wanaoitafuta haki yao. Kutokana na mfano huu tunapata msimbo wa kiseme unaotowa sifa kamili ya tukio linalohusishwa kutokana na vielezea vyake katika jamii ambapo inafungamana na nadharia ya simotiki kupitia misimbo yake.

*MFARANYAKI: “Giza linaingia”*
*“Niliwakabili nikifumbata upanga wangu, Huu uitwao chetocheto”*
*(UK:25)*

Lugha ya picha inajitokeza hapa ni ile ya kuliona “Giza” kihisiajinsi linavyoingia, na pia tunapata kitendo cha “Upanga” kufumbatwa. Dhamira inayojitokeza hapa ni kuendeleza majigambo ya kudhihirisha kitendo na hali halisi ilivyo na jinsi inavyojitokeza. Mfano huu pia umejikita katika msimbo wa kiishara kama ulivyojitokeza katika hali inayomfanya msomaji kuvumbua maana kutokana na ishara iliyojitokeza katika kazi ya fasihi kwa jamii ambayo inaendana na nadhariya inayohusishwa katika uchanganuzi huu wa data.

*MFARANYAKI: Ubinda uliokuwa umefunika zunga lake, siku ya tahiri niliye yafyeka yale marapurapu yaliyokuwa yakining’inia hadi magotini. (UK:26)*

> *Nikayasokomeza ndani ya mazibala ya domo lake, mwenyewe nikapasua anga, jitafune mwenyewe, mtoto wa mbwa "wee!"*

Lugha ya picha ambayo inajitokeza hapa ni ile ya utumizi wa vifaa na vitendo kwa binaadamu, tunapata picha ya "Ubinda" "Zunga", "niliyafyeka", "marapurapu", "magotini", "mazibala ya domo lake", "nikapasua anga", pia kitendo cha kusema "jitafune mwenyewe".

Kuipangilia lugha na kuimarisha majigambo ya muhusika wake katika harakati za kutaka kujikomboa na utawala wa Kisultani. Dhamira iliyojengwa hapa ni kuipambamba lugha kwa kuisherehesha kwa misamiati teule kama ilivyojitokeza hapo juu. mfano huu unafungamana na nadhariya ya simiotiki kupitia Msimbo wa kiishara ambao umejikita zaidi katika kumpa nafasi msomaji kuvumbua maana iliyotumika kiishara.

> *OKELLO: Wakaingia Pangoni- Faraghani Hisia zao zikaumana kiu zao zikakatika katika (UK:26).*

Lugha ya picha iliyopo hapa ni ile ya maeneo ya "Pangoni, "Faraghani", pamoja na kitendo cha "Hisia zao zikaumana" na picha ya kiu zao zikakatika katika. Hii inajenga picha fulani inayompitikia msomaji moja kwa moja ndani ya macho yake" Dhamira ya kuburudisha kwa kuzivuta hisia za msomaji, kwa kuitumia lugha hii kwa kuivutia hadhira kwa kuyaona mazingira yanavyozungumziwa na muandishi katika hali ilivyo kwa mujibu wa mazingira yalivyotumika. Napo pia kunaendana na nadaariya ya simiotiki kupitia Msimbo wa kiseme ambao umechukuwa nafasi zaidi ya vielezea vinavyotowa sifa kamili a hali zivyojitokeza katika mfano uliotajwa hapo juu.

*OKELLO: Povu la moto linatoka mdomoni (UK.28).*

Lugha ya picha inajitokeza hapa bi ile ya kitu “Povu” jinsi linavyoonekanwa pale linapotamkwa na “moto” ambao ndio unaotoa povu hilo, pia tunapata hali ya mdomoni ambamo ndimo mnatoka mto huo wenye kutoa nafasi kwa kuweza kutoa povu*”*.Dhamira ilijengwa hapa ni kuisherehesha lugha kwa vionjo vya kisanaa. Hivyo, mfano huu unaingia katika nadhariya ya simiotiki kuptitia msimbo wa kiseme unaompa nafasi msomaji wa kazi ya fasihi kuelewa sifa kamili ya hali au ntukio husika.

**4.4.3.7 Kejeli**

Kwa mujibu khatib (1985) kejeli ni usemi ambao maana ya ndani na kinyume cha yale yasemwayo. Kejeli ni aina ya usemi ambao unatumia neno au maneno kinyme kwa kumwambia mtu au watu ambao hupewa ujumbe kwa lengo la kuwakejeli kutokana na muktadha husika.

Kejeli ambazo zimejitokeza katika Tamthiliya ya “Sadaka ya John Okello” kuna baadhi ya kejeli ambazo zimejitokeza kama ifuatavyo:

*RASHID: “Ali Babu, wewe ni Babu Ama Babuni? Ama Bamboo, tete tupu lisilojaa nyama. Au ni Babu kubabuka, Kapanda mti kaanguka?” (UK: 13).*

Kejeli iliyotumika hapa ni ile ya kuonesha jinsi muhusika anavyomdharau na kumtolea maneno yasiyokubalika kwa mtu kumwambia mwenziwe katika hali ya kumkejeli kwa kumwambia “wewe Babu Ama Babuni?” “Ama Bamboo,” “tete tupu lisilojaa nyama na hata katika muendelezo wa mazungumzo ya muhusika nao unaulizia “Babu kababuka, kapanda mti, kaanguka “zote hizo ni kejeli baada ya

kujiona yeye yupo madarakani chini ya Uongozi wa utawala wa “JAMSHID”. Dhamira ya kusherehesha katika utumizi wa kejeli ni kuonesha jinsi gani wahusika wa upande wa pili wa utawala wa “Jamshid” walivyokuwa wanakwenda kinyume zaidi kwa watawaliwa hata kama ni wenzao wanatoka sehemu moja, eneo moja na hata wakiwa ndugu. Msimbo uliosadifu mfano huu ni msimbo wa kiishara ambao unampa nafasi msomaji kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

> *ASHURA: Huna mama Rashidi, asituletee uhanisi wako (anafyonya). (UK: 14)*
> *ASHURA: Huna Mama Rashidi, ndio maana huna chembe ya huruma ibilisi we!” (UK: 14).*

Katika mifano hiyo hapo juu tunaipata kejeli inatokana na muhusika mmoja kumwambia muhusika mwengine neno “Usituletee uhanisi” na maneno ya “ASHURA” kumwambia “RASHIDI” “Huna mama Rashidi, ndio maana huna chembe ya huruma ibilisi we!” zote hizo ni kejeli ambazo zinazungumzwa kwa kumdhihaki au bezo ambalo linatokana na vitendo vya mtu pale anapotumia maneno hayo. Dhamira ya muandishi katika uingizaji wa kejeli hizi ikiwa ni kipengele cha lugha ni kuweza kuzitofautisha kauli za muhusika mmoja na muhusika mwengine, kutoka watawala na watawaliwa, pia kwa upande wa uongozi uliopo madarakani na vibaraka wake kwa kuingiza vionjo hivyo. Mfano huu unaendana na msimbo wa kimatukio ambao unaonesa kushikana na kuathiriana kwa matukio kulingana na jamii husika.

> *MFARANYAKI: Nikamvika tusi: wewe msonga Ugali jikoni, moto wa ushuzi wa mtoto unatosha kukubabua na kukuteketeza (UK: 25).*

Kupitia mfano huu pia tunapata kejeli ambayo imetumika kwa lengo la kuonesha hali ngumu ambayo imemfika muhusika na kutumia kejeli hizo zenye bezo kubwa ndani

yake, kejeli ya “Kuvika tusi” na ushuzi wa mtoto “ambao umepewa sifa ya “kubabuwa na kuteketeza, hizo zote ni kejeli kwa mifano iliyowazi. Dhamira ya Mwandishi wa Tamthiliya hii ni kuonesha matumizi ya kejeli kupitia muhusika mmoja kwenda kwa mwengine, ubunifu wa maneno teule kuweka wazo halisi kitamathali ili kuepusha kuingiliana kwa matamshi ya kawaida na yale yasiyo ya kawaida. Mfano huu unendana na nadhariya ya simiotiki kupitia msimbo wa kiseme ambapo elementi zinapelekea kupata picha Fulani kutokana na viashiria na kuelewa sifa kamili ya jambo kama ilivyo katika nadhariya ya simotiki.

> *OKELLO: Njoni ninyi mafedhuli niwatoe roho, mama mzazi! Njoni enyi wenye akili fugutu Niwasinge liwa la damu kwa mifupa yenu wenyewe (Uk: 27).*

Kejeli inayojitokeza hapa ni ile ya kutoka kufanya tendo kulingana na hali za wale wanaotaka kupewa au kuambiwa jambo husika kwa mfano “ninyi mafedhuli niwatoe roho,” “wenye akili fungutu,” niwasinge liwa la damu kwa mifupa yenu,” zote hizo ni kejeli zinazotoa ishara ya kudharau na kuwabeza wale wanaowanyanyasa wenzao (watawaliwa). Dhamira ya kutumika kwa kejeli hii ni kuonesha ukakamavu wa muhusika mmoja dhidi ya mwengine kwa kutaka kupambana na utawala wa Sultani, muandishi huyu ametumia misamiati hii kwa ustadi wa hali ya juu. Kutokana na mfano huu tunapata msimbo wa kiishara ambpo unampa nafasi msomaji kuweza kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi msimbo ambao unaendana na nadhariya ya simiotiki kama alivyosema Barthes (1994).

> *ZABANIA 2: Na sikilizeni wanaharamu minyi (UK:39).*
> *IDDI: Namtaka Rashidi afande, nimchambe, nimsute mwanaharamu Yule kabla sijasahau ukatili alionifanyia nilipokuwa Mtumwa wa Ikulu (UK: 44).*

Kejeli tuipatayo katika mifano hii ni ile ya “nimchambe”, “nimsute mwanaharamu Yule”, pamoja na neno “waharamu ninyi.” Kejeli hizi zina majiigambo ya muhusika katika kukabiliana na vibaraka vya “Sultani Jamshid” na kutumia maneno haya ya kejeli. Dhamira ya kutumia kejeli hizi ni kuonesha athari za unyanyaswaji wa raia kipindi cha utawala wa sultani hali ilikuza jazba kwa muhusika alieathirika na utawala huo. Kwa mfano huu tunapata msimbo wa kiseme ambapo tunapata picha Fulani inayotokana na viashiria Fulani kueleza sifa kamili, jambo, tukio, hali zinazojitokeza katika tamthiliya pamoja na hali iliyopo.

> *Zimwi 1: Maswali ya kijinga! Ulifuata nini hapa,*
> *Nani alikualika? Lione kwanza! Kazi majigambo tu! (UK: 55)*
> *IDDI: Yule shetani, kibaka mkubwa! (UK: 58).*

Vile vile tunaiona mifano mengine ambayo inatokana na wahusika wanavyotumia neno “Yule Shetani “kibaka mkubwa” ni kejeli ya kutaka kumtoa mtu katika nafasi ya ubinaadamu na kumpa nafasi isiyokuwa yake (kinyume) kwa mazingira anayohusishwa nayo, “Maswali ya kijinga ulifuata nini hapa”, “Lione kwanza kazi Majigambo tu.” Hizo zote ni kejeli zilizotumika kwa kumbeza mwenzao baada ya mafanikio au kuupata uhuru wao, Dhamira iliyojitokeza ni ya tunayoipata hapa ni ile ya kuonesha mgongano wa mawazo waliokuwa nao wahusika kwa utawala wa sultani na kukitumia kiswahili kwa maneno ya mkato yaliyojaa bezo kwa mazingira husika ili kuongeza mawanda zaidi katika kuitumia lugha kwa muktadha husika na kuipanga kwa ustadi wake. kupitia mifano hii ni wazi kwamba unaendana na msimbo wa kihementiki ambao unahusu taharuki na pia unajulikana kama msimbo wa kusimulia hadithi.

> *OKELLO: Aa! Sultan Jamshid yuko London anakula raha, na wewe Okello umeishia ndani ya shimo hili la Panya buku (UK: 63).*

Kejeli nyengine ni ile ya kuoensha dharau kwa muhusika anaezungumzia nafasi iliyomuweka na majuto baada ya kusalitiwa na wenzake kwa kutothamanika baada ya Mapinduzi waliyofanya huko visiwani Zanzibar, neno Jamshid anakula raha London wewe Okello umeishia ndani ya shimo hili la Panya buku" kauli zote hizo zinaingia kwenye bezo la kujitia nafsi yake muhusika kwa kitendo alichotendewa na wenziwe. Dhamira kutumika iliyojengwa hapa ni ya usaliti wa wafuasi wa Okello baada ya kuifanikisha kazi waliyoipanga pamoja na kulifikia lengo khatimaye walimkana kama wasiemjua. Pia tunapata msimbo wa kimatukio ambao uaendana na matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na kusababishana au kuathiriana.

Matumzi ya lugha mchanganyiko (Kiswahili na kiarabu) aghlabu matumzi haya ya lugha mchanganyiko huwa yanatumia baadhi ya maneno yasiyokuwa ya Kiswahili, yaani huongeza maneno ya lugha ya Kiarabu kwa wakati mmoja. Katika Tamthiliya hii ya "Sadaka ya John Okello "yaani huongeza maneno ya lugha ya kiarabu kwa wakati mmoja. Katika Tamthiliya hii ya "Sadaka ya John Okello" kuna baadhi ya misamiati ya kiarabu imetumika kama ifuatavyo:

> *MWARABU: "Hata wewe shetani! Kelbi (UK: 11).*
> *MFARANYAKI: "Tazama! Astaghfirullah (UK:10).*
> *ashura: Karudi nyumbani akiwa hai inatosha Alhamdulillahi labillaalamina (UK: 15)*
> *TIPPUTIP: Washenzi ninyi Kelb! Laanatullahi aleiki" (UK: 18)*
> *RASHIDI: Alhamurillakh! Kufuru gani hii isiyokifani: Bibi? (UK: 58)*
> *IDDI: Mtume Muhammad Swallalwahu aleihi wasalaam!" (UK: 61)*

Mifano yote hiyo imetumia baadhi ya misamiati ya lugha ya kiarabu ndani ya lugha ya kiswahili katika mawasiliano ya watu wawili ambao hutoa ujumbe kulingana na

muktadha husika. Mifano hiyo ni kama vile neno “Kelb,” “Astaghfirullah”, “Alhamdulillahi labillalamina”, “laanatullahi aleik”, “Alhamdulillakh”. Hayo ni maneno yanayotokana na lugha ya kiarabu kwa asili yake na maana zake ni Mbwa (Kelb), kumuomba msamaha alwenyezi Mungu (Astaghfirullhah), kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa Viumbe vyote (Alhamdullillahi labillaalamina), Mbwa ulilaaniwa na Mwenyezi Mungu juu yako (Kelb! Laanatullahi alaiki), Rehma za Mwenyezi Mungu zimshukue juu yake na Amani

Matumzi ya lugha ya kiingereza ndani ya matamshi ya Kiswahili, muandishi ametumia baadhi ya maneno ya kiingereza ndani ya mazungumzo ya muhusika kwa kuzungumza na wahusika wengine kwa mfano:

> *BABU: “Tunahitaji kumobilaizi umma ili kuinua urazini wao ukifikia kilele ni mintarafu nadharia ya Marxisim Leninism na ile ya Diale etical Materialism na Class- struggle ee… (UK: 15).*

Hapa tunapata maneno yasiyokuwa na asili ya Kiswahili wala maandishi yake hayana uasili wa Kiswahili ila yamechanywa katika matumiz ya lugha ya kiswahili inajihidhirisha ndani ya mifano iliyopo hapo juu. Dhamira ya utumizi wa lugha mchanganyiko inatokana na kuathiriana kwa lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni ikiwemo kiarabu na kiingereza ni miongoni mwa njia ya kuonesha ustadi wa hali yajuu kutaka kuonesha muingiliano wa watu wenye lahaja tofauti na kuiathiri luga mama. Nayo pia inaendana na nadhariya ya simiotiki katika msimbo wa kiseme ambao unaendana na viashiria Fulani ambavyo hupelekea kuelewa sifa kamili ya jambo, jambo, jambo au muhusika Fulani.

Lugha ya mdokezo, aghalabu huwa na njia ambayo hutumika pale ambapo muhusika

hutumia maneno yasiyokuwa na ukamilifu wa kile kinachowasilishwa wakati wa mazungumzo na kumtaka msomaji ajalizie kifikra au hata kwa msikilizaji ambapo baadhi ya maneno hudondoshwa na kuacha alama ya desh desh = (---------------) katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* mifano ya lugha ya mdokezo yamejitokeza kama ifuatavyo:

> *OKELLO: (Anarukia, anamkaba koo na wakati huo huo Mfaranyaki na Ramadhani wanafika na kumsaidia… wanamnyonga…wantoroka).*
> *MTUMWA: ( analia kwa maumivu…anmsogelea maiti… Anashtuka….Sasa anamhurumia, anmlilia bwana wake ) Oh! Bwana wangu… Umekufa!? Watu wabaya wale. Sasa mimi nitaenda wapi? ( Machozi ) sasa nnitalala wapi? Nitakula wapi? Tumwa mie? ( anlia kwa majuto makuu. Polepole taa zinafifia…)*

Mifano yote hiyo ni miongoni mwa matumizi ya lugha mdokezo ambayo yamejitokeza katika Tamthiliya ya Muandishi “Emmanuel Mbogo.” Na kuonesha jinsi ya lugha ya mdokezo ilivyotumika kwa lengo la kuongeza vionjo mbali mbali kwa kuipamba lugha na kuvivuta fikra za msomaji kuwa karibu zaidi na msomaji kwa kujenga hisia juu ya matukio yanavyojitokeza. Vile vile inahusiana na nadhariya ya Simiotiki kwa msimbo wa kiishara anavyoihusisha msomaji anavyoweza kuvumbua maana ya kiishara.

#### 4.4.3.8 Mafumbo

Mafumbo ni miongoni mwa matumizi ya lugha kimafumbo zaidi kwa lengo la kuitumia lugha kwa kuficha kitu ndani yake ili kuepusha uwazi wa kinachozungumzwa. Katika Tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello* kuna baadhi ya mafumbo ambayo yamejitokeza ambayo ni kama hii ifuatayo:-

*OKELLO: Wale fisi maji ngulumbili wale wale walionyonga utu wetu wale mwisho wa ufisadi na ufisadi wao (UK:27).*
*OKELLO: Mama anguka ukamvika baba angu kidani cha kito kitakatifu shingoni (UK: 26).*
*OKELLO: Minyororo ya Muafrika inamfunga na kumnyonga muanfirka mwenyewe (UK:65).*

Kutokana na mifano hiyo tunapata mafumbo ambayo yamejitokeza kwa hali tofauti kupitia kurasa tofauti kama vile “Fisi maji ngulumbili” ambao wamefumbwa wale watawala wa kikundi cha Sultan naye mwenyewe “kidani kitakatifu shingoni “ambacho amevishwa baba wa Okello ni fumbo kwa wale waliokuwa wamemdharau hadi kumpandikiza chuki zaidi. Dhamira ya kutumia mafumbo ni kuzivuta fikra za msomaji kuwa na shauku ya kutaka kujuwa kinachoendelea. Lengo jengine ni kutaka kuonesha unyonge wa muhusika na uhusika wake. Utumizi wa mafumbo haya nayo pia inaendana na msimbo wa kiseme ambao uapelekea kuelewa sifa kamili ya kitu, jambo, tukio, au hali na kuhusisha na hali haalisi katika jamii husika.

#### 4.4.3.9 Mubalagha

Kwa mujibu wa Wamitila (2008)” balagha ni Sanaa ya usemaji na uzungumzaji.” ni mbinu inayotumiwa katika fasihi ili kuyakuza mambo kuliko yalivyo kawaida yake hii husaidia kuongoza maana au hata kuchekesha tu au kuburudisha. (Haji, 1992), katika Tamthiliya hii ya “Sadaka ya John Okello” tumepata baadhi ya misamiati inayoonesha kuwa ni sifa hizo za mubalagha kama hivi ifuatavyo:

*OKELLO: Hisia zikaumana, kiuzao zikakatika katika (UK:26).*
*MFARANYAKI: Mimi mwana wa nchumbiji, Mwana wa Nchumbiji akikohoa ardhi inachanika (UK:24).*

Kutokana na mifano hiyo tunaweza kuipata sifa hiyo ya kutumia mubalagha katika sentensi za muandizi zilizotumiwa na wahusika wake kama vile “Hisia zikaumana”

hapa hali ya Hisia ambazo ni za kimtazamo wa mtu na mtu zimepewa sifa ya kutenda tendo la kuuma/ Kugusana/Kuchukuana na kuwa sawa baina ya mtu mmoja na mwengine, pia kuna mubalagha nyengine ni ile ya kauli ya muhusika 'Mfaranyaki' kwa kusema, "Mwana wa Nchumbiji akikoho ardhi inachanika", hapa pia tunapata sifa ya mubalagha ambayo mtu kapewa uwezo zaidi wa kutenda kuliko kawaida na kuwa na nguvu za kikohozi . Dhamira ya kutumia vionjo hivi ni kuipamba lugha na kuiboresha na kuongeza mvuto wa kazi ya fasihi. Sambamba na hili tunapata msimbo wa kiishara ambao unahusisha jinsi wasomaji wanavyoweza kuvumbua maana ya kiishara katika kazi ya fasihi.

Kutokana na mchanganuo huu mtafiti amegunduwa kwamba muandishi huyu mahiri Profesa Emmanuel Mbogo katika tamthiliya zake hizi ambazo ni za miaka tofauti ambayo tamthiliya ya Fumo Liongo ni tamthiliya ya mwaka (2009|) ambacho kimesheheni tamathali za semi matumizi ya methali, lugha ya picha, lugha ya ishara, misemo, kejeli,kriri, mdokezo, tash-hisi, taharuki na tanakali sauti ni miongoni mwa vipengele ambavyo muandishi amevitumia sana na kuifanya kazi yake iwe na mvuto na iliyo nzuri kifani na kimaudhui na kwa upande wa tamthiliya ya Sadaka ya John Okello mwaka (2014) muandishi huyu huyu amesheheneza utomeaji wa vionjo mbali mbali vya lugha ambavyo vingi vyao vinafanana ikiwemo matumzi ya lugha ya picha, lugha ya shara,misemo, methali, takriri, tanakali sauti, tash-hisi, mdokezo na kejeli ni mingoni mwa matumizi ya lugha yanayoonesha kuwa yamejitokeza pande zote za tamthiliya teule ambazo kwazo kila kipengele kimetumika kwa ustadi wa hali ya juu.

Vile vile muandishi huyu kadiri miaka inavyosonga mbele ndipo anapokomaa na kubobea katika fani hii ya utunzi na kuingia na wingi wa vionjo vya lugha ambavyo kwa upande wa tamthilia hii mpya ambayo ni Sadaka ya John Okello ametomea tomea vionjo kama vile lugha ya mafumbo, methali, tashbiha na matumizi ya lugha mchanganyiko yamechukuwa nafasi ndani ya tamthiliya hii ambayo ni miongoni mwa muendelezo mzuri wa kuikuza na kuiendeleza lugha kwa ustadi wa hali ya juu. Hivyo kwa ujumla tamthiliya zote mbili zimechukuwa nafasi ya utumizi wa lugha katika muktadha stahiki unaofungamana na matukio na wahusika wake pamoja na nafasi zao kwa uhusika wao kisanaa zaidi.

## 4.5 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha uchambuzi wa data za utafiti kulingana na malengo ya utafiti wetu. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambapo lengo moja lilihusu kuchambua matumizi ya lugha katika tamthiliya teule na la pili lilihusu kubainisha dhamira katika tamthiliya teule. Data za utafiti zilizochambuliwa zimehusu malengo haya mawili.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii ya mwisho tutawasilisha muhtasari wa utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti huu. Mtiririko wa sehemu utakuwa kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza itahusu muhtasari wa utafiti, sehemu ya pili itahusu hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhutasari wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchambua matumizi ya lugha katika tamthiliya teule za Emmanuel mbogo. Tamthilia zilizolengwa zilikuwa ni Sadaka ya John Okello na Fumo Liongo. Malengo mahsusi yalikuwa ni kuchambua namna lugha ilivyotumika katika tamthiliya hizo pamoja na kuchambua dhamira zilizoibuliwa na matumizi hayo ya lugha. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba mwandishi ametumia vipengele tofauti vya lugha katika tamthiliya zake hizo mbili kama vile tamathali za semi, lugha ya ishara, lugha ya picha, takriri, mdokezo, tankali sauti na nyenginezo. Matumizi hayo ya lugha yalikuwa na dhamira tofauti kama vile kushajiisha ukombozi, kujenga umoja, kukemea usaliti, utabaka, umasikini, uongozi mbaya na kadhalika.

## 5.3 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, tunaweza kusema kwamba muandishi Emmanuel Mbogo amefanikiwa sana katika matumizi ya lugha ndani ya tamthiliya mbili hizi. Matumizi

bora ya lugha katika tamthiliya ndio yamezifanya tamthiliya hizi kuwa kazi za sanaa badala ya kuwa maandishi ya kuhistoria kama ilivyo kwa matukio yaliyomo katika kazi hizi.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na utafiti huu, mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:

Kwanza, mtafiti alifanya tu katika kipengele cha matumizi ya lugha, hivyo kuna haja ya kutanua utafiti katika vipengele vyengine ambavyo mtafiti hakuvigusia au hakuvifanyia uchambuzi zaidi kama vile ufasaha wa lugha teule, uwiyano wa lugha na wahusika na kadhalika.

Pili, kuna haja ya kufanyika kwa utafiti zaidi kuhusu kazi nyengine za fasihi za mwandishi huyu ili kuona umahiri wake katika Sanaa ya fasihi.

Tatu, kuwepo kwa mlingano na mtofautiano wa wasanii wa kitanzania katika kuiakisi lugha kisanaa kwa utomeaji wa lugha teule katika tafiti zijazo ili kuiboresha lugha ya Kiswahili.

Nne, kuwepo kwa tafiti za ana kwa ana baina ya mtunzi wa kazi ya fasihi na mtafiti ili kuipata ladha na azma ya mwanafasihi (msanii) kwa kujikita katika kuitumia lugha kwa ustadi wa hali ya juu.

Tano, kuna haja ya kutowa nafasi kwa wasanii chipukizi katika kuitumia nafasi yao ya kisanaa kwa kutunga kazi zao za kifasihi zenye kuimarisha utumizi wa lugha kwa kutumia maneno teule kwa kukuza kipaji na kuibua umahiri wa wasanii chipukizi.

Sita, kuwepo kwa mtaala wa elimu kupitia elimu ya msingi, sekondari na vyuo utakaozalisha wanalughawiya na wanafasihi kwa ujumla kwa jifunza na kutoa machapisho yatakayokuza vipaji vya wasanii wa kazi za fasihi wakiwa na umahiri wa kutosha kupitia lugha yao ya taifa kwa kuiboreza kitaalamu zaidi.

Saba, kuna haja ya serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viswani Zanzibar kushirikiana katika kuwapatia Tunzo maalum wasanii wakongwe wa nchini Tanzania kwa jitihada zao za kuielimisha jamii kwa kuibua wasanii chipukizi kupitia jitihada za wataalamu wao ambao ni Madaktari wa Elimu, Maprofesa na wahadhiri wanaotuwakilisha wtanzaia nje ya nchi kwa kuzisambaza au kusomwa kazi zao za fasihi.

Nane, kutokana na fani hii ya uandishi wa tamthiliya kazi nyengine za kifasihi unavyozingatia na kuijali lugha yetu ya taifa ni vyema tukajidhatiti katika kuiboresha kivitendo zaidi kwa kuitumia katika ufundishaji kwa ufasaha zaidi na kujiepusha na kuchanganya lugha kama inavyojitokeza kwa baadhi ya kazi za wasanii.

## MAREJELEO

Abass, M. A. (2015). Uchunguzi wa Tamthilia za Usemi Katika Kuibua Dhamira Katika Tamthilia: Ulinganishi wa Morani na Fumo Liongo. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili).

Babbie, E. (1999). *The basic of Reserch.* Belmont: Wadsworth.

Babie, E. (1998). *The Practice of Social Science Research*, (9th Edition), Belmont: New Age International.

Bakhresa, S. (1993). *Kamusi ya Manna ya Matumizi.* Nairobi: Oxford University Press.

Chum, H. (1994). Msamiati wa pekee wa kikao (kaespecific vocabulary), Hesinki: Hesinki University Print House.

Enon, J. C. (1998). *Educational Research, statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University Press.

Habwe, J. & Karanja P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phonix Publishers.

Haji, M. M. (2007). Sababu zinazopelekea utatanishi katika mmatamshi kwenye Lugha ya Kiswahili, Kisiwani Unguja. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. https:/Learning. Uombi.ac.ke/courses/BSW 103/scorm Packages s/path-2/sura- ya – 2 lugha – na – mazingira – yake. Html. Imepakuliwa tarehe 11/2/2016.

Jilala, H. (2008). “The Artistic Uses of Metaphors in constructing Meanings and Messages New Generation Songs in Tanzania” M.A Dissertation (Unpublished), University of Dar es Salaam, Tanzania.

Jilala, H. (2011). “Lugha na jinsia katika Ushairi: Uchunguzi wa sitiari za UKIMWI na Mapenzi katika Mashairi ya Bongo Fleva” Katika Toleo Maalumu La Muziki wa kizazi Kipya *Mulika*. Taasisi ya Taaluma Za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. 29, 55-68.

Juma, S. U. (2007). Matumiz ya Lugha katika Nyimbo za Uganga Zanzibar. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

K.W.Wamitila (2002) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Kenya Litho Ltd.

Khamis, A. A. (2013). *Uchambuzi halisi wa Matumiz ya Kiswahili Bungeni,* Dar-es Salaam: TUKI.

Kiango, D. (1992). “Taswira ya Mwanamke Katika Tamthiliya za Kiswahili za Kenya zilizochapishwa – Katika *Baragumu*, 1 na 2.” Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Maseno. (Haijachapishwa).

Kimai, N. & Rocha, C. (2008). *Ufundishaji wa fasihi, Nadharia na Mbinu,* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation,

Kothari, C. (2004). *Research Methodology*. New Delhi: New Age International Limited.

Ligembe, N. E. G. (1995). The Uses of metaphor in Penina Muhando’s Lina Ubani. A stylistic anlysis. M.A Dissertation, (Unpublished). University of Dar es Salaam, Tanzania.

Magumbi, P. J. M. (1982). Uhakiki wa Maudhui katika Tamthiliyta za Kiswahili za Kenya zilizochapishwa”. Tasnifu ya M. A. Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Masota, Z. M. (1993). “Maudhui katika Tamthiliya Nne za mwandishi Emmanuel Mbogo”. Tasnifu ya M.A Chuo kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Massamba na wenzake (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. (SAMIKISA) Dar-es-Salaam:.TUKI.

Mirikau, S. A. (2011). “Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za Wamitila K. W.” Tasnifu ya shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mponde, J. (2002). Uchambuzi wa Tamthiliya na ushairi. Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Muhammed, N. A. (2013). Matumizi ya lugha tandawazi katika simu za kiganjani. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Tanzania.

Muller, H. N. (1970). Statical Reasoning in Sociology. Boston: Hongton Mufflin Company.

Musyoka, F. M. (1996). Uhakiki wa Fani katika Tamthiliya za Jay Kitsao”. Tasnifu ya Uzamili Chuo kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa).

Nguta, (2011). Fani na Usawiri wa Kike katika Tamthiliya ya Pango na Mama ee.” Tasnifu ya shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu* Nairobi: Nairobi University Press.

Omar, I. M. (2011). “Education Research; Concept and Methods, Dar-es-Salaam: Delah Educational Publishers ltd.

Opie, C. (2004). *Doiing Educational Research,* London: SAGE Publication Ltd.

Ramadhan, S. (2005), Ulinganisho wa Sitiari katika Tamthiliya. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sarara, M. M. (1997). “Maudhui katika Tamthiliya za S.A. Mohammed”. Tasnifu ya M A. Chuo kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa).

Schutt, R. K. (2006). *Investigating the social world: The process and practice of research.* London: Sage Publications.

Sengo, T. S. Y. (2009). Sengo na Fasihi za Kiinchi. Dar es Salaam: AERA Kiswahili Researched Products.

Talcot, M. (2010). *Research: From Theory to Practice*. Apprentice Hall, Canada.

Too, M. (2011) “Matumizi ya lugha katika Tamthiliya ya Nguzo Mama” Tasnifu ya Uzamili, (haijachapishwa). Chuo kikuu cha Nairobi.

TUKI, (2004) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Kenya Oxford University Press.

Vartanian, T. P. (2011). *Secondary Data Analysis*, New York, Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya Kiswahili na Fasihi na Istilahi, Nadharia. Prof: Mulokozi, M. M., Da-es-salaam: Focus books.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wellington, S. (2000). *Educational Research, contemporary Issues and Practical Approaches.* London: Biddles Ltd.